ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	**-**	**SPIKA**
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma

		na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani

15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais
19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Mihayo Juma N'hunga	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa pili

		wa Rais wa Zanzibar/ Jimbo la Mwera
22. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ / Jimbo la Micheweni
23. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
24. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
25. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
26. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
27. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Naibu Waziri wa Uwezeshaji,Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake
28. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo,

		Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
30. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
31. Mhe. Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
32. Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil	-	Uteuzi wa Rais
33. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
34. Mhe. Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
35. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele
36. Mhe. Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi
37. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Nafasi za Wanawake
38. Mhe. Asha Abdalla Mussa	-	Jimbo la Kiwengwa
39. Mhe. Bahati Khamis Kombo	-	Jimbo la Chambani
40. Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-	Nafasi za Wanawake
41. Mhe. Hamad Abdalla Rashid	-	Jimbo la Wawi
42. Mhe. Hamida Abdalla Issa	-	Nafasi za Wanawake
43. Mhe. Hamza Hassan Juma	-	Jimbo la Shaurimoyo

44. Mhe. Hassan Khamis Hafidh - Jimbo la Welezo

45. Mhe. Hidaya Ali Makame - Nafasi za Wanawake

46. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa) - Jimbo la Mtoni

47. Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Paje

48. Mhe. Khadija Omar Kibano - Jimbo la Mtambwe

49. Mhe. Machano Othman Said - Jimbo la Mfenesini

50. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti - Jimbo la Mtopepo

51. Mhe. Makame Said Juma - Jimbo la Kojani

52. Mhe. Maryam Thani Juma - Jimbo la Gando

53. Mhe. Masoud Abrahman Masoud - Jimbo la Bububu

54. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Jimbo la Chumbuni

55. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha - Jimbo la Mtambile

56. Mhe. Mohamed Said Mohamed - Jimbo la Mpendae

57. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini

58. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini

59. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake

60. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole

61. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani

62. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake

63. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake

64. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani

65. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani

66. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni

67. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde

68. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake

69. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Jimbo la Magomeni

70. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Nafasi za Wanawake

71. Mhe. Said Omar Said - Jimbo la Wingwi

72. Mhe. Said Hassan Said - Mwanasheria Mkuu

73. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma - Nafasi za Wanawake

74. Mhe. Salma Mussa Bilal - Nafasi za Wanawake

75. Mhe. Shaib Said Ali - Jimbo la Chonga

76. Mhe. Simai Mohammed Said - Jimbo la Tunguu

77. Mhe. Sira Ubwa Mamboya - Uteuzi wa Rais

78. Mhe. Suleiman Makame Ali - Jimbo la Ziwani

79. Mhe. Suleiman Sarahan Said - Jimbo la Chakechake

80. Mhe. Tatu Mohamed Ussi - Nafasi za Wanawake

81. Mhe. Ussi Yahya Haji - Jimbo la Mkwajuni

82. Mhe. Viwe Khamis Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
83. Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Nafasi za Wanawake
84. Mhe. Yussuf Hassan Iddi	-	Jimbo la Fuoni
85. Mhe. Zaina Abdalla Salum	-	Nafasi za Wanawake
86. Mhe. Zulfa Mmaka Omar	-	Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem	-	Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Kumi na Sita - Tarehe 30 Mei, 2017

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti (Mwanaasha Khamis Juma) alisoma Dua

TAARIFA YA SPIKA

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe katika Kikao cha Baraza cha tarehe 23 Mei, 2017 Mhe. Hamida Abdalla Issa aliuliza swali la nyongeza kwa Wizara ya Fedha na Mipango na kuahidiwa kujibiwa kwa maandishi.

Katika kutimiza masharti ya Kanuni ya 40(4) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2016, Wizara hiyo imeleta majibu kama Waziri wa Wizara hiyo alivyoahidi. Sasa namuomba Waziri wa Fedha na Mipango asome jibu la swali la nyongeza alililoulizwa na Mhe. Mjumbe huyo. Mhe. Waziri tafadhali.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti,katika Mkutano wa Sita wa Baraza la Wawakilishi, Kikao cha tarehe 23, Mei 2017 wakati ninajibu swali Namba 29, lililoulizwa na Mhe. Abdalla Maulid Diwani, juu ya kusimamishwa kwa baadhi ya watendaji wa Wizara yangu kutokana na ubadhirifu wa fedha niliahidi kujibu swali la nyongeza la Mhe. Hamida Abdalla Issa, swali hilo la nyongeza lilikuwa linauliza kwamba ni kiasi gani cha fedha kilichorudishwa na watendaji ambao walihusika na ubadhirifu wa fedha za Serikali.

Mhe. Mweyekiti, jibu la swali hilo la nyongeza ni kama ifuatavyo:-

Kati ya Watendaji waliohusika na Bodi kuridhishwa na kuhusika kwao, Washika Fedha wawili (2) ambao walikiri mbele ya Bodi ya Uchunguzi kwamba baada ya kuvunja Hundi walizokabidhiwa, walipewa fedha taslimu kati ya fedha za Hundi walizozivunja. Malipo hayo ni kama hivi ifuatavyo:-

1) Mmoja alipewa TZS 6,000,000/- alikiri kupokea fedha hizo na yeye alikubali na kurejesha fedha hizo zote tarehe 21/10/2016.

2) Mwengine alipewa 16,000,000/- alikiri kupokea fedha hizo na amerejesha TZS. 2,000,000/- tarehe 27/10/2016.

Hivyo, jumla ya fedha zilizorejeshwa hadi sasa ni TZS 8,000,000/-
Naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Fedha. Katibu

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 57

Utaratibu Unaotumika kwa Viongozi Kufika Zanzibar

Mhe. Simai Mohamed Said - Aliuliza:

Katika miaka ya karibuni tumeona kuwa viongozi wa kitaifa kutofika Zanzibar.

Je ni utaratibu gani unaotumika kuwakumbusha wenzetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania juu ya jambo hili.

(Mhe. Mjumbe aliyetaka kuuliza swali hili ameliondoa)

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Mwenyekiti kwa heshima kabisa naomba swali langu katika orodha ya kazi za leo kwa sababu katika mchango alipotoa Ofisi ya Makamu wa Pili alitoa majibu ya kina. Kwa ushauri tu basi naomba kila baada ya muda tuweze kupata maelezo juu ya masuala ya viongozi wakuu wanaokuja Kitaifa kufika hapa Zanzibar mbali ya kuja pande zote za muungano. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Waziri wa Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Simai Mohamed Said: Mhe. Mwenyekiti, nimeliondoa swali langu.

Mhe. Mwenyekiti: Aah! umeliondoa.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ninachoomba tu basi Afisi ya Makamu wa Pili tuweze kupata majibu au maelezo kila baada ya muda kuhusiana na Viongozi Wakuu wanapokuja kutembelea Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Mwenyekiti: Haya ahsante sana Mhe. Simai Mohammed, Katibu kwa Wizara inayofuata. Nakuona Mhe. Ali Suleiman (Shihata) kwa niaba.

Nam. 93

Mapato Yanayokosekana Baada ya Kuvunjwa Maduka Darajani

Mhe. Ali Suleiman Ali (Kny: Mhe. Jaku Hashim Ayoub) – Aliuliza:

Mhe. Mwenyekiti,ni kipindi kirefu kimepita tokea maduka ya makontena ya Darajani kuondolewa kupisha ujenzi mpya wa eneo la biashara la Darajani *(Darajani Coridoor).* Hata hivyo, hatua za ujenzi huo zimekuwa bado kuanza kwa kile kinachoonekana Serikali haijawa tayari kujenga sehemu hiyo.

(a) Tokea kuvunjwa kwa maduka ya Makontena ni kiasi gani cha mapato ambayo Serikali imepoteza.

(b) kama mpango wa kujenga upya eneo hilo haujawa tayari, kwanini Serikali imeharakisha kuvunja maduka ya makontena.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, (OR), Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ – Alijibu**:**

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 93 lenye vifungu (a) na (b)

Mhe. Mwenyekiti, kabla sijamjibu Mhe. Mwakilishi naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba kukiri kwamba mtazamo juu ya mradi wa uendelezaji wa ukanda wa biashara ya Darajani unaonekana kuchukua kipindi kirefu kuanza tokea pale yalipoondolewa maduka ya makontena. Aidha nakiri pia kuwa

hali hii inakuja ikiwa ni kinyume cha matarajio ya wananchi kwa ujumla ambapo walikuwa na shauku kubwa ya kuona mabadiliko hasa ya miundombinu katika eneo lile.

Mhe. Mwenyekiti, taarifa ya hatua zinazoendelea kuchukuliwa katika mradi huu zimekuwa zikitolewa na Serikali katika vyombo vya habari kupitia Waziri wa Nchi, (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ. Kamati Maalum ya Wataalamu iliyoundwa na Serikali nayo imekuwa ikitoa taarifa juu ya hatua zinazoendelea kuchukuliwa.

Mhe. Mwenyekiti, eneo la Darajani limo katika Hifadhi ya Mji Mkongwe ambapo ni sehemu ya Urithi wa Dunia. Hivyo basi uendelezaji wowote katika eneo hili unafanyika kwa tahadhari kubwa na mazingatio ya Sheria zikiwemo za Uhifadhi na Mazingiria, Miongozo na Mipango ya kuuendeleza Mji wa Zanzibar pamoja na ushirikishwaji wa wahusika mbali mbali. Kwa mantiki hiyo, kuchelewa huku hakutokani na ama kwa kuzembea au kwa sababu nyengine yoyote ile ambayo ingemaanisha kukosekana kwa umakini wa serikali katika kulisimamia jambo hili.

Mhe. Mwenyekiti, hata hivyo hatua kadhaa kwa upande wa serikali zimekuwa zikichukuliwa zikiwemo kupokea michoro ya awali ya ujenzi, kupokea rasimu ya kwanza ya tathmini ya kimazingira, kijamii na kiuhifadhi, kufanyika mawasiliano na Shirika la *UNESCO* ambalo hatimae litatoa maoni yake juu ya mradi huo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu kama ifutavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, eneo la Darajani lilikuwa na idadi ya wafanyabiashara 258 ambao kwa pamoja walipaswa kulipa Manispaa ya Mjini jumla ya Shs.68,460,000.00 kwa mwaka. Kati ya fedha hizo Shs.43,200,000.00 zinatokana na malipo ya leseni na Shs.25,260,000.00 zinatokana na ada ya huduma *(service charge).* Katika mwaka huu 2017 zaidi ya asilimia thamanini ya wafanyabiashara hawa wanaendelea na biashara zao sehemu nyengine. Hivyo Baraza linaendelea kukusanya malipo ya leseni kama kawaida. Hata hivyo sehemu kubwa ya mapato iliyokosekana ni yale yanayotokana na ada ya huduma za usafi.

(b) Mhe. Mwenyekiti, uondoshwaji wa makontena eneo la Darajani ilikuwa ni utekelezaji wa amri ya Mahkama sambamba na azma ya Serikali kuliendeleza eneo hilo. Ni dhahiri kwamba eneo kama la Darajani hatua ya kulipima kitaalamu ilikuwa ni ya mwanzo na ya lazima ili kupata taarifa zote muhimu zinazohitajika. Zoezi hili la upimaji lisingewezekana kama makontena yale yangeendelea kuwepo mahali pale.

Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, (OR), Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kutokujibu au kutokidhi swali la msingi kama nilivyouliza na Kanuni zetu zinatukataza ya 59 (3) na sina haja ya kuisoma lakini nimwambie kabla ya kujibu Mawaziri na Manaibu Waziri, Bosi wetu alitueleza tufanye utafiti kwanza kabla ya kujibu maswali humu ndani, wewe mwenyewe ulikuwa shahidi tulipoyazungumza hatuna haja ya kurudia.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim Ayoub uliza swali la nyongeza.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Serikali kwanza imesema uwongo mapato ya milioni 68 ni pesa kidogo sana, pesa zilizopotea hapa zaidi ya bilioni. Ukitaka ushahidi wa huo niko tayari kukupa ushahidi. Mtu mmoja tu ana makontena sita, saba. Maduka hayo yana makontena mangapi. Kwa hili jawabu hujajibu swali la msingi kabisa ndugu yangu ukiri.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kuna majengo yaliyovunjwa kama Sinema Malindi, *Park Hyatt* sura za mbele zimebaki vile vile ni Sheria za Mji Mkongwe, leo inakuwaje. Kipi kinachokuja mwanzo kati na mchoro na ramani. Hadithi hiyo unataka kuniambia kuku na yai lipi linalokuja mwanzo. Mheshimiwa sina hata cha kumuuliza naona bora nimuache arudi akae kitako hapa.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima zote kwanza nataka afute kauli yake. Kwanza ametumia vibaya kifungu cha 59(6) cha kumtaja kiongozi wetu wa Nchi kwa dhihaka.

Mhe. Rais kweli anasisitiza kwamba Mawaziri tunapokuja Baraza la Wawakilishi tufanye utafiti kwanza ndipo tujibu maswali. Nataka nilihakikishie Baraza hili la Wawakilishi kwamba suala hili tumelifanyia utafiti na ndio maana tumekuja na jibu. Tungekuwa hatujafanya utafiti wala tusingekuja na jibu Barazani.(*Makofi*).

Lakini jengine kwa mujibu wa Kanuni ya 58(5) ni hisani yetu tu kama Serikali kuendelea kutoa taaluma juu ya jambo hili. Lakini Kanuni ya 58(5) inakataza suala ambalo limezungumzwa na likapata majibu na Spika akahoji Baraza, wakaridhia kutokurejewa tena suala hilo. Kwa hivyo sisi swali ambalo tumelijibu tumefanya utafiti na ndio maana tumekuja hapa. Lakini ile kumtaja Mhe. Rais kila wakati kwa jambo ambalo halina uhakika, nadhani hili hatuitendei haki Serikali. Sisi tumefanya utafiti na ndio maana tumekuja na jibu.

Mhe. Mwenyekiti, kiti naomba kichukue hatua ahsante sana.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru sana Mhe. Waziri...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim Ayoub sijakuruhusu. Mhe. Jaku ulikuwa una swali la nyongeza lakini hukuonesha lile swali la nyongeza isipokuwa ukasimamia vifungu vya Kanuni yetu kuhusiana na jawabu uliyopewa.

Lakini na Mhe. Waziri ametoa ufafanuzi na yeye amekusikiliza kwa makini kutokana na hilo umevunja hiyo Kanuni. Kwa hivyo naomba tu uombe radhi tuendelee.(*Makofi*).

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, mimi nimechaguliwa na wananchi ninachokizungumza sibahatishi, tuwe makini humu.

Mimi nina duka ambalo jamaa pale analeta kontena sita kwa mwezi mmoja karibu, twambie mapato haya shilingi ngapi kwa *TRA*. Mhe. Mwenyekiti, unajua ukijenga hoja, jenga na ushahidi, usije tu ukakurupuka humu. Mimi suala la kuomba radhi, nije

nimpe darasa nimuelimishe ndiyo nilichosema mimi, elimu yangu ndogo, sijapata Uwaziri na Unaibu Waziri, lakini milioni 68 huu ni mlango mmoja tu wa duka.

Mhe. Mjumbe Fulani: Mhe. Mwenyekiti....

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku nakuomba kidogo.

Taratibu zipo kama jawabu halijakuridhisha lakini umejibiwa kwa vile wao wamesema wamefanya utafiti. Kwa hivyo kama wamefanya utafiti na jawabu imeletwa hapa haikukuridhisha, inaonekana labda na wewe ulikuwa na jawabu yako mfukoni. Kwa hivyo nilikuwa nakuomba jawabu iliyotoka kwa serikali tayari wameshakupa jawabu na kama hujaridhika na jawabu fuata taratibu zile nyengine ambazo tunazo katika Kanuni zetu.(*Makofi*).

Kwa hivyo taratibu zile utakapozifuata basi utaendelea na kutoridhika na hiyo jawabu, lakini nilikuwa sitaki tena kuruhusu hilo jambo nijirejee.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub naomba uombe radhi kwa hiyo kauli uliyoizungumza.(*Makofi*).

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Niombe radhi kwa suala ambalo liko wazi.

Mheshimiwa unavyotaka kuamua amua, wewe ndiyo Mwenyekiti wasikuendeshe Mawaziri, tupo hapa kwa niaba ya wananchi. (*Makofi*).

Hapa juzi Mhe. Haji Omar Kheri alibabaika hapa kwenye bajeti yake. Mimi hili naapa kwa Mungu siombi radhi, naapa kwa Mungu siombi radhi, kitu ushahidi. Wewe unaendeshwa na Mawaziri. (*Makofi*).

Sisi tupo hapa kuitetea serikali. Juzi hapa Mhe. Haji Omar Kheri anatetemeka kwenye bajeti yake hapa, akataka ushahidi nikatoa ushahidi. Sasa usiyumbe na kiti hicho. Wewe kama unataka kunihukumu Ramadhani hii nitoe nje niondoke tu mimi. Hoja naisimamia kwa ushahidi na Mwenyezi Mungu shahidi....(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim, uombe radhi kwa mujibu wa kauli uliyoitoa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Hii ni Ramadhani mimi namuogopa mmoja tu Mheshimiwa kitu kipo wazi. Mhe. Mwenyekiti, unayumba kwa kiti, kitu kiko wazi.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim tatizo, nimekuona Mhe. Mohammed Said Mohammed kuhusu utaratibu lakini ngoja tuwekane sawa kwanza na hili.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim ninachokisema mimi hapa kuwa wewe hukuridhika na jawabu na kauli uliyoitoa kuwa Mawaziri hawajafanya utafiti. Sasa Waziri amesema kuwa amefanya utafiti ndio maana wakaja na hilo swali. Kwa maana hiyo wewe umetamka neno ambalo silo kwa mujibu ya Kanuni yetu, ndiyo maana nikakwambia uombe radhi kwa hilo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, mimi nilichokwambia kwamba jawabu silo, niko tayari nimuelimishe.

Mhe. Mwenyekiti: Baada ya kuomba radhi halafu hilo jawabu lililokuwa silo utafuata utaratibu. Kuhusu utaratibu Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa).

UTARATIBU

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii lakini nimesimama kwa Kanuni ya 63 nikitilia mkazo sana Kanuni aliyeizungumza kaka yangu Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.

Hii Kanuni ambayo yeye ameitaja haihusiani kabisa na neno ambalo amelizungumza Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Mhe. Jaku Hashim amem-*quote* Mhe. Rais kwa kila siku kwa lile jambo ambalo analisema. Jambo ambalo analisema ni Waheshimiwa Mawazini na Manaibu Mawaziri watujibu majibu kwa ufasaha, hakusema jibu baya. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, kwa maana hiyo ukiendelea kumwambia aombe radhi hutomtendaa haki kwa sababu amewakilisha wananchi wa Paje. Na si vyema Waheshimiwa Mawaziri kutumia vifungu ambavyo sivyo na kusema watu waombe radhi si vyema. Mhe. Mwenyekiti muongozo wako. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe nakuombeni sana. Sasa itabidi na mimi nitumie Kanuni hii hii inayoniruhusu kuwa na mimi nitoa maamuzi nikiwa kama kiti hapa mbele.

Waheshimiwa Wajumbe wote nimekueleweni na *concern* zenu zimezipokea, kwa hivyo naomba tuendelee. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe tunaendelea swali la pili na nyongeza litaulizwa nakuona Mhe. Hamida Abdalla Issa.

Mhe. Hamida Abdalla Issa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti kwa kuniona nimesimama kumuuliza Mhe. Waziri pamoja na majibu yake mazuri aliyoyatoa na mimi nina swali moja na nyongeza lenye kitoto (a) na (b).

Kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri amekiri kwamba kuna uendelezwaji wa eneo hilo na tayari kuna michoro ambayo ipo, naomba kumuliza swali

(a) Ni kiasi gani cha fedha kilichopatikana kwenye *BOQ* ya michoro hiyo kwa hatua ya awali.

(b) Ujenzi huo ambao unataka kufanya katika eneo hilo unatatumia fedha za Serikali au kuna *financial* ambaye atauendeleza. Ahsante sana

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri kwa majibu haya.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Eeeh**!**

Mhe. Mwenyekiti: Kwa jawabu la alilouliza Mhe. Hamida.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Eeh! ndio.

Mhe. Mwenyekiti kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Hamida swali lake la nyongeza lenye (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Suala la gharama gani kwenye *BOQ* ambazo zimepatikana, kwanza kama tulivyojibu suala mama kama amelisikia vizuri kwamba tumepokea michoro ya awali na kama tumepokea michoro ya awali bila shaka hatua za kuanza na *BOQ* zitakuwa bado hazijafikia.

(b) Mjenzi gani anataka kujenga mpaka sasa hatujaweza kumpata mjenzi kwa sababu hatujamaliza *process* mpaka itakayotupelekea katika kutengeneza *Tender Document.* Kwa hivyo hatujawa na mjenzi mpaka sasa hivi. Ahsante sana

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mheshimiwa nakuona Mhe. Viwe kwa swali la mwisho la nyongeza.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Ahsante Mhe. Mwenyekiti na mini kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo lenye kitoto (a) na (b).

Mhe. Waziri hivi karibuni tuliona eneo la makontena Michenzani eneo lile limevunjwa na wafanya biashara wale wameondoshwa na wafanya biashara wale waliomba ili Serikali wawastahamilie waweze kumaliza mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani.

(a) Je, ni lini ujenzi ule utandelea katika maeneo yale ya Michenzani.
(b) Wafanyabiashara wale mmewapeleka wapi ili kuendelea kufanya biashara zao na tukiangalia wafanyabiashara wale wengi wao ni wanawake.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (OR), Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba niendelee kumjibu Mhe. Mwakilishi Viwe Khamis Abdalla.

Mheshimiwa alitaka kujua ni wapi ambapo katika jibu (b) ni wapi maeneo wafanya biashara ambao wameondolewa katika maeneo ya Michenzani wapi ambapo wamepelekwa kufanya biashara zao.

b) Mhe. Mwenyekiti, baada ya uvunjaji wa maeneo yale pale kukamilika wafanyabiashara wale ilikuwa tayari Serikali ilishakuwa tayari kutenga eneo ambao ilikuwa wao walitakiwa wafanya biashara hao waende kuendeleza biashara zao katika la Kinazini ambalo ni sehemu maalum zilitayarishwa kwa ajili ya wafanya biashara wale.

a) Kuhusu maombi ambayo wafanyabiashara wale waliweza kuomba ili waendeleza biashara zao baada ya kumalizika mwezi Mtukufu wa Ramadhani kuondoka, naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi kwamba matangazo na maagizo mbali mbali yalikwisha kufanyika na maamuzi yalikwishafanyika mapema, na kazi kubwa iliyokuwepo walitakiwa wale wafanyabiashara kundoka katika maeneo yale ambayo tarehe maalum ilipangwa na ilitolewa na wakashauriwa.

Lakini kwa bahati nzuri vile vile katika kutekeleza amri hiyo pia ilichelewa na hatimaye pia wafanyabiashara wale kwa muda ulipofika sasa wa kutaka kuchukuliwa hatua zile ambazo ni za ziada Mheshimiwa wafanyabiashara wale waliweza kuondoka na kwa muda ambao umepangwa ndiyo maamuzi ambayo ya Serikali ilikwisha yazingatia na haikuwa na lengo ya kuwakomoa wafanyabiashara wale.

Nam. 60

Kuimarishwa kwa Eneo la Fukwe la Nyuma ya Ikulu Zanzibar

Mhe. Simai Mohammed Said - Aliuliza**:**

Kwa kuwa eneo la fukwe nyuma ya eneo la Ikulu Zanzibar, lina mandhari ya sura ya mapumziko na kuvutia.

Ni lini Serikali itaandaa utaratibu wa kuboresha eneo hilo kwa ajili ya tafrija ya wageni wa Mhe. Rais pamoja na viongozi wa Kitaifa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi - Alijibu**:**

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Simai Mohamed Said swali lake Nam. 60 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba nikubaliane na Mhe. Mwakilishi kuwa eneo la fukwe lililopo nyuma ya Ikulu ya Mnazi Mmoja mjini Zanzibar ni lenye mandhari ya kuvutia sana. Hata hivyo, eneo la Ikulu kwa maana kwamba majengo ya Ikulu yana kumbi na maeneo ya kutosha kwa ajili ya tafrija za wageni wa Mhe. Rais pamoja na viongozi wa Kitaifa na wa Kimataifa.

Kutokana na hali hiyo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haijaona haja ya kuandaa utaratibu wa kulitumia eneo hilo kwa ajili ya tafrija za wageni wa Mhe. Rais pamoja na viongozi wa Kitaifa na wa Kimataifa.

Nam. 125

Ukaguzi Kwa Afisi Ya Mdhibiti Na Mkaguzi Mkuu Wa Hesabu Za Serikali

Mhe. Abdalla Maulid Diwani – Aliuliza**:**

Pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Afisi ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (*CAG*) lakini bado kumekuwa na manung'uniko kutoka sehemu mbali mbali za nchi yetu ya kutofanya kazi kama ilivyoelezwa na taratibu husika za ukaguzi.

a) Je, Taasisi ya CAG inakaguliwa na Kampuni gani.

b) Je, kwa kipindi cha miaka 10 iliyopita, *CAG* imekaguliwa mara ngapi.

c) Je, ripoti za Ukaguzi wa afisi hii zimewahi kujumuishwa kwenye ripoti za ukaguzi zinazowasilishwa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Naibuu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora – Alijibu**:**

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Abdalla Maulid Diwani swali lake Nam. 125 lenye kifungu (a), (b) na **(**c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi naomba kutoa maelezo yafuatayo:

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (*CAG*) inafanyakazi zake kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na taratibu za ukaguzi tulizojiwekea. Aidha, Ofisi hii imekuwa ikihakikisha kwamba viwango vya ukaguzi vya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa vinavyotolewa na jumuiya na

taasisi za ukaguzi za Kitaifa, Kikanda na Kimatifa vinafuatwa na kutekelezwa ipasavyo na Ofisi hii.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo naomba sasa kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la msingi kama ifuatavyo:-

a) Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (*CAG*) imekaguliwa na Shirika la Taifa la Ukaguzi la Tanzania - *(Tanzania Audit Corporation (TAC).*

b) Kwa kipindi cha miaka kumi (10) iliyopita *CAG* imekaguliwa mara tisa (9) kama ifuatavyo:-

1).Hesabu za 2007/2008
2).Hesabu za 2008/2009
3).Hesabu za 2009/2010
4).Hesabu za 2010/2011
5).Hesabu za 2011/2012
6).Hesabu za 2012/2013
7).Hesabu za 2013/2014
8).Hesabu za 2014/2015
9).Hesabu za 2015/2016 - ukaguzi bado unaendelea.

c) Ripoti za ukaguzi wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zinawasilishwa Serikalini kwa mujibu wa taratibu za kisheria na ni mashahidi tu kwamba hivi karibuni pia ripoti hiyo ililetwa katika Baraza letu hili la Wawakilishi. Ahsante

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri swali la nyongeza lina (a) na (b)

(a) Mhe. Waziri amezungumza kwamba Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zimewasilishwa Serikalini kwa mujibu wa kanuni na utaratibu. Je, ni sheria gani na ni kifungu gani naomba nielezwe.

(b) Kutokana kwamba hakuna aliye juu ya sheria katika hili, taratibu za Serikali ziko chini ya sheria na tumeona ukaguzi mbali mbali za taasisi ya Serikali zinaletwa ndani ya Baraza la Wawakilishi. Je, kwa nini ukaguzi wa *CAG* bado haujaletwa Barazani.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Tatizo ya mbele sikuwahi kuyapata sikuweza kuyapata

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana umesema kwamba Ripoti ya Ukaguzi wa Ofisi Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali inawasilishwa Serikalini kwa mujibu wa taratibu za kisheria. Swali langu nataka kujua ni sheria gani na kifungu cha ngapi kinapolekea hiyo ambayo ripoti kuja Serikalini. Kwa hivyo ripoti zote za ukaguzi zinakwenda Serikalini lakini baadae zinakuja kwenye Baraza, lakini hii bado haijaja na swali langu liko hapo.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Samahani Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Abdalla Maulid Diwani swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, ameuliza ni sheria gani na kifungu gani ambacho *CAG* kinampa mamlaka ripoti hiyo kuipeleka Serikalini

halikadhalika vile vile kuletwa hapa katika Baraza letu la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba ninukuu Katiba yetu ya Zanzibar ya mwaka 1984. Kwa hivyo tunajua kwamba Katiba ni Sheria Mama. Hivyo Sheria zote zinakuwa ziko chini ya Katiba yetu hii. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, naomba kunukuu.

Mhe. Mwenyekiti, niwaombe Waheshimiwa wende moja kwa moja katika kifungu cha 112 ambacho kinazungumzia Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, lakini niwachukue moja kwa moja katika kifungu 112 (5), naomba kunukuu.

112(5) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atawasilisha kwa Rais kila taarifa atakayotoa kwa mujibu wa masharti na kijifungu cha (3)(c) cha kifungu hiki. Baada ya kupokea taarifa hiyo Rais atawaagiza watu wanaohusika wawasilishe taarifa hiyo kwenye kikao cha kwanza cha Baraza la Wawakilishi kinachofanyika baada ya Rais kupokea taarifa hiyo na itabidi iwasilishwe katika kikao hicho kabla ya kupita siku saba tangu siku ile kilipoanza kikao hicho. Iwapo Rais hatachukua hatua za kuwasilisha taarifa hiyo kwenye Baraza la Wawakilishi basi Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atawasilisha taarifa hiyo kwa Spika wa Baraza la Wawakilishi au Naibu Spika ambaye atawawilisha taarifa hiyo kwenye Baraza la Wawakilishi.

Mwisho wa kunukuu.

Mhe. Hamida Abdalla Issa: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza swali moja na nyongeza.

Kwa kuwa umekiri kwamba ukaguzi wa Ofisi ya *CAG* unafanyika kwa kila mwaka wa fedha na kwa kuwa ukaguzi wowote unaofanyika wa Wizara na Taasisi za Serikali ripoti yake hupelekwa kwa Kamati ya *PAC* kwa niaba ya Baraza.

Je, ni lini sasa ripoti hiyo itakabidhiwa kwa Kamati ya *PAC* ili kuweza kuifanyia kazi.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako kumjibu Mhe. Hamida swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, ripoti hii italetwa Barazani mara tu taratibu zitakapokamilika.

Nam. 85

Usumbufu Usiokwisha Kwenye Matumizi ya Mashine za Kutolea Fedha (*ATM*)

Mhe. Ali Suleiman Ali (Kny: Mhe. Jaku Hashim Ayoub) - Aliuliza**:**

Utaratibu wa kuanziasha na kueneza mashine za kutolea fedha (ATM) kwa Benki zetu mbali mbali hapa nchini, hasa Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) na Divisheni yake ya Tawi la Kiislamu, ni wa kupongezwa na unapaswa kuendelezwa ili kuwapunguzia usumbufu wateja. Hata hivyo, pamoja na hatua hizo bado kumekuwa na usumbufu wa mashine hizo kutoa huduma hasa inapofika kipindi cha mshahara mwisho wa mwezi, nyakati za sikukuu na siku za mapumziko usumbufu unakuwa mkubwa zaidi.

Mara nyingi katika nyakati hizo mashine huwa zinazima au hazina fedha au mtandao haupatikani.

(a) Kwanini tatizo hili limekuwa endelevu, halirekebishwi na kutafutiwa suluhu ya kudumu.

(b) Kwanini wakati mashine zinapogoma na wananchi kukimbilia kupanga foleni benki ndani ili wapate fedha, wanakatwa fedha zaidi za kutolea wakati kosa la kutopatikana huduma ya ATM siyo lao, Je huu siyo mpango wa benki kujipatia fedha zaidi kwa ujanja.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango - Alijibu**:**

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kujibu swali namba 85 la Mhe. Jaku Hashim Ayoub naomba kutoa maelezo yafuatayo:

Kutokana na maendeleo ya teknolojia, benki duniani kote zimefanya mabadiliko makubwa ya utoaji wa huduma zake kwa huduma nyingi zaidi kutolewa kwa kutumia teknolojia ama kupitia mashine za utoaji fedha (*ATM*) au kupitia mitandaoni *(Online banking),* na hata kwa kutumia simu za mikononi. Ili kutolewa kwa ufanisi huduma hizo zote zinahitaji mfumo maalum na wenye ufanisi wa kompyuta *(core banking system)* ambayo ukubwa wake hulingana na idadi ya wateja. Huduma pia zinahitaji kuwa na umeme wa uhakika, sambamba na kuunganishwa na Kampuni ya Mawasiliano inayoaminika.

Tokea mwaka 2006 *PBZ* imeanza kutumia mfumo wa kompyuta kutoa huduma tofauti, wakati huo ikiwa na wateja wasiozidi elfu hamsini.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sasa *PBZ* ina wateja zaidi ya laki mbili na bado huduma za umeme na mawasiliano hazijafikia kiwango cha uhakika wa masaa 24. Aidha, matawi ya benki yameongezeka hadi 14 na vituo vinne (4) vya huduma wakati watumiaji wasiokuwa wateja wa benki wameongezeka katika huduma za kulipa mapato ya serikali na kulipia ada za skuli binafsi mbali mbali na hivyo mfumo wa benki nao umezidiwa na wateja.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu swali nambari 85 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

(a) Tatizo la *ATM* sio endelevu, kwani panapotokea tatizo benki hutafuta chanzo chake na kuwasiliana na mamlaka husika katutua tatizo lililopo. Benki ya Watu wa Zanzibar inakusudia kubadili "*Core Banking System*" ili kuhimili ongezeko kubwa la miamala na wateja.

(b) Benki zote hutoza ada kwa huduma inazozitoa, zikiwemo za matumizi ya *ATM*. Hata hivyo, ada zinazotozwa kwa wateja wanaopata huduma ndani ya benki hazihusiani na matumizi ya *ATM* ambayo pia yanatozwa ada. Ada zote za *PBZ* (*Tarriff*) zimebandikwa katika matawi yote ya benki.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali la nyongeza.

Kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa dhati kabisa kwa majibu yake mazuri na ya utulivu kabisa. Lakini pili nizipongeze benki zetu *PBZ* kwa ongezeko wa wateja wake mpaka kufikia 200,000 na kuendelea, hilo ni suala la kupigiwa mfano.

Pamoja na taratibu zote zinazoendelea sasa hivi mishahara yote inapokelewa katika benki, siku za mwisho wa mwezi pa kuweka mguu huna, ukienda Mwanakwerekwe, Darajani, Forodhani, *Mao-Tse-Tung,* Mazizini na kwengineko.

Je, Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri hivi sasa haoni kama kuna haja kwamba benki zetu hizi zikaenea sehemu mbali mbali Wilayani ili kuondoa tatizo hili. Maana mtu akikosa Mjini aende zake Wilayani akapate pesa kwa urahisi. Kwa mfano maeneo mengi tu sasa hivi, ukienda Nungwi, Mahonda, Micheweni na kwengine. Waziri ana mpango gani wa kulitafakari hili ili tuondoe usumbufu katika nchi yetu.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo.

Ni kweli wateja wameongezeka na mahitaji yameongezeka, na kutokana kwa kuongezeka huko kama nilivyosema kwenye jibu mama kwamba Benki ya Watu wa Zanzibar inataka kubadilisha ile *Core Banking System* yake ili kuhimili wateja wengi zaidi. Lakini pamoja na hilo wana mpango wa kuongeza *ATM* na katika kipindi cha hivi karibuni wanaongeza *ATM* nne katika vituo vya Mahonda, Chwaka, Paje, Saateni JKU. (*Makofi*).

Kadri hali itakavyoendelea na mahitaji yatakavyoongezeka basi pia haja ya kuanzisha vituo vyengine nayo itaonekana na kuchukuliwa hatua. Kwa hivyo tunaongeza *ATM* ili kutoa huduma zaidi, lakini pia tunaongeza *plat form* ili kuhimili wateja wengi zaidi, lakini vile vile benki hii itaangalia kwa vigezo ambavyo inavyo vya miundombinu iliyopo katika eneo, lakini na wateja waliopo katika eneo ili kuongeza vituo kwa ajili ya kuondoa usumbufu na matatizo yaliyopo.(*Makofi*).

Mhe. Zulfa Mmaka Omar: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mhe. Waziri hivi juzi serikali imetoa tangazo la watu wote ambao wanalipia baadhi ya vitu kama zile *road license* pesa zile kulipia kwa njia ya benki. Na tunaona kwamba kuna misongamano mikubwa sana ya watu ambao wanakwenda pale kwa ajili ya kulipia pesa ingawa pesa nyengine inakuwa ni kiwango kidogo tu kama shilingi 3000/-.

a) Je, Mhe. Waziri huoni kwamba ipo haja ya kufungua matawi madogo madogo ili kuwawezesha wale ambao wanakwenda kulipa pesa zile wapate kulipa kwa urahisi.

b) Je, huoni kwamba usumbufu ule unaweza kuwasababisha walipa hawa kodi zile ndogo ndogo kukimbia na kusababisha kwamba pato letu la serikali kushuka.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mhe. Mwakilishi lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo.

Ni kweli kutokana na ongezeko la kutakiwa malipo yote yawe yanapitia benki, kumekuwepo na msongamano huo na kama nilivyosema wakati najibu, jibu la nyongeza la Mhe. Ali Suleiman Ali, nilisema kwamba tatizo hili tunalielewa, tunalijua na hivi sasa benki inalifanyia kazi kwa ajili ya kuondosha usumbufu huo.

Na katika shughuli ambazo zitafanyika na benki ni pamoja kuongeza madirisha lakini pia kufikiria uwezekano wa kuanzisha vituo vyengine vitakavyoweza kusaidia kuondosha msongamano huo. Kwa sababu mbali ya malipo hayo ya leseni lakini sasa hivi

mwelekeo wa serikali ni kuhakikisha kwamba malipo yote hayaendi *cash* mkononi, malipo yote yanakwenda katika utaratibu wa kibenki. Kwa hivyo mahitaji yataongezeka na hata pale bandarini sasa hivi tunafungua kituo cha benki kutokana na maongezeko ya miamala ambayo inatakiwa ipitie kupitia benki.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na Mkurugenzi wa *PBZ* kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kuongeza huduma za wateja na kuongeza wateja katika Benki ya Watu wa Zanzibar. Na katika majibu yake amesema kwamba katika 2006 takriban *PBZ* ilikuwa na wateja 50,000.

Je, kwa mwaka huu 2017 ni wateja wangapi ambao wamesajiliwa na wako katika *PBZ* na ni faida gani ambayo tumeipata kutoka 2006/2017.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, naomba alirudie lile la mwanzo sikulisikia vizuri.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Ali Salim Ali lirudia swali la mwanzo.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nilitaka kujua katika mwaka 2006 katika majibu yake amesema kwamba wateja 50,000 ndio waliokuwa ni wateja wa *PBZ.*

Je, kutoka 2006/2017 ni wateja wangapi mpaka sasa wameshapata kwa Benki yetu ya *PBZ.*

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Wameshapata kitu gani.

Mhe. Nassor Salim Ali: Kutoka 2006/2017 ni wateja wangapi walionao *PBZ*…

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Waliopo.

Mhe. Nassor Salim Ali: Eeeh!

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo.

Nilisema katika jibu mama kwamba mwaka 2006 *PBZ* ilikuwa na wateja 50,000 lakini mwaka huu *PBZ* ina wateja zaidi ya 200,000. Kwa hivyo kuna ongezeko kubwa la wateja na kuvutika kwa wateja hao kunatokana na huduma bora zinazotolewa na benki yetu, lakini vile vile fursa zilizopo na hasa mikopo ile *consumer credit* ambayo inatoka kwa wananchi wa Zanzibar. Kwa hivyo kuna faida kubwa sana na ndio maana imevutia watu wengi sana wa Zanzibar kutumia huduma zinatolewa na benki hii.(*Makofi*).

Nam. 105

Uimarishaji wa Mashamba ya Serikali Yaliopo Pemba

Mhe. Omar Seif Abeid - Aliuliza:

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipa ruhusa ya kuuliza swali lakini kabla ya jibu langu kuna sehemu kidogo nikitaka niifanyie hansard ipokee kwa marekebisho nitakayofanya, huo mstari wa chini usomeke, "Hali ya mashamba hayo kwa sasa hairidhishi kutokana na kuwepo kwa pori kwenye mashamba hayo, hali inasababishwa na upungufu wa wafanyakazi na fedha".

Baada ya marekebisho hayo naomba Serikali itoe jibu kwa swali langu Nam. 105.

Kwa kuwa kuna mashamba maalum yaliyo chini ya Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kama vile Makuwe ambalo ni shamba la mikarafuu na shamba la viungo Daya, Kinyasini Mtambwe (mikarafuu), Chwaka – Tumbe shamba la minazi na Ukutani Gando kwa Mkoa wa Kaskazini Pemba. Hali ya mashamba hayo kwa sasa hairidhishi kutokana na kuwepo kwa pori hali ya mashamba hayo kwa sasa hairidhishi kutokana na kuwepo kwa pori kwenye mashamba hayo, hali inayosababishwa na upungufu wa wafanyakazi na fedha.

(a) Je, serikali hupata kiasi gani cha fedha kutokana na ukodishwaji wa mazao ya mashamba haya hasa la Makuwe na shamba la Kinyasini Mtambwe.

(b) Je, ni kwa sababu gani mashamba hayo yakaendelea kuachwa na pori wakati msimu wa mazao kama vile karafuu mashamba hayo hukodishwa kwa bei nzuri.

(c) Je, serikali ina mpango gani wa makusudi wa kutenga angalau asilimia 35 ya fedha zinazokodishiwa mashamba hayo ili kuweza kutumika kwa kusafishia mashamba hayo na kupanda miti mingine.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa misimu mikubwa shamba la Makuwe huwa linachangia pato kubwa la serikali kutokana na ukodishaji wa zao la Karafuu. Kwa mfano, katika msimu wa Vuli, 2014 shamba hilo lilikodishwa kwa shilingi 51,220,000/- na msimu wa Vuli, 2015 lilikodishwa kwa shilingi 134,000,000/-. Katika msimu wa mwaka 2016 shamba hilo halikuzaa, hivyo halikukodishwa.

Mhe. Mwenyekiti, shamba la Kinyasini ambalo Wizara ya Kilimo ilipewa wakati wa kukabidhiwa mashamba ya eka tatu kutoka Wizara ya Ardhi, shamba hili limeshakodishwa mara tatu ambapo mwaka 2014 lilikodishwa kwa Shs 6,000,000/-, mwaka 2015 lilikodishwa kwa Shs 12,000,000/- na mwaka 2016 msimu wa Vuli lilikodishwa kwa shilingi 1,400,000/-.

Mhe. Mwenyekiti, mashamba hayo yanaendelea kuwa na pori kutokana na kukosa huduma za kusafishwa kwa wakati kutokana na uhaba wa wafanyakazi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kuona kasoro hizo, serikali imeridhia kutenga asilimia 30 ya mapato yanayotokana na ukodishwaji wa mashamba yanayosimamiwa na Wizara hii. Agizo hilo litakapoanza kutekelezwa, pesa hizo zimekusudiwa kutumika kwa uendeshaji wa mashamba ya mikarafuu ikiwa ni pamoja na usafishaji wa mashamba hayo, kufanya tafiti na kutoa elimu kwa wakulima juu ya usimamizi bora wa mshamba ya mikarafuu pamoja na kuchanganya na mazao ya viungo ndani ya mashamba ya mikarafuu.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza na nampongeza Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri yaliyokuwa yanatoa mwelekeo mzuri na serikali kwa kuyaona haya naipongeza sana serikali.

a) Lakini kwa kuwa Mhe. Waziri umekiri kwamba kumekuwepo na uhaba wafanyakazi na kwa sababu serikali imeshaamua kutenga hiyo asilimia 30 ya pesa zitakazopatikana kwenye hayo mashamba. Sasa mimi nataka nijue je, wizara ina mpango gani wa kuajiri wafanyakazi ijapo kwa muda kwa ajili ya kuyashughulikia mashamba hayo ili yawe kwenye hali nzuri yaweze kuzaa vizuri na kuongeza pato letu la taifa. Hilo la kwanza.

b) Lakini hapa Mhe. Mwenyekiti, sikuona jibu la shamba la Daya ambalo nalo pia niliuliza, nilitaka pia nijue ni kiasi gani cha fedha kimepatikana na kukodishwa kwa hilo shamba la Daya. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza nikubaliane naye kabisa kutokana na uhaba wa wafanyakazi, hii mbinu ambayo ya kuajiri kwa muda baada ya kupata hii asilimia 30 tutaitekeleza ili tuhakikishe kabisa mashamba haya yanakuwa safi.

Kuhusu suala la Daya Mhe. Mwenyekiti, namuomba radhi nitamjibu kikamilifu, naomba radhi sana naona lime-*miss* hata mimi. Naomba radhi tu Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Maryam Thani Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipa fursa hii ya kuuliza swali moja lenye (a) na (b) kama ifuatavyo.

a) Kwa kuwa mashamba haya yanakodishwa kwa kila msimu wa mazao. Je, wizara huwa inafanya utafiti gani wa mazao yaliyomo katika kuyatathmini kabla ya kuyakodisha.

b) Utaratibu gani wa wizara unaotumika katika kuyakodisha mashamba haya baada ya kuzingatia tathmini iliyofanyika. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, napenda nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kabla ya mashamba kukodishwa huwa tunafanya tathmini mara mbili. Mara ya kwanza ni pale tu tunapoona kwamba karafuu zinaanza kuzalishwa kwa kushirikiana na *ZSTC* pamoja na wataalamu wengine, Kamati hiyo hupita kwenye mashamba na kuangalia uwezekano wa mashamba kuzaa.

Nafikiri wale wanaoshughulika na karafuu wengi wanajua kabisa kuna kipindi ukiangalia majani tu unaweza kujua sasa karafuu zitazaliwa kiasi gani. Kipindi kile ni cha kwanza kabisa kufanya tathmini.

b) Kipindi cha pili ni kipindi ambapo tunaona karafuu sasa karibu zinataka kuchumwa ndio tunaweza kufanya tathmini ya pili. Baada ya tathmini hizo mbili kwa kutumia sheria ya manunuzi (*Procurement Act*) ndio tunatumia taratibu za kukodisha ama kwa tenda au kwa mnada. Hizo ni njia mbili ambazo zinatumika katika kukodisha.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa na mimi fursa ya kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza lenye (a) na (b).

a) Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa tunafahamu kwamba shamba la michungwa Kizimbani ni shamba ambalo lina mazao ya aina tofauti. Katika shamba hili kuna michungwa, mishokishoki bundala, mishokishoki kawaida, *mangosteen*, kuna na miratabu. Lakini kwa kuzingatia mazao ambayo yanazaliwa kwenye shamba hili ni mazao mengi na yenye umuhimu zaidi. Je, wizara inakuwa inachukua taratibu gani ya kuyakodisha mazao hayo.

b) Je, kwa vile shamba hili tukizingatia hasa kwa miti hii ya mishokishoki na *mangosteen* na miratabu ni miti ambayo tayari imeshakuwa ya siku nyingi na imeshapea sana. Je, wizara ina utaratibu gani wa kuyaimarisha miti hii kuwekeza tena mbegu ili shamba lile libaki kwenye uasili wake na kuweza kuingiza pato la nchi yetu. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa maswali ya Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo.

a) Mhe. Mwenyekiti, pale kuna mashamba ya aina mbili, kuna mashamba ya kituo cha utafiti na kuna mashamba ambayo yako chini ya Chuo cha Kilimo. Sasa mashamba haya ya utafiti kazi yake kubwa miti iliyokuwepo pale ni kufanyia utafiti, hayapo pale kwa ajili ya kukodishwa kwa biashara, hii kazi ya utafiti na kufanya utafiti. Pale mazao yanapokuwa mengi ndio husema kwamba tunawauzia mara nyingi tunawaambia tu wananchi na wafanyabiashara kuja kununua, hatuna utaratibu kama ule ambao tunautumia kwenye mikarafuu.

Kwa hivyo, lakini nasema tutakwenda kuangalia namna gani tunaweza tukaboresha hasa Bodi ya Chuo itakapoanza kazi rasmi kuona ni namna gani tunaweza kuyatumia mazao haya kuweza

kusaidia kupata mapato katika chuo chetu. Kwa hivyo nasema nakubaliana na ushauri wako kwamba ni vizuri sasa tukauratibu zaidi utaratibu wa mazao yanayopatikana katika kituo cha taaluma kuweza kuwasaidia wananchi.

Kwa upande wa miradi ya mashamba ambayo yako Chuoni kazi yetu kubwa pale ni kutoa taaluma kwa watu wetu. Na katika bajeti mara hii nimeshauri kwamba ni vizuri wale wanafunzi wetu pale sasa wakapata ujasiriamali. Kwa hivyo mpango tulionao ni kuyapanua mashamba yaliyoko pale, tutoe taaluma kwa vijana wetu ili wakitoka pale wawe na wao ni wajasiriamali katika suala zima la kilimo. Kwa hivyo nasema tunalizingatia.

Mhe. Mwenyekiti, samahani la pili sikulisikia vizuri.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Mhe. Mwenyekiti, swali langu la pili lilikuwa linasema hivi, kwa vile shamba lile miti yake iliyokuwemo mle mingi yao tayari imeshakuwa ya siku nyingi. Je, wizara ina utaratibu gani wa kuimarisha na kuwekeza mbegu kwa ajili ya miti ile ambayo iliyokuwepo pale imeshapea na kuweka miti mengine ambayo itakuwa ni endelevu zaidi ili kuimarisha shamba lile na kuongeza pato la nchi yetu.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu kama ifuatavyo.

b) Kama ulivyoona katika programu zetu za mwaka huu katika bajeti, kazi yetu moja kabisa ni kuimarisha mashamba yale na kuona kabisa kwamba tunapanda miti mipya na ile mikongwe inaondolewa ambayo haina mazao tena zaidi. Kwa hivyo ipo katika programu ya bajeti ya mwaka huu.

Nam. 73

Mpango wa Zanzibar kuwa na Nishati Mbadala ya Umeme

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:

Hivi karibuni kumetolewa tishio la kukatwa umeme Zanzibar kutokana na deni kubwa ambalo Shirika la Umeme Zanzibar (*ZECO*) inadaiwa na *TANESCO*. Tishio hilo limezuwa taharuki kubwa na mjadala kwa wananchi.

(a) Pamoja na serikali kuchukuwa hatua madhubuti za kulipa deni hilo, kuna mpango gani kuhakikisha Zanzibar inakuwa na umeme wake mbadala badala ya kutegemea chanzo kimoja peke yake.

(b) Kwa nini *ZECO* inadaiwa deni kubwa na *TANESCO* wakati wananchi wanalipa Ankara zao.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Nishati na Mazingira – Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake Nam. 73 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Katika kukabiliana na tatizo la ukosefu wa umeme, serikali hivi sasa inakamilisha utafiti yakinifu wa kupata vyanzo mbadala vya uzalishaji wa umeme ndani ya Zanzibar. Utafiti huo umejikita katika nishati ya jua na upepo.

(b) Deni ambalo Shirika la Umeme Zanzibar linadaiwa na *TANESCO* linatokana na mkusanyiko wa malimbikizo ya ankara za umeme kwa muda mrefu. Hali hiyo imesababishwa na watumiaji wa umeme kwa kipindi kirefu kutokuwa na utamaduni wa kulipia ankara zao kwa ukamilifu. Licha ya mikakati ya uwekaji wa mita za TUKUZA, bado shirika linakabiliwa na malimbikizo ya madeni kutoka kwa watumiaji wengine wanaotumia mita za kawaida.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri.

Wizara hii ina Waziri, Naibu Waziri, Wakurugenzi, Makatibu Wakuu na Naibu Katibu Wakuu. Ni muda mrefu sasa hivi na umeme tunaotumia Zanzibar ninafikiri ni *megawatt* kidogo sana ukilinganisha na viwanda huko duniani. Kiwanda kimoja tu kinatumia umeme kuliko Zanzibar.

Je, hawaoni kuwa wakati sasa hivi umeshafika wa kuondosha tatizo hilo pamoja na kuwa umejibu kuwa serikali hivi sasa inakamilisha utafiti yakinifu kwa kupata vyanzo mbadala vya ukusanyaji wa umeme ndani *ya* Zanzibar. Huoni ukamilishaji wake utachukua muda na haya ndio majibu ya mazowea ya siku zote tuko mbioni, taratibu zinafuatwa, matunda yataonekana. Lini mutakamilisha utaratibu huu ili kuogopa yasije yakatokea yaliyotokea, kuna wakati Zanzibar tulikaa miezi mitatu kiza na hivi sasa tunatishiwa deni. Hilo la kwanza.

La pili, kuna taarifa deni tulilokuwa tunadaiwa limefutwa mwaka 2006, hebu atupe kauli ni kweli deni hilo limefutwa au halijafutwa. Kama huna taarifa lifuatilie hilo suala, tusije tukalipa mzigo ambao sio wetu.

Lakini chengine kwa kuongezea hapo hapo, huoni kuwa wananchi umeme huo wananunua wakatia kwenye mita zao kwa kulipa huku deni hilo limetokea wapi, hebu tufahamishwe ni la wananchi au la serikali.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Naibu Waziri jibu mawili.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti ahsante, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

a) Ni kwamba serikali inaona haja ya kuwa na chanzo chake cha umeme na ndio maana kama nilivyokuwa nimesema kwamba inaendelea kukamilisha utafiti. Huko nyuma tulisema kwamba utafiti wa awali ungemalizika Februari mwaka huu na imekamilisha na sasa tunakwenda katika kutafsiri *data* na kuona kwamba tunatumia vipi na tunategemea Agosti mwaka huu itapatikana ripoti na kuwasilishwa Serikalini.

b) Taarifa sina za kwamba kuna deni ambalo limefutwa, lakini kama alivyokuwa anasema basi tutalifuatilia lakini taarifa tulizonazo ni kuwa hakuna deni ambalo limefutwa na ndio maana akaona kuna deni hili na tunaendelea kulilipa. Ahsante sana.

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana napenda kumuuliza swali la nyongeza Mhe. Naibu Waziri.

Kuna taarifa ya utofauti wa deni hili, *TANESCO* wanasema *ZECO* wanaidai shilingi bilioni mia moja na *ZECO* inasema tunadaiwa shilingi 65 bilioni. Je, suala hili ni sahihi na kama ni sahihi kuna utofauti huo ni sababu gani ambazo zimepelekea kuwa na utofauti huo.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Asha Abdalla Mussa swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Ni kweli kuna tofauti kati ya deni ambalo wanalijua *TANESCO* na deni ambalo wanalijua *ZECO*. Lakini baada ya kulifuatilia imegundulikna kwamba chanzo ni kwenye kodi, wenzetu walikuwa wanatu-*charge* kwenye *KVA* moja kwa shilingi 16,000 wakati *ZECO* tunasema tunapaswa kulipa shilingi 8,000. Hii ni sehemu moja kati ya eneo ambalo limeleta tofauti. Lakini niseme kwamba lile deni ambalo sisi kama *ZECO* na *TANESCO* tunakubaliana lilipwe ndilo ambalo tunalipa na hilo ambalo kuna tofauti za kimahesabu litatatuka kwa mujibu wa taratibu za kimahesabu. Ahsante sana.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana afadhali umeniona nakushukuru sana, nitaomba kuuliza swali la nyongeza lenye (a) na (b) kwa Mhe. Naibu Waziri.

(a) Ningependa kujua katika deni wanalodai wao *ZECO*, serikali wanawadai shilingi ngapi kama taasisi au wizara, na watu binafsi wanaowadai wanaosema wao wanawadai shilingi ngapi, anipe jumla ya ile hesabu halafu tuone tofauti sasa na *TANESCO* wanadai shilingi ngapi tuangalie *balance* iko vipi.

(b) Sababu zipi zinazosababisha wananchi wanapohitaji umeme kulipishwa kuanzia *wire*, nguzo, mafuta ya kwendea kule mpaka posho za mafundi na kila kitu, wakati nchi nyengine

hizi *service* zote zinatakiwa zifanywe na Shirika, umeme ndio alipe mwananchi. Ni sababu zipi munazofanya kuwalipisha wananchi wanyonge kuanzia kila kitu mpaka kufunga mita.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti ahsante, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo, nianze na (b) kwa nini wanalipishwa.

Niseme kwamba Shirika linahitaji kujiendesha lazima wananchi wachangie. Lakini hata hivyo, katika uhalisia Shirika linakuwa limebeba baadhi ya sehemu ya gharama hizo kama utaambiwa ubebe zile gharama halisi hasa pia ungeona tabu zaidi, lakini ujue tu kwamba inamchangisha mwananchi kwa ajili ya lile Shirika liweze kujiendesha kutoa huduma zaidi.

Naomba angerejea lile la (a).

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Mwenyekiti, mimi hata hilo la (b) pia naona hajanijibu vizuri, lakini nitaanza na hilo la (a) analolitaka yeye.

Mhe. Mwenyekiti, nimeuliza *TANESCO* wanasema wanadai fedha fulani ikiwa shilingi bilioi mia moja au mia na ishirini wanajua wenyewe. Nimetaka kujua *ZECO* kama *ZECO* Zanzibar inadai Taasisi za Serikali au serikali nzima inadai shilingi ngapi kwenye deni lao la umeme na watu binafsi wanawadai shilingi ngapi wananchi wa kawaida. Halafu ndio tutaangalia sasa *ZECO* inafanya kazi vizuri ama inafanya kazi vipi, tunataka kujua hesabu hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, ahsante naomba nimjibu Mheshimiwa swali lake kama ifuatavyo. Ni kwamba hili suala linataka takwimu na hapa ni sehemu ambayo utoe jibu la usahihi, lakini nimwambie kwamba tutamletea kwa maandishi.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba nijibu hili swali la (b) la Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf kama ifuatavyo. Kwamba katika deni la shilingi 65.6 ambalo tunadaiwa katika Taassi za Serikali tuna deni la shilingi 33 milioni na katika wananchi wa kawaida na watu wengine wadai shilingi 32.6. Hilo ndio deni ambalo tulikuwa tunadai mpaka Januari.

Lakini baada ya serikali kulipa shilingi bilioni kumi ambayo sasa hivi na baada ya kufanya *reconciliation* na *ZECO* kuangalia tofauti ya deni baina ya *TANESCO* na *ZECO* mpaka sasa hivi tunadaiwa shilingi 57.7 bilioni ambazo fedha hizo serikali imepanga utaratibu kwamba Wizara ya Fedha kuna deni wanapunguza na *ZECO* wanapunguza. Kwa hivyo serikali italipia lile deni la serikali.

Kwa hivyo baada ya miaka miwili deni hilo tutakuwa tumelikamilisha na naomba nifafanue tu kidogo lile alilokuwa akilizungumza kwamba hii tofauti ya deni. Tofauti ya deni lilikuweko baina ya *TANESCO* na *ZECO,* kulikuwa kuna makubaliano ya nyuma hakuna deni lililofutwa mwaka 2006 ila kulikuwa kuna makubaliano kwamba kuna deni ambalo litaingia moja kwa moja kwenye Serikali ya Jamhuri ya Muungano ambalo hili lilikuwa ni *thirty one percentage* ya deni, bili ile ilikuwa inaletwa kwetu.

Lakini vile vile kulikuwa kuna *charge* za *EURA* ambao wana-*charge* miundombinu yote kwa ujumla wake Tanzania ambayo pia tulikuwa tunaingiziwa sisi. Kwa hivyo baada ya ile *reconciliation* na kukaa katika vikao tofauti, tukakubalina deni halisi ambalo halina mgogoro ndio hili ambalo lilikuwa 65.6 ambalo *ZECO* ndio walikuwa wanalitambua, lakini vyenginevyo deni jengine lilikuwa linalipwa. Sasa hivi naomba nilifahamishe Baraza lako tukufu kwamba deni la kawaida zile bili za kawaida zinavyokuja ankara, bili zile zote zinalipwa kwa wakati tokea Disemba, 2016 mpaka sasa hivi. Kwa hivyo deni hili liko 33 ambalo serikali ilikuwa inadaiwa na watu wa kawaida wanadaiwa 32.6.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Waziri, maswali kwa *order paper* yetu ya leo yamekwisha katibu kwa shughuli inayofuata.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 - Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe majadiliano yanaendelea sasa naomba nimwite Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf akifuatiwa na Mhe. Omar Seif Abeid na Mhe. Hidaya Ali Makame ajitayarishe.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Mwenyekiti ahsante sana. *Bismillahi Rahmani Rahiim* kwa kunipatia nafasi hii

mtu wa mwanzo kuchangia Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko.

Kwanza niwape Ramadhan Kareem wananchi wangu wote wa jimbo la Chaani. Lakini pia nitachangia mambo machache kwenye wizara hii na nitatoa ushauri wa mambo machache ambayo nayafahamu mimi mwenyewe, lakini pia nitakuja kutaka kuuliza masuala machache kidogo katika wizara hii nije nijibiwe.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Biashara ni wizara kubwa, ukiiona kimuundo utasema ndogo lakini hizi wizara zote zinazoingiza *income* katika nchi, ikiwa Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo; Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji hata Wizara ya Fedha na Mipango, mama yao ni Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko. Chochote kile cha kukusanya, cha kuuza, cha kuleta, cha kupeleka kinaitwa biashara ikiwa kidogo au kikubwa. Sasa ninachotaka kusema kwamba wizara hii ni kubwa naweza kusema kuliko zote ukiangalia muundo wake, lakini sasa kutokana na *department* tofauti na wizara tofauti ndipo ambapo imepunguziwa majukumu. Lakini kama Wizara ya Biashara basi pia ingewezekana kuunganishwa hizi sehemu zote za vitega uchumi akapewa Waziri wa Biashara afanye yeye, lakini kutokana na mazingira ya nchi tofauti kila mmoja na msimamo wake.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwa wizara hii sitokuwa na mengi sana kwa sababu vitu vinaonekana baadhi vizuri na baadhi ambavyo havijakaa sawa wanajitahidi na nafikiri sana wanajitahidi kutaka kuhakikisha vitakaa sawa.

Mimi nasema sana penye sifa mtu atapewa sifa, penye tatizo mtu ataambiwa. Sasa kwenye wizara hii nimeshaanza kuzungumza

kwamba inafanya vizuri na yale ambayo hayako vizuri wameshaeleza kwamba wanataka kuyatatua na yanaonekana kwenye kitabu hiki ambacho wamekileta kimeeleza vitu wazi wazi na hiki ndicho kilichonifurahisha mimi. Ijapokuwa inawezekana yako matatizo kwenye wizara hii na naamini yatakuwa si matatizo makubwa yanataka kuelimishwa, kufanyiwa kazi na utatuzi. Kwa Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake naamini wana uchungu na Zanzibar na watafanya hili suala lirudi katika hali iliyokuwa mwanzo tofauti na sasa hivi katika baadhi ya mambo. Sasa hivi tuwape sifa zao kuna mambo yanakwenda vizuri kwenye biashara, lakini tukiangalia huko nyuma kulikuwa kuna vitu vile vile vinafanya biashara nzuri sana Zanzibar lakini sasa hivi vimekatika kutokana na masuala fulani.

Mimi nitakwenda kwenye michango yangu kidogo pamoja na ya kwenye kitabu hiki kilicholetwa na wenyewe. Kwanza niipongeze serikali kwa kuleta bajeti ambazo zilizobakia Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko, Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Afya, Wizara ya Ujenzi, Mawasialiano na Usafirishaji na Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kutuletea kwenye mwezi wa Ramadhani, maana yake Ramadhani ni wakati wa kusema ukweli. Sasa hapa tutakuja kuzungumza kila kitu wazi wazi kifahamike.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitakwenda katika *page* ya 6 kwenye "Usafirishaji na Uagiziaji Bidhaa Duniani 2016". Ukiangalia nchi ambazo zinaongoza katika masuala ya biashara duniani na itakuwa ndio kwa miaka mingi mbele ni nchi hizi za Ulaya, Amerika, Asia na *Middle East*. Ukiangalia kwenye kila kitu Afrika iko mwisho, lakini tuangalie katika uchumi wa nchi ni asilimia 3.17 Afrika nzima ambayo wana percent hiyo. Sasa ukiangalia kwamba Afrika nzima ina kiwango hicho cha biashara

kidogo. Je, Zanzibar itakuwaje *East Africa* na kipande hiki ambacho tuko huku ambapo ni nchi ndogo sana. Kwa ufupi kiuchumi tunatakiwa tuwe *careful* sana kwa upande wa Zanzibar na ninaamini Mhe. Waziri anafanya kazi ya jitihada pamoja na watendaji wake.

Vile vile ukiangalia kwenye *page* ya 8 Mwenendo wa Biashara Zanzibar (2012 - 2016), uagiziaji *imports* 2012 shilingi 271,273.1 milioni hii ni uagiziaji. Lakini 2013 shilingi 208,051.9 milioni, 2014 shilingi 279,552.8 milioni, 2015 shilingi 156,941.1 milioni, 2016 shilingi 167,088.0 milioni. Inaonekana kwamba uagiziaji umekuwa mkubwa katika kipindi cha mwaka 2016, lakini usafirishaji katika mwaka 2012 ulikuwa ni shilingi 67,390.5 milioni, mwaka 2013 shilingi 87,799.6 milioni, mwaka 2014 shilingi 133,587.7 milioni na mwaka 2015 shilingi 42,407.0 milioni na mwaka 2016 shilingi 96,234.9 milioni.

Usafirishaji ume-*drop*, lakini vyanzo vya ku-*drop* vinatokana na sababu tofauti, aidha baadhi ya vikwazo kutoka nchi jirani au kuna vitu ambavyo vimekwamisha kwenye masuala ya kodi au nchi yenyewe wafanyabiashara wenyewe wameamua kuacha kile kitu na ndio hiki kilichofanya kwamba usafirishaji sasa utaona kutoka Zanzibar kwenda Tanzania Bara kwenda na sehemu nyengine nchi za jirani umepungua. Mimi nitamuomba Mhe. Waziri atapokuja aje atujuilishe sababu zipi ambazo zilizofanya kwa kipindi hiki usafirishaji wa bidhaa zinazotoka Zanzibar kwenda nje zimepungua. Hata katika huu uagiziaji umekuwa mkubwa ni uagiziaji gani ambao ulioletwa, vifaa aina gani ni vyakula ama *electronic items,* ama vitu vyengine vipi.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kuna kitu chengine hapa kimeeleza wazi kabisa biashara baina ya Zanzibar na Tanzania Bara (*inter-state*

trade balance). Mhe. Mwenyekiti, imesema *page* nambari 8 hiyo hiyo, 'Biashara baina ya Zanzibar na Tanzania Bara inahusisha utoaji wa bidhaa kutoka Zanzibar kwenda Tanzania Bara na uingizaji wa bidhaa kutoka Tanzania Bara kuja Zanzibar'. Biashara hiyo inahusisha bidhaa za mchele, mbatata, maharagwe, vitunguu, tungule na mboga mboga, vitu vya elektroniki, magari na bidhaa nyengine zinazohitajika hapa nchini.

Kwa kipindi cha mwaka 2016 Zanzibar ilipeleka Tanzania Bara bidhaa zenye shilingi 84,760.9 ikilinganisha na bidhaa zenye thamani ya shilingi 401,219.4 zilizopelekwa mwaka 2015. Hapa inaonesha dhahiri kwamba Zanzibar kuna vitu vinasababishwa kwamba visiweze kupelekwa Tanzania Bara, kuna jambo hapa lipo inawezekana kwenye masuala ya kodi au kuna vitu vinazuiliwa kwa njia ambazo wanataka Zanzibar tusiendelee kwenye suala la uchumi.

Mhe. Mwenyekiti, kiwango hicho cha bidhaa ni zile bidhaa ambazo zinapelekwa katika mfumo ulio rasmi wa kiforodha. Hali hiyo imesababishwa na kupungua upelekaji wa bidhaa za magari na vifaa vyengine vya kieletroniki kutokana na mabadiliko ya usimamiaji wa baadhi ya kodi zikiwemo *VAT* na kadhalika huko Tanzania Bara na kutokubaliana juu ya usajili wa magari yanayotoka Zanzibar kwenda Tanzania Bara.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sitaki kupoteza wakati kwa sababu nina risala zangu karibu sita tofauti sijui kama nitawahi. Mimi ningeiomba sana Wizara ya Biashara ndugu zetu wa Tanzania Bara wasitu-*block* kutaka kutukwamisha sisi nchi ndogo kwenye vitu kama hivi vya biashara. Mhe. Mwenyekiti, wakati wa kipindi cha nyuma nchi hii ilikuwa inafanya biashara vizuri na nchi ndio

hizo hizo. Sasa imekuwaje sasa hivi kuna vikwazo ambavyo vinawafanya Wazanzibari wasiweze
kupeleka gari zao, wasiweze kupeleka vitu vyao wakapanidishiwa kodi.

Mhe. Mwenyekiti, biashara tunayotegemea Zanzibar ni biashara ya magari kwa wanaoza magari na Zanzibar inajulikana gari bei nzuri. Lakini cha kushangaza tuna *TRA* na ndio inayolipisha hapo *TRA* Zanzibar. Kwa nini wapofika Tanzania Bara wa *TRA* inawaweka vikwazo kuwapandishia bei kubwa. Sasa kama *TRA* ya Zanzibar haina maana Mhe. Waziri wa Biashara kushirikiana na Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais *TRA* iondoke. Kama *TRA* ya Dar es Saalam haiwezi kuiamini *TRA* ya Zanzibar basi *TRA* ifutwe. Huu ni usumbufu ambao unasababishwa na watu wachake kuuwa uchumi wa Zanzibar. Mhe. Waziri ni mzalendo, haya masuala yameweka dhahiri kwenye hichi kitabu nawaponegeza na mimi ndio napenda mtu awe muwazi na ndio maana ukakuta mimi sitaki hata kumwambia kitu kwenye wizara yake.(*Makofi*).

Lakini Mhe. Mwenyekiti, kuna vitu vingi sana kwenye kitabu hichi ambavyo vya *statistics* na mambo mengine sitoweza kuvimaliza nikivijali acha niende kwenye masuala yangu ya pamoja. Mhe. Mwenyekiti, suala la masoko Zanzibar kipindi cha nyuma wakati wa Mhe. Dkt. Salim Amour Juma na wengine ambao mpaka leo Dkt. Ali Mohamed Shein tulikuta nchi za Comoro, Kenya, Uganda, Afrika ya Mashariki kwa ufupi kwa ujumla pamoja na Ethiopia na nchi nyengine kuja kuchukua vitu Zanzibar, wananunua kwa wingi walikuwa wakitumia *Euro* kulipia vitu.

Lakini leo nchi zile zimehamia Tanzania Bara na sehemu nyenginezo haziji Zanzabar. Sasa ni sababu zipi ambazo zilizofanya uchumi huu wa Zanzibar umeuliwa, kitu gani kimetokezea hapa hata leo mpaka Wacomoro leo hawaji tena Zanzibar, uchumi umekufa, wafanyabiashara wa Afrika ya Mashariki hawaji tena wanakwenda Tanzania Bara. Hii ningeomba nije nipate ufafanuzi sababu zipi zinazosababisha haya masuala hata hawa watu wenzetu ndugu zetu wa East Afrika kutofika Zanzibar.

Lakini nikienda kwenye suala la *ZBS. S*uala hili hivi vifaa vinavyokaguliwa na *Zanzibar Bureau Standard* (*ZBS)* kina nguvu gani kitengo hichi. Mimi ningependa kujua na Mhe. Waziri atakapokuja aje kunijibu. *ZBS* hii Tanzania Bara inathaminika vipi na inatambulikana nchi ngapi. Kwa sababu kama *TBS* na nchi nyengine ambazo dunia nzima zinazozalisha vitu zina nembo yao ambayo ya ukaguzi bora wa vile vitu. Sasa hii *ZBS* ya Zanzibar ukiitoa Zanzibar nchi ngapi inaitambua *ZBS,* na ina nguvu gani na tunaweza ku-*supply* vitu vyetu kwenda nchi ngapi kwa mujibu wa *brand* hii tuliyokuwa nayo kwa upande wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia biashara nyingi za Zanzibar utakapoziteleka sehemu nyengine watu watazidharau, kwa sababu wanapotaka wenyewe sijui wanataka vipi, labda kwamba kuonea au labda kwamba wanasema tu hawaijatimia vigezo, lakini sio kweli. Zanzibar tuna vitu, mfano vyakula *number one very fresh*, tuna vitu ambavyo tunapotengeza hapa hiko *high standard*.

Mhe. Mwenyekiti, mimi Mhe. Waziri nitaomba aje anipe ufafanuzi mzuri wa haya mambo yameparaganyika vipi. Lakini ushauri wangu mwengine ningeomba sana itengenezwe *executive board.* Ushauri wangu Wiraza ya Biashara, Wizara ya Fedha,

Wizara ya Kilimo, Wizara ya Utalii na Wizara ya Mawasiliano watengeneze Bodi yao *special* ambayo wataweza kujadiliana, wataweza kuiangalia nchi watainua vipi kiuchumi, kwa sababu wizara hizi ndio wizara nzito ambazo zinategemea mapato ya nchi nzima.

Ningeomba sana Mhe. Mwenyekiti, watengeneze *executive board* yao wenyewe wa wizara hizi tano nilizozitaja, waangalie hasara iko vipi, tupunguze nini, tuzidishe nini, tufanye nini ili nchi irudi kama iliyokuwa hali ya mwanzo kipindi cha nyuma, sasa tukitaka tusitake Zanzibar uchumi wa Zanzibar hauko mzuri. Uchumi wa Zanzibar ume-*drop purchasing power* iko *very low* Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, ukiona nchi kwamba inanunua vitu sana lakini inavyotoa kidogo ujue hiyo nchi haiko *stable* kwenye suala la biashara. Nchi za wenzetu tukiangalia zilizokuwa *powerful* zinatoa zaidi kuuza nje na wanazonunua wao inakuwa kidogo na ambazo zile hawana ni *very rare thing* ambazo wananunua kutoka nchi nyengine. Mhe. Mwenyekiti, huo ulikuwa ushauri wangu kutoka wizara hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, lakini vitu vyengine ambavyo nataka nivizungumze. Ningeshauri kwamba ile meli ambayo imenunuliwa basi ianze kwenda huko wanakosema Comoro mpaka Kenya Mombasa, ikachukue biashara pamoja na vitu ambavyo watakuja kununua Zanzibar waweze kupakia kwenye meli, waweze kwenda kushusha nchi za kwao kuliko kutumia ndege, ndege saa nyengine zina gharama zake kwenye kupakia kilo, wana-*charge* fedha nyingi kwenye kilo lakini meli kama hii tuliokuwa nayo MV Mapinduzi II, kama itafanyakazi za umuhimu kabisa kwenye nchi hizo basi itaweza kufanya biashara kama hapo mwanzo walipokuwa wakija hapa.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, ningependa kujua hii *Chamber of Commerce* ya Zanzibar ambayo ipo watu ambao wanatakikana kwenye *chambers* hii wanatakiwa wawe na vigezo gani, wawe na elimu ipi, wawe lazima wafanyabiashara au wenye uzoefu tu. Mhe. Mwenyekiti, ninataka kujua vigezo vyao gani ambavyo vinaweza kumfanya mtu awe *board members* wa hii *Chamber of Commerce* ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, nitakwenda kwenye suala soko la bidhaa. Suala la bidhaa za *used* Zanzibar, hili suala hatulikatai lije lakini wanaleta bidhaa mbovu na inawezekanaje mtu analeta makontena ya vitu *used* anakwenda kufungulia kwake, visifunguliwe pale bandarini. Vitu ambavyo vinaletwa vya *used* nchi hii vibovu vimejaa mende, wanauziwa wananchi vitu ambavyo vimeshatupwa na wazungu hapa wanakuja kuuziwa wananchi na wanakuja kuuziwa kwa bei kwa kubwa kwa kudanganywa kwamba hivi vitu vimetoka UK, vimetoka Canada, vimetoka USA, wakati kule vimeshatupwa Wazanzibari kule wanakusanya vile vitu kwenye magodauni yao na vitu ambavyo vimetupwa havina thamani. Ningeomba sana vitu vyote vya *used,* makontena yafunguliwe bandarini, vilivyokuwa havina viwango vizamishwe vikatupwe na vichomwe moto. Mhe. Mwenyekiti, unapompa mfanyabiashara *loop hole* ya kwenda kufungulia kontena nyumba kwake basi hujui kaweka vitu gani ndani.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, ningeomba sana Wizara ya Biashara wakishirikiana na Wizara ya Mawasiliano makontena ya vitu vya *used* vifunguliwe ndani ya bandari pale, sio nje mtu nyumbani kwake hujui kapakia nini na vitu vibovu vingi wanaleta na vitu vile vya hatari vya umeme na vitu vyengine vitasababisha *short* na kuungua nyumba za watu ambazo za wanyonge.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitaendelea kwenye suala la bidhaa hizo hizo za elektroniki na mambo mengine ambazo ni mpya. Biashara za Zanzibar nyingi wanazozileta vitu vya elektroki hasa vya umeme ni vitu ambavyo haviko *high quality,* haziko katika *standard* iliyokuwa bora ni vitu *fake* na vitu ambavyo vinasababisha *short* ni masuala la *switch,* taa, na masuala ya vitu vingi. Vitu hivi ningeomba mukenda kukaguliwa halafu mkaweka na nembo yenu ya kuridhika kwamba hivi vitu vinaweza vikatumika Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, tunaona vifaa vingi wanauza bei kubwa, kuna vifaa wanaita mpaka *brand* hasa, utaambiwa hii *brand* ya *USA* kumbe kitu kimetengenezwa China. Hebu Mhe. Waziri aje atujulishe mnafanya utafiti gani, mna vifaa gani vya mashine ambavyo mtaweza kuvikamata hivi vitu *fake* vya elektroniki vinavyosababisha ma-*short* na watu kutozwa pesa nyingi wakati sio vitu *quality*.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, baadhi tu ya vitu ambavyo vinavutia wawekezaji kuja nchini kibiashara ni vitu vuchache nitavitaja nimeviandika sasa hivi hapa. Kitu cha kwanza usalama wa nchi ambao usalama tunaringia tunao kwa muda huu. Lakini kitu cha pili urahisi wa *procedures* zile za kutengeneza *document.* Zanzibar bado katika watu wanaokuja ku-*invest* kufanya mambo ya biashara wanasumbuliwa sana kwenye mambo ya *registered* na vitu vyengine katika suala la kujiandikisha kwenye biashara zao, mpaka wawe na mtu labda mwenyeji au mtu ambaye anajulikana serikalini ndio atapata *as soon as possible*. Lakini akija yeye mwenyewe kama mwenyewe anapata tabu sana mpaka kufikia kile kiwango cha mara moja cha kufungua biashara yake. Hichi kitasababisha kwamba pia kipunguze ma-*invertors* katika nchi yetu kwa sababu ya kutokwa na imani.

Lakini cha tatu kodi Mhe. Mwenyekiti, nchi yetu Zanzibar nimezungumza ni lini serikali yetu ilifikiria kushusha kodi za nchi, hata kama kwa muda wa miaka minne haikupandisha. Lakini huo wakati wote toka enzi za mapinduzi mpaka leo, fikra zilizokuwepo ni kupandisha kodi tu katika serikali, ndio wanavyohisi wao kwamba uchumi utakwenda, tunaweza tukashusha kodi kwenye nchi hii na nchi hii ikaenda. Lakini nashangaa kwamba wachumi wanaowatumia ni kupandisha kodi, hawajafikiria hata siku moja kutafuta fikra nyengine za kushusgha kodi halafu kuangalia nchi itakwenda vipi.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, unataka kunambia nisimame au vipi, naona unataka kuwasha taa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ningeomba sana Mhe. Waziri suala la kodi ashirikiane na Waziri wa Fedha hili suala litakuja kuuwa nchi. Mhe. Mwenyekiti, watu wanavutiwa pia ma-*investors* wakubwa wanavutiwa na nchi ambayo ina kodi ndogo na tukijaribu hichi kitu, tujaribuni tusione tabu, tunaweza tukaja tuka-*gain* sana kwenye masuala ya *investment*. Lakini chengine umeme bei kubwa, hii unakimbiza hasa ma-*investors* wakubwa kwenye *industrial* kubwa, mahoteli makubwa wanatumia umeme na umeme wetu ni fedha nyingi.

Mhe. Mwenyekiti, ningeiomba sana wizara ikaangalia kwenye masuala ya ma-*investors* wakubwa ambao watataka ku-*invest* inchi yetu, basi wawekewe tahafifu kwenye suala la umeme au kwa nchi nzima warudishe umeme wakaweka kiwango kidogo, na hiyo migogoro iliyoko Tanzania Bara waitatue. Haiwezekani Zanzibar mpaka hivi leo tunapewa fedha ambayo kama maana yake watu ambao watu wanaita sisi ni *commercially*. Zanzibar ni *commercially* tunanunua umeme kwa biashara, hatununui umeme

kwa mtu nmoja mmoja, lazima tuuziwe umeme kwa bei ya jumla. Mhe. Mwenyekiti, ukiona kwamba hili suala wana-*charge* bei hii, inamaanisha kwamba hapo tayari kunataka kufanyika uuwaji kwa masuala ya uchumi. Nchi kama hii inatakiwa sasa hivi tujitegemee kwa umeme wetu wenyewe, tuna umeme wa upepo unakubali, umeme wa gesi, umeme wa bahari, umeme wa jua, kila kitu tunaweza tukakifanya. Tunaomba sana Mhe. Waziri haya uyaangalie.

Lakini...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf naomba umalizie.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Jengine ambalo nilitaka kulizungumza ni suala la *foreign investment support*. Suala ambalo linavutia wawekezaji wanaangalia nitapokwenda nchi ile vipi sisi *foreigners* tuna nguvu na kupewa *power* gani katika nchi ile. Sasa naomba sana kwa upande wa wawekezaji wageni wawazidishie kuwawekea nafasi nzito, kwa sababu yametokezea matatizo kipindi cha nyuma, baadhi ya wageni unakuta watu wazalendo au kwa njia wanazozijua wao kwenye mawizara wengine baadhi yao watendaji huwasababishia matatizo sana wale ma-*investors*, hasa katika kuwanyang'anya maeneo au kwenda kusema huyu kafanya kitu hivi wakati wanamsingizia sio kweli. Nchi hii tuweke vitu sawa ndio biashara iende.

Namuomba sana Mhe. Waziri aangalie vipi vya kuja kuendeleza hii biashara pamoja na viwanda na leo tume-*target* kwamba tunataka viwanda kwa wingi, tunataka masoko kwa wingi bila ya

vitu hivi kuvipunguza kodi kupunguza bei, mambo kuweka sawa, mambo ya *TRA* basi nchi hii kwa biashara hatutofika. Mimi sitaki kumlaumu yeye, naona wizara yake kwa sababu hivi mpaka viwekwe sawa nchi hii...

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Nadir- Abdul-latif Yussuf muda wako umekwisha.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Eeh!Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti asilimia 90 nai-*support* na asilimia 10 nangoja majibu yangu ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Nadir- Abdul-latif Yussuf kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Omar Seif Abeid akifuatiwa na Mhe. Hidaya Ali Makame na Mhe. Panya Ali Abdalla ajitayarishe.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru na mimi leo kwa kunipa nafasi ya kuchangia mapema nashukuru sana.

Awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu Mwingi wa Rehma ambaye ametuwezesha tukafika hapa asubuhi na tukiwa kwenye funga hii ya mwezi wa Ramadhan. Namuomba Mwenyezi Mungu atujaalie tuifunge Ramadhan kwa salama, tuione siku kuu, tuifurahie sisi sote kwa amani na salama. Mwenyezi Mungu awape hekma na busara viongozi wetu wazidi kutuongeza katika nchi hii.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya shukurani hizo kwa Mwenyezi Mungu mimi leo nataka nichangie nitaanza katika ukurasa wa 7 ambao kwenye ibara ya 14 inasema, hali ya biashara ya Zanzibar usafirishaji na uingizaji wa bidhaa. Naomba kunukuu kidogo.

Hali ya kibiashara kwa ujumla inaonekana kwamba Zanzibar imefanya biashara ya thamani ya TZS 263,322,000 milioni kwa mwaka 2016.

Lakini hapa kwanza nilikuwa nataka nipate maelezo hizi zilizojatwa hapa ni milioni au ni bilioni kwa sababu kama ni milioni, huu ni mtaji mdogo mno. Na hii biashara nilitaka nijue ni pamoja ni ya serikali tu au ni pamoja na wafanyabiashara. Maana kama ni wafanyabishara kuna wafanyabishara ambao wanaingiza bidhaa nyingi, *amount* kubwa zaidi ya hii.

Sasa nilitaka nijue tu hii tuliozungumza hapa ni bilioni ni matatizo ya kimaandishi tu au ni milioni yenyewe na kama ni milioni yenyewe pia mimi nilitaka nijue ni bidhaa gani ambazo zimeingizwa na zimesafirishwa. Kwa sababu tukenda kwenye usafirishaji tunakuwa huko kuna pesa nyingi sana *billions* ambazo zimetajwa kwamba Zanzibar imesafirisha kwenye *page* ya 48 nikifika nitaizungumza. Tatizo hili Mhe. Mwenyekiti, mimi napenda kunukuu yale maneno ya Rais wetu mpendwa Dkt. Ali Mohamed Shein wakati alipokuwa akifungua au akiweka jiwe la msingi la Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali pale Mazizini.

Mhe. Mwenyekiti, alisema moja katika tatazo tulilonalo ambalo linatusumbua ni takwimu. Upatikanaji wa takwimu imekuwa ni kikwazo kikubwa na bila ya takwimu hatuwezi kuwa na maendeleo. Kwa hivyo ili tuweze kuendelea na tuweze kupanga mipango yetu mizuri ni lazima takwimu zije na uhalisia wake. Mimi bado sijaamini kwamba sisi tumeingiza hii biashara ya milioni 263,322,000. Lakini nitamuomba Mhe. Waziri atakapokuja anipe maelezo kwamba hizi zilikuwa ni *millions* au ni *billions* ambazo zimetajwa kwenye hiyo *page* ya 7.

Lakini pia sisi tuna Kiwanda cha Sukari cha Mahonda. Kiwanda kile kimeanza uzalishaji. Sasa mimi nilitaka nijue hichi kiwanda kinazalisha sukari kiasi gani, kiasi gani inatumika Zanzibar na kiasi gani inauzwa nje ya Zanzibar. Sambamba na hilo kiwanda hiki pia kinazalisha *spirit*, hii *spirit* ambayo haya yeye mwenyewe ameizungumza Mhe. Waziri humo kwamba inategemewa kutumika majiko yatetengezwa ya kutumia *spirit.* Mhe. Mwenyekiti, nilitaka nijue hawa watu wenye hichi kiwanda wawekezaji wanauza hizi *spirit* kwa viwanda vya Bara kwa sasa hivi. Je, wamepewa leseni ya kuzalisha hii *spirit* katika hichi kiwanda cha Sukari cha Mahonda, kama hawajapewa, vipi wanalipa kodi na kodi yao ikoje ya *siprit* ukiachilia mbali kuna vitu vingi tu vinavyopatikana kwenye sukari.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, mimi sina tatizo na Mhe. Amina Salum Ali, najua ni Waziri makini ni mfanyakazi mzuri ni, mama yetu ni mzoefu kwenye serikali. Lakini kwenye mambo haya ya uwiano nikenda kwenye *page* 8 nilitaka nijue tumeambiwa hapa mwenendo wa biashara ya Zanzibar kwenye hili jadweli namba 3, naona hapa kwenye uingizaji *import* kwa mwaka huu 2016 kuna laki moja sitini na saba na thamanini na nane. Sasa sijui ni *tones* au kitu gani ningeomba pia ufafanuzi. Lakini kama ni hivyo kama biashara yetu mwenendo wetu ni huu kama ni wa kuingiza na wa kutoa.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kuna meli hapa zinakuja kutoja nje zinafunga na saruji ma-*tones* kwa ma-*tones*. Sasa mbona hii *volume* naiona iko ndogo kiasi hichi, ukichukulia mbali viwanda vyetu viliko hapo Bara uingiziaji wa bidhaa, kuna bidhaa za vifaa vya ujenzi kama nilivyotaja saruji, nondo, *pipes* na vitu vyengine vingi ambavyo vinaingizwa kutoka Tanzania Bara. Kwa hivyo ningeomba ufafanuzi na hili mimi nilikuwa nasihi sana kwamba

wakati wa kuyaandika haya, sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi mutwambie kama hizi, maana yake hapa nimeona kwamba kuna *T.shillings* mia moja sitini na saba labda ndio hivyo. Lakini bidhaa za kiasi gani ambazo ujazo wake imeingizwa kwa mwaka na wafanyabiashara wetu ionekane kama kwenye takwimu kwamba wafanyabiashara wa chakula wameingiza kiasi hichi kutoka Bara na kutoka nje kiasi hiki, ili sisi tuweze kujua na kuishauri vyema serikali.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu bila ya takwimu tukajua kinachoingia halisi ni kiasi gani hatuwezi kuishauri vizuri serikali. Lengo letu ni kuangalia na kuweza kuishauri vizuri, kwa sababu siku zote tunajua kwamba wafanyabiashara siku zote ni mtu aliyekuwa anapenda kuvutia upande wake. Lakini mambo kama haya yatakapowekwa wazi ikajulikana, inakuwa ni rahisi hata kwetu sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuweza kushauri.

Lakini nikienda kwenye *page number 9* hapa naona kuna-*tones* laki moja hamsini na mbili mia tisa sabini za chakula, mchele, sukari na ngano unaona nimeiona hiyo. Sasa pia ningependa kujua na kupata ufafanuzi wake hali ya bei ya chakula na uingiaji wake na vipi. Napenda kunukuu, "Aidha katika kipindi hiki cha mwaka 2016, Zanzibar iliingiza kutoka Tanzania Bara bidhaa zenye thamani hiyo shilingi milioni 138, ikilinganishwa na uingizwaji wa bidhaa ya shilingi milioni 94 kwa mwaka 2015".

Mhe. Mwenyekiti, idadi hii ni ndogo sana. Leo majahazi sikuambii meli na vitu vyengine, majahazi yanayotoka Tanga kuja pale Pemba tu, sita au manane yanayoingia kwa kila wiki inapita hii na hili, na hili ni tatizo ambalo tunalikuta. Kwa hivyo mimi naomba sana kwamba kitengo chako cha kuchukua takwimu za mizigo inayoingizwa kifanye kazi vizuri na kitoe takwimu vizuri

ili na wewe zikupe hesabu vizuri uweze kusimamia vizuri. Vyenginevyo itakuwa sisi tutasema aah! mama mara hii kaamua kutudanganya?, Jambo ambalo hulifanyi, mimi naamini hulifanyi. Lakini sasa hili nakuomba sana ulisimamie ili tupate takwimu sahihi ya bidhaa inayoingizwa kutoka Bara.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, nataka sasa niingie katika kazi yangu ya karafuu. Mhe. Mwenyekiti, kazi yangu ya karafuu nimeiona mara hii kwamba Shirika la *ZSTC* lilinunua karafuu hadi kufikia tarehe 30/03/2017 tani 2,257.7 ikiwa ni sawa na *kilograms* milioni 2,257,700 kwa bei ya shilingi 14,000 kama ulivyonieleza, na swali hili Mhe. Waziri niliwahi kukuuliza na ukanijibu na leo umenijibu tena kwamba karafuu zinanunuliwa kwa *grade* tatu ambavyo ndivyo ilivyo.

Lakini ukitizama sasa uhalisia, tukirudi kwenye uhalisia utakuta kwamba wanasema thamani ya *T.Shillings* ambazo karafuu hizo zimenunuliwa ni shilingi bilioni 31.7. Sasa ukizigawa pesa hizo shilingi bilioni 31.7, ukizigawa kwa kilo 2,257,700 basi utakuta kila kilo moja inasimama elfu kumi na nne na shilingi arubaini, ambazo hesabu hii ilitakiwa iwe ni ya *grade one* tu. Swali hili nililiuliza na leo limejirejea tena vile vile lakini sijui kwa nini. Nina wasi wasi wa jambo moja Mhe. Mwenyekiti, kwamba wakati wa kuandika hii bajeti maafisa wako wana tabia ya kukopi baadhi ya maneno au ya ku-*paste,* wana-*edit* baadhi ya vitu na haya ni matatizo. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, mimi namuomba Mhe. Waziri akitoka aigae hiyo hesabu na utaione hiyo hesabu ninavyokuambia. Hapo hakuna daraja la pili wala hakuna daraja la tatu, yote imesimama elfu kumi na nne na shilingi arubaini, wakati karafuu zinanunuliwa *grade one* kwa shilingi 14,000 tu. Mhe Mwenyekiti,

ukiichukulia hesabu hiyo ukiifanyia basi utakuta kuna tofauti ya pesa ya shilingi milioni 90,308,000. Mimi naomba sana wakati tukifanya mambo haya tuwe wazuri na tuweke kila kitu wazi, kama karafuu daraja la kwanza tumezinunua hivi, daraja la pili hivi, daraja la tatu hivi na thamani yake hii na gharama ya uendeshaji ni hii. Kwa hivyo hapo tutakuwa hatuna masuala tena, lakini ukituambia hivi sisi tunaingia tunaona mambo kama haya, inakuwa Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri mama yetu mpendwa hayapendezi.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, mimi nawaomba sana watu wa *ZSTC*. Mimi pale naona kama roho yangu ya pili kwa sababu uchumi wa nchi yetu kwa asilimia kubwa uko pale. Hivyo tuwe makini katika kutekeleza majukumu yetu haya, haya ni majukumu mazuri na makubwa ambayo tunayo. Serikali yetu imefanya jambo kubwa, imetoa pesa nyingi kwa wakulima asilimia 80 katika ulimwengu, mimi nasema Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein ni Rais wa kupigiwa mfano, kuchukua asilimia 80 akairudisha kwa wakulima ili wanufaike.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, mimi Rais huyu sitamsahau mpaka kufa kwangu kwa sababu huko tulikotoka tuliambiwa na tukaimbiwa na nyimbo sisi. Kulikuwa na bwana mmoja akiitwa Bambuti, alituimbia wimbo kwamba kilo moja shilingi ishirini mwaka wetu ndio pishi moja za kuchuma. Lakini leo mchumaji anachuma karafuu analipwa kibarua shilingi 2,000. Mhe Mwenyekiti, zao la karafuu ni mkombozi, inatoa ajira kubwa sana kuanzia kwa mwenye shamba, kibarua, anayekodi, mwanikaji, serikali yenyewe inapata faida. Kwa hivyo mimi ikizungumzia suala hili nazungumzia likiniuma, wakati haijaishia hapo na mbebaji pia anayezitoa kule kwenye ile kambi kunakochumwa karafuu

kuzipeleka sokoni, kuna wasafishaji wa mashamba, hii ni ajira kubwa sana.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri mama yetu Mhe. Bi. Amina nakuomba suala la *ZSTC* ulielekezee macho sana na sisi ukitutaka tuwe nyuma yako kwa kukushauri bure tutakufuata tuwe pamoja. Lengo letu ni kuona kwamba Shirika la *ZSTC* linafanyakazi zake vizuri, linaendelea, tunapata faida kubwa na nchi yetu inanufaika na watu wetu wananufaika. Leo msimu unaokuja huo watu wote sasa hivi roho zao zimeshakaa mikarafuuni, kila unayemsikia anakuambia karafuu lini tunaanza kuchuma. Hii ni neema kubwa. Hivyo tumpongeze tena Rais wetu kwa kuuona umuhimu wa karafuu na kuupa kipa umbele na ndio maana Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi mimi kila nikisimama namuuliza masuala ya mashamba ya mikarafuu

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Omar Seif Abeid, naomba umalizie.

Mhe. Omar Seif Abeid: Aah! Mhe. Mwenyekiti, unanionea kidogo nakuomba kwa heshima na taadhima zote leo uniazime dakika tano.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe naomba umalizie.

Mhe. Omar Seif Abeid: Basi ahsante sana, nimemaliza.

Baada ya haya nataka niende kwenye hawa wajasiriamali. Mhe. Mweyekiti, kwenye vikundi vya ujasiriamali nilipokuwa natembelea na Kamati yangu Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa, tulifika kwenye eneo moja la Mtambile, tukenda tukawakuta wajasiriamali ambao ni walemavu, walituambia maneno mengi na moja katika maneno waliotuambia ya kilio

chao, ni kwamba wanazalisha bidhaa bora lakini wamekosa masoko, na hapa tunaiona hii programu ya uendelezaji wa masoko. Mhe. Waziri nakuomba katika programu hii tuwaangalie zaidi wale watu wenye ulemavu ambao wana vikundi vyao vya ushirika na ni wajasiriamali ili tuweze kuwaendeleza, tukifanya hivi basi tutakuwa tumewasaidia wao, tumeisaidia serikali na sisi wenyewe pia tumejisaidia.

Baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima nasema naunga mkono hotuba hii lakini atakapokuja Mhe. Waziri anipe maelezo kidogo ili niridhike na mimi roho yangu juu ya bajeti yako.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Omar Seif Abeid kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Hidaya Ali Makame atafuatiwa na Mhe. Panya Ali Abdalla na Mhe. Suleiman Makame Ali ajitayarishe.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipatia na mimi nafasi ya kuweza kuchangia machache juu ya hotuba hii ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko.

Kwanza kwa kuanza na mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia na leo tukafika hapa tukiwa katika hali ya uzima na afya. Lakini tu niwaambie Waislamu wote kwamba tumo katika mwezi mtukufu wa Ramadhani, kwa hivyo tujitahidi kuyafanya yale yote ambayo Mwenyezi Mungu anayapenda kwetu na ni wajibu wetu Waislamu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuanza na mimi nianze kwa kumpongeza sana Mhe. Waziri kwa hotuba yake hii nzuri ambayo imetupa

moyo. Lakini pia kutuamsha ari vijana kujijua kwamba na sisi vijana sasa hivi tunaweza tukafanyakazi na ikaonekana kwamba ni kazi kutokana na maelezo mengi ambayo yameelezwa katika hotuba hii. Pia kutokana na maelezo ya miundombinu mbali mbali ambayo kayaweka Mhe. Waziri kwa mpango kazi huu wa mwaka 2017/2018, tuna nia vijana ya kwamba na sisi tutainuka kimaisha na hali yetu ya kiuchumi katika nchi yetu itazidi kuimarika.

Mhe. Mwenyekiti, moja kwa moja niende kenye suala la wajasiriamali. Mhe. Waziri humu alitueleza mambo mengi na kuna mipango mingi ambayo inatarajiwa kutekelezwa kwa ajili ya wajasiriamali wadogo wadogo, lakini pia kuimarisha suala la viwanda vidogo vidogo. Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa kuliona suala hili lakini pia kwa kuwaona wajasiriamali kwamba ni watu ambao wanahitaji kusaidiwa kwa asilimia mia moja. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti, tukiangalia katika nchi yetu hii tunaona kwamba wajasiriamali ni watu wenye kuhangaika na kutafuta kila hali kuona ni jinsi gani wanajikwamua na kimaisha. Pia tunampongeza Rais wetu Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein tumemsikia katika hotuba zake mbali mbali jinsi anavyowapa moyo wananchi wake, lakini pia jinsi ya kupambana na hii hali ya umaskini katika nchi yetu. Mhe. Mwenyekiti, tumpongeze sana Rais wetu kwa kuwajali watu wake lakini pia kwa kuwajali wananchi wake wote kwa ujumla. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti, kuna haja kubwa ya kuwaangalia wajasiriamali, wajasiriamali hawa wamegawika katika sehemu tofauti. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri hapa alisema katika hotuba yake kwamba kuna hawa wajasiriamali ambao wako kwenye vikundi, lakini katika maelezo yake hapa kuna kitu kama

kimenipa wasi wasi kidogo, kwa sababu katueleza kwamba kuna vikundi saba ambavyo vimeshapatiwa usaidizi na ushauri wa kitaalamu, na vikundi hivi ametuambia kwamba vyote saba ni vya kutoka Pemba. Mimi nimuulize tu Mhe. Waziri hivi kweli hivi vikundi vya ujasiriamali katika Zanzibari yetu hii yote ndio viko kutoka Pemba tu. Je, hivyo vikundi hata huko Pemba kweli ndio viko saba tu hakuna vikundi vyengine ambavyo vinahitaji kusaidiwa na vinahitaji wataalamu, ili kuweza kuviimarisha vikundi hivi. Mhe. Mwenyekiti, mimi ningemuomba Mhe. Waziri hapa aje anipe maelezo ni namna gani walivyofanya mpaka wakapata hivi vikundi saba tu na vikundi vyenyewe vyote ni kutoka Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli tunaona kwamba katika nchi hii wajasiriamali wamegawika katika kila Mkoa na kila Wilaya pia wapo. Lakini kwa kuzingatia vile vile kuna hawa wajasiriamali ambao ni vikundi vya vijana, vikundi hivi vinakuwa vinakosa nyenzo na muelekeo kutokana na hali ngumu ya usaidizi, lakini pia hali ngumu ya kimaisha kwa sababu ukimuangalia kijana ni mtu ambaye anahitaji muda wote kusaidiwa, kupewa mawazo na pia kupewa maelekezo jinsi ya kujitatua na hali ngumu ya maisha.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri akinieleza kwamba kuna vikundi saba ambavyo ndio vimepatiwa huo usaidizi, mimi nitakuwa katika hali ya unyonge. Kwa sababu hivi vikundi saba vyenyewe pia hukutufafanulia ni vya namna gani. Kwa hivyo ningemuomba sana Mhe. Waziri uje utuambie hivi vikundi kweli vimewekwa katika kipaumbele gani ili viweze kusaidiwa na viweze kuonekana kwamba navyo vinafanyakazi ya kuisaidia nchi yao, lakini pia kujiendeleza kimaisha wao wenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitalizungumzia sana hili suala la ujasiriamali. Kwa sababu tunafahamu kwamba wananchi wengi waliopo mitaani sio wote wapo katika ajira za serikali au na ajira nyengine za makampuni binafsi, wapo wengi ambao ni wajasiriamali. Lakini nikizungumzia vijana Mhe. Mwenyekiti, kuna vikundi vingi ambavyo sasa hivi vipo vya vijana. Kuna hawa vijana ambao wanajishughulisha na kazi za mikono kama hivyo kufuma au kutengeneza sabuni. Lakini pia kuna hivi vikundi vya vijana ambavyo vinajishughulisha na masuala ya ukulima wa mboga mboga na ukulima wa *spices*.

Mhe. Mwenyekiti, katika Wilaya ya Magharibi tunaona ni mkoa ambao sana masuala haya ya viungo uko katika kipaumbele. Lakini tukiliangalia suala hili tunakuta kwamba ile nguvu ya hawa vijana kufanya hii kazi inakuwa ni ndogo, kwa sababu tukiangalia kwanza kwenye suala la masoko vitu hivi masoko yake ni makubwa huko duniani lakini kwa hapa kwetu ni madogo, kwa sababu wanaona hawanufaiki na hizi biashara zao.

Mhe. Mwenyekiti, tukiangalia kwenye suala la *spices* kuna ukulima huu wa kungu manga, pilipili manga, mdalasini, manjano na tangawizi. Mhe. Mwenyekiti, vijana wengi wamehamasika katika shughuli hizi za ukusanyaji wa pilipili manga, pia ukusanyaji wa kungu manga kupita kwenye kila mitaa kununua hivi vitu. Lakini utakuja kwamba vijana hawa wanaanguka kimitaji kutokana na hizi hali za biashara zilivyo. Soko lake kwa hapa kwetu linakuwa ni dogo tofauti na huko nje wanakokwenda. Huko nje wanakokwenda kupeleka biashara hizi huwa wanakumbana na changamoto kubwa za kisafari.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, ningemuomba sana Mhe. Waziri akaliangalia suala hili, angefanya kila hali katika hivi viwanda

vidogo vidogo ambavyo umeviandika katika bajeti yako hii kuviimarisha, ukaviangalia viwanda vidogo vidogo vinavyohusu suala la *spices* ili kuweza kuliimarisha suala hili, kwa sababu tunaliona suala hili hata kwenye masuala ya kitalii lina kipa umbele kikubwa. Mhe. Mwenyekiti, tukiangalia kwenye suala hili la utalii Kizimbani magari hayaondoke wakati wowote watalii wanakwenda kuangalia masuala haya ya *spices*, lakini pia na vijana wanapata moyo kuona hawa wazungu au watalii wanakwenda kule kuangalia haya masuala ya *spices* na wakaweza kupata pesa mbili tatu. Lakini bado suala hili kwa hapa kwetu liko chini na umakini wake kiufupi bado uko mdogo. Kwa hivyo ningekuomba sana Mhe. Mwenyekiti, maeneo yapo ufanye kila hali ili kuona hivi viwanda vidogo vidogo vinaimarishwa na suala hili linapatiwa ufumbuzi kwa vijana wetu hawa, ili waweze kujiajiri na waweze kupata chochote katika maisha yao.

Mhe. Mwenyekiti, pia nizungumzie suala la kuhusu hali za kibiashara kutoka hapa kwetu Zanzibar kwenda Tanzania Bara. Mhe. Mwenyekiti, katika maelezo ya Mhe. Waziri hapa alitaja baadhi ya vitu ambavyo vinapatikana kutoka Tanzania Bara kuletwa hapa kwetu kwa ajili ya biashara na masoko. Lakini hakutuandikia vitu ambavyo na hapa kwetu vinatoka kwenda kule na tunafahamu kwamba pia hapa kwetu vipo vitu hivi ambavyo vinatoka kwenda Tanzania Bara. Tukizingatia vitu hivi hususan vinakuwa ni vya matunda.

Mhe. Mwenyekiti, ningemuomba sana Mhe. Waziri aliangalie suala hili, sio kama hapa kwetu hapana hizi bidhaa ambazo zinapelekwa kule Tanzania Bara. Mhe. Mwenyekiti, tunajua kwamba shokishoki, sifikirii mimi Tanzania Bara kama kuna sehemu ambayo inalimwa shokishoki, shokishoki zinatoka hapa kwetu. Lakini pia ukulima wa mastafeli sasa hivi umezidi kuwa

mkubwa kutoka hapa kwetu kwenda Tanzania Bara ijapokuwa na kule yapo, lakini na hapa kwetu tunajua na tuna uhakika kwamba yanatoka kupelekwa kule na yakifika kule bei inakuwa ni kubwa zaidi kuliko iliopo hapa kwetu.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo tunakuomba sana Mhe. Waziri uyaimarishe masoko yetu haya ya vyakula vyetu hivi vya matunda, ili na sisi tuone faida ya wakulima wetu wanaolima mazao haya na matunda na wao waweze kufaidika, kulikoni kutoka mtu hapa akayapeleka huko, ile gharama ikazidi kuwa kubwa ya usafirishaji na mengineyo kuliko kutoka kule akaja hapa lile soko na sisi likaweza kuwa kubwa zaidi na nchi yetu ikaweza kufaidika pamoja na wananchi wake.

Mhe. Mwenyekiti, matunda yapo na watu wanajitahidi kulimwa kwa sasa hivi. Nimuombe sana Mhe. Waziri viwanda vidogo vidogo vina umuhimu sana kwetu kwa sasa hivi lakini pia vitatuwekea hali nzuri ya kiuchumi kwa wananchi wetu na kuingizia pato kwa wananchi wetu na Serikali yetu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi leo nisingependa nizungumze mengi ningemwambia sana Mhe. Waziri wakulima wadogo wadogo ni wakulima ambao na wao wanajitegemea, pato lao ni dogo lakini na masoko yanawakwaza. Mhe. Mwenyekiti, tunaona kwamba katika kipindi kikubwa wakulima hawa wanakuwa katika hali duni mpaka inapofika mwezi wa Ramadhani ndio soko lao angalau ndio linakuwa kubwa kidogo kutokana na huu mwezi mtukufu. Lakini hapa hapa ukiangalia kwa hali nyengine inakuwa ni tofauti kwa sababu kupandisha vitu bei kwa mwezi wa mtukufu kama huu, kwanza sijui tunajijengea gani katika maisha yetu lakini pia tunakuwa kama tuna ukosefu wa imani hata kwa Muumba wetu. Kwa sababu kama ni soko basi liendelee siku zote

lisiwe kwa mwezi mmoja tu hususan huu mtukufu wa Ramadhani, kwa sababu kila mtu sasa hivi amekuwa vile vitu vya muhimu basi hawezi kuvitoa mpaka ifike mwezi mtukufu wa Ramadhani, yeye ndio anaweza kufanya zile biashara zake ilimradi tu anajua hapa ndio nitapata chochote. Kwa kweli hii hali inasikitisha na haiko vizuri. Mhe. Mwenyekiti, tungemuomba sana Mhe. Waziri alizungumze sana suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la nazi. Ningemuomba sana Mhe. Waziri nazi sasa hivi imekuwa ni kitu adimu katika nchi yetu wakati tunaambiwa kwamba hapo nyuma hii nazi ilikuwa ni kitu ambacho wewe utoke pale nyumbani kwako uzunguruke nyuma tu basi unarudi na nazi bindo zima. Lakini sasa hivi imekuwa ni tofauti kutokana na hali iliopo tuseme kama ni tamaa kwa wananchi wetu hasa wanaomiliki haya mashamba ya minazi.

Mhe. Mwenyekiti, tunafahamu kwamba vilikuwepo viwanda vya mafuta lakini vilikuwepo viwanda vya mbata, lakini pia nazi hizi hizi zilikuwa zinatumika kwa kila hali kwenye kila jitihada kutokana na kwamba hizi nazi zilikuwa nyingi na minazi ilikuwepo ijapokuwa tunaambiwa sasa hivi minazi ile inakatwa, lakini mimi naweza nikasema kwamba hii minazi inakatwa kutokana na kwamba haizai, ndio maana mtu anaukata mnazi kwa sababu minazi tayari imeshakuwa mipevu mingi yao, lakini na hiyo ambayo sio mipevu haina uzazi kama ule wa mwanzo. Kwa kweli zao hili sasa hivi limeshuka sana katika nchi yetu kutokana na kwamba hawa wakulima wanaomiliki mashamba haya au wanaokodi mashamba haya ya minazi utaratibu wa majangusho umekuwa ni mbovu.

Mhe. Mwenyekiti, utaratibu wa majangusho ulikuwa ni kwa kila baada ya miaka mitatu au mitano kiufupi, lakini sasa hivi tunaona

kwamba kila baada ya mwezi mmoja na nusu au siku kumi na tano mtu anapanda mnazi anakwenda kufanya majangusho. Je, tujiulize hili soko litakuwepo au litakufa. Kwa kweli hii hali imekuwa ni mbaya na inasikitisha. Sasa hivi sisi tunatoa nazi kutoka Tanga au kutoka Bara hali ambayo ilikuwa ni tofauti hapa, hapa kwetu sisi ndio tulikuwa tunatoa nazi kupeleka nje, sasa hivi ndio tunapokea. Jambo ambalo liko kinyume na ni tofauti kwa hali ya nchi yetu ilivyokuwa. Ningemuomba sana Mhe. Waziri aliangalie sana suala hili lakini kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo waliangalie kwa umakini mkubwa suala la upandaji wa minazi lakini na soko lake pia ila na uimarishwaji wa hii minazi na kutafutwa viwanda vya kutengeneza mafuta yetu ya nazi ambayo kila mtu anayajua umuhimu wake.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia nimuombe sana Mhe. Waziri, viwanda vya *spices* tunahitaji sana katika nchi yetu, ukizingatia suala la *spices* lina umuhimu mkubwa katika afya lakini pia kuingiza wageni wetu au hawa watalii katika nchi yetu, wanavutika sana na vivutio hivi, lakini na masoko yake yaimarishwe, yawe yanawapa moyo na nguvu hawa wananchi wanaohusika na kujiimarisha na suala hili la uimarishwaji wa hizi *spices,* lakini pia kwenye masuala ya *spices* hizi za urembo.

Mhe. Mwenyekiti, nimelizungumzia suala la miti hii ya milangi langi…….

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hidaya muda wako umekwisha.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Namalizia Mhe. Mwenyekiti. Milangi langi, mipachori na mihaliudi tunaona kwamba nalo soko lake linakuwa ni dogo na hata hiyo miti yenyewe nayo inapotea. Ningemuomba sana Mhe. Waziri nayo kwa kushirikiana na

Wizara ya Kilimo miti hii nayo imarishwe ili izidi kuwepo na soko lake pia liwepo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumaliza na mimi naunga mkono hotuba hii asilimia mia moja ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Hidaya Ali Makame, sasa naomba nimwite Mhe. Panya Ali Abdalla kifuatiwa na Mhe. Suleiman Makame Ali na Mhe. Rashid Makame Shamsi.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote na mimi nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujaalia uhai tukaweza kukutana hapa katika Baraza lako hili tukufu, lakini pia nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema yake aliyotuletea ya kuweza kutufikisha katika mwezi huu mtukufu wa Ramadhani ambao sisi Mwenyezi Mungu aliotujaalia kuudiriki na kukutana nao, basi namuomba Mwenyezi Mungu atujaalie tuweze kupata afya njema, tuweze kuufunga kwa salama na inshaallah Mwenyezi Mungu atujaalie zile fadhila zote alizozipanga katika mwezi huu mtukufu aweze kutujaalia tuweze kunufaika nao inshallah.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo nichukue fursa hii kumpongeza sana sana Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko kwa kazi kubwa na nzuri na kwa kweli niseme huyu mama ni mzalendo kabisa wa nchi yake. Mhe. Rais tunampongeza sana kwa kututeulia mama huyu kwa sababu anaijali sana nchi yake na mtu akiijali nchi yake basi huwa anaipendelea mambo mazuri wakati wote, inshaalllah Mwenyezi Mungu atakupa nguvu na uwezo uweze kutuendesha vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze mchango wangu katika ukuzaji wa ujasiriamali na ushindani wa kibiashara. Kwanza niishukuru Serikali sana kwa kuona kwamba kuna umuhimu wa kuibadilisha ile Sera na Sheria ili wajasiriamali wetu hawa waweze kupatiwa mitaji mkubwa ya kuweza kuendesha biashara zao. Kwa kweli hili ndilo tegemeo la Wawakilishi wote ambao tuko hapa, siku zote tunakuwa tunaomba Serikali iweze kuwaona wajasiriamali hawa katika kuwaongezea mitaji yao ili waondokane na zile biashara ndogo ndogo tu na ili waweze kukua sasa wafanyabiashara hawa ili waweze kufanya biashara kubwa na biashara zao tukizingatia kuweza kuzipatia masoko. Mhe. Mwenyekiti, mfanya biashara siku zote anaanza na biashara ndogo lakini huwa hategemei agande pale pale tunategemea lazima mfanya biashara huyu iko siku basi ageuke awe na yeye ni mfanya biashara mkubwa, ili aweze kujisaidia yeye mwenyewe lakini hata kuisaidia nchi yake katika kuiongezea mapato ya Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli wajasiriamali ambao tunao na mimi niiombe tu Serikali, hasa niziombe hizi Wizara tatu; Wizara ya Kilimo, Wizara ya Uwezeshaji na hii Wizara ya Viwanda na Masoko. Kwa kweli wizara hizi zikifanya kazi katika muungano mzuri wa kuungana wao katika utendaji wao wa kazi basi nadhani tunaweza tukafika pahala pazuri sana, kwa sababu tukiangalia tuna muwezeshaji na akiweza kuviwezesha vikundi vyetu halafu mzalishaji pale Wizara ya Kilimo akaweza kuzalisha kile kinachotegemewa, lakini mwenye masoko akaweza kuzitafutia bidhaa hizi masoko, naamini tutaweza kupunguza kwa kiasi kikubwa uagiziaji wa bidhaa kutoka nje. Mhe. Mwenyekiti, tunao uweo kilimo akiamua kushughulikia kilimo cha *Irrigation* tunaweza tukazalisha mchele mwingi hapa kwetu pamoja na kwamba tuna eneo dogo lakini kama tutajipanga vizuri tunaweza kufanya kazi hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niziombe Wizara hizi zifanye kazi kwa mashirikiano makubwa ili basi ziweze kuwasaidia wajasiriamali wetu, wazalishaji wetu au wenye viwanda wetu wadogo wadogo waweze kufikia katika hatua moja kubwa kabisa. Mhe. Mwenyekiti, pia nilitaka ukjua Mhe. Waziri atakapokuja hapa aweze kunifafanulia kati ya *ZBS* na *ZFBA.* Taasisi hizi naziona zinafanya kazi ya ukaguzi kama kwa pamoja. Je, hakuna mgongano wowote ambao unaosababisha kuweza kukwazana katika majukumu kwa sababu hawa kama wanaangalia bidhaa za chakula na hawa wanaangalia, au hatuoni kama hapa tunatumia fedha nyingi katika kuwawezesha hawa na wote wanakagua kitu kimoja. Mhe. Mwenyekiti, nilitaka basi atakapokuja Mhe. Waziri aweze kuipa ufafanuzi juu ya taasisi hizi mbili.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, pia nikiendelea na mchango wangu pamoja na juhudi kubwa ambazo Serikali inafanya, kwa kusema kweli Serikali inajitahidi na jitihada tunaziona lakini bado niseme katika uletaji wa bidhaa mbovu bado kunahitaji ukaguzi wa kina kabisa. Mhe. Mwenyekiti, bado kuna wafanya biashara ambao wanaonekana si waaminifu wala hawajali afya za wenzao, bado mchele mbovu upo, bado bidhaa nyengine mbovu zipo. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, mimi nikuombe na wewe najua ni mtu makini sana hupendi kuona Wizara yako inapata misuko suko kama hii, najua utalifuatilia kwa kina. Kwa hivyo bado watu hawa wapo tuweze kuwasaka na kuona wanatutendea haki katika kutupa vyakula ambavyo vina kiwango.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia nilitaka kuzungumzia juu ya biashara hii ambayo naona kwa sasa utamaduni umekuwa mkubwa, biashara ya *pampers.* Biashara hii imekuwa kwa kiasi kikubwa iko tofauti na ule utamaduni wetu sisi ambao tuliuzowea, sisi tulikuwa tukitumia nepi na vitambaa na ilikuwa inatuweka wasafi

zaidi na ilikuwa pia haiwezi kuharibu mazingira kama ilivyo sasa. Mhe. Mwenyekiti, lakini mimi nilitaka tu kujua kwa sababu nahisi tunakwenda tukinunua, upo uangalizi mzuri kuhusu viwango vya hizi *pampers* zinazoingia katika nchi yetu. Lakini pia ukaguzi kuhusu mwisho wa matumizi wa hizi *pampers* upo unaangaliwa vizuri, lakini pia nilitaka kujua kama Wizara imefanya utafiti wowote juu ya hizi *pampers* kuwa hazina madhara kwa watoto wetu ambao tunawavisha. Kwa sababu mwisho wa siku kitu kikija kama hichi kipya ni vizuri tukakifanyia utafiti mapema ili basi tuweze kujua usalama wake ili tusije tukagundua baadae huko mwisho kwamba kumbe *pampers* zina madhara fulani. Kwa hivyo mimi nilitaka kujua hilo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niseme sina mengi sana ya kuzungumza katika Wizara hii, kwa sababu mwenye kitabu hichi nimpe sifa moja kubwa ambayo ameieleza katika kitabu chake na imekosekana katika baadhi ya vitabu vyengine. Mhe. Mwenyekiti, ni kuzieleza changamoto na kujua kama kuna changamoto ni suala moja, lakini ukizielezea kwamba changamoto hizi ndio zinazonikwaza, maana yake tuseme umejiweka tayari katika kujirkebisha au kuzitatua taratibu changamoto hizo. Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa kuweka hizi changamoto kwa sababu imezidi kutupa moyo kama ataweza kuzishughulikia na sisi tunamuombea Mwenyezi Mungu aweze kushughulikia changamoto zake zinazomkwaza ili Wizara hii iweze kuendelea vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kwamba tunasema sisi ni maskini lakini kama tutajipanga vizuri umaskini utatuondoka na tutaweza kuishi katika mazingira mazuri. Nchi yetu hii ni ndogo tunatakiwa tujipange tu vizuri, tukijipanga vizuri tutaweza kufikia mafanikio makubwa kabisa katika nchi yetu, hatuna haja hapa sisi hapa ya

kuagiza baadhi ya vitu, wajasiriamali wafugaji wa kuku tukiwawezesha kufuga kuku tukawapa mitaji mizuri, tukawapa wataalamu bila ya shaka kuku sisi hatutaagiza kutoka nje. Mhe. Mwenyekiti, tunaweza tukafuga na tukalidhibiti soko letu la ndani, tunaweza wajasiriamali hawa mwisho wa siku tukawaona ni wafanya biashara wakubwa kabisa na wanaweza kuzalisha hata na wao wakawea kuuza nje.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ilitaka niseme hayo tu na niseme naiunga mkono hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko kwa asilimia mia moja na inshaallah Mwenyezi Mungu atakuwezesha na ataiwezesha Serikali hii katika mipango yake mizuri ambayo inajipangia kwa kila siku.

Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Panya Ali Abdalla kwa mchango wako. Sasa naomba nimuite Mhe. Suleiman Makame Ali atafuatiwa na Mhe. Rashid Makame Shamsi.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko.

Kabla ya kutoa shukurani zangu kwanza niwape Ramadhan Kareem wananchi wangu wa Jimbo la Ziwani na wananchi wa Zanzibar kwa ujumla, kuwatakia mwezi mwema wa mfungo wa Ramadhani, Mwenyezi Mungu atupe kila lenye kheri na baraka ndani yake.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye ukurasa wa 47, "Shirika la Biashara (*ZSTC)"*. Hapa tunapitisha bajeti lakini mimi nilitaka

kujua kwa sababu kidogo nina mushkeli hapa, walisema kwamba uvunaji na usafirishaji wa karafuu, wanasema "Shirika la Z*STC* lilijiwekea lengo la kununua karafuu tani 2,810 kwa thamani ya Shilingi Bilioni 39 kwa msimu wa mwaka 2016/2017, hadi kufikia tarehe 30 mwezi wa March, 2017 jumla ya tani 2,257.7 za karafuu zimenunuliwa kutoka kwa wakulima zenye thamani ya Shilingi bilioni 31.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, mimi sijasoma sana lakini hapa kidogo niliumiza kichwa na nikafanya hesabu yangu, nikaona kwamba hizi karafuu zote zimenunuliwa kwa bei moja ya shilingi elfu kumi na nne ambayo ni *grade one*. Ssasa mimi nikitaka nijue hakukuwa na *grade two* huko, hukukuwa na *grade three* huko na hapa walisema kwamba *grade one* ni Shilingi ni kumi na nne, *grade two* ni shilingi elfu kumi na mbili na *grade three* ni shiling 10,000, lakini sasa hapa karafuu zote zimenunuliwa kwa bei moja na mimi najua kwamba karafuu kuna mpeta na *grade* nyengine ambaza ndio za chini yake.

Kwa hivyo mimi nataka nijue kulikoni na najua kwamba karafuu *grade* wano *grade two* na *grade three* zipo. Sasa ndio kweli hazikupatikana hizo ndio karafuu zote zimepatikana *grade one* tu. Lakini pia nikitaka kujua vile vile kwamba hichi kitabu walivyotuandikia walikuwa waeleze hapa kwamba *grade one*, tumenunua kiasi hichi, *grade* three tumenunua kiasi hichi na *grade two* tukanunua kiasi hichi na thamani yake ni hii hapa kwa pesa hii hapa. Sasa Mhe. Mwenyekiti, tukenda hivi itakuwa sasa tuhoji sana, tukisema jambo tutakujaambiwa tunakiuka Kanuni. Lakini hapa Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nifafanuliwe zaidi ili wananchi pamoja na Baraza hili wapate kufahamu kwenye ununuzi huu wa karafuu, isijekuwa tunavunganywa vunganywa.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende kwenye suala la wajasiriamali. Jana Mhe. Waziri hapa alisema kwamba kuna wajasiriamali walitoka hapa Zanzibar kwenda kuuza biashara zao kule Uganda, lakini Mhe. Waziri alizungumza hapa kwamba ni wajasiriamali kumi. Lakini Wizara ya Wanawake na Watoto na Uwezeshaji ikasema imetoa wajasiriamali 27. Kwa hivyo nataka nijue nishike ipi ile 27 au hii 10. Lakini vile vile Mhe. Waziri wa Biashara alisema kwamba aliwasaidia hawa nauli. Sasa ilikuwaje wajasiriamali wale kutoka hapa kwenda Uganda ikabidi sasa waombe nauli, lakini vile vile waweke rehani vitu vyao, kwamba walipofika kule Uganda ile safari ya kutaka kurudi huku wakashindwa ikabidi kuweka rehani vitu vyao, wakauza mikoba wakati mikoba iko Pemba, wakaamua Mheshimiwa nakuuzia mkoba wangu nipe kiasi kadhaa, utafanya nini utachukua kwa sababu unataka kumsaidia.

Lakini pia vile vile Wizara ya Biashara kwa sababu nyinyi ndio mnayoshughulika na masuala ya biashara, muwatizame wale wajasiriamali munapowapeleka kule Uganda kwa biashara gani ina soko. Sio watoke hapa na makombo alawi wanataka kuyajaza kwenye mapolo na makasheba ya mitumba, wakafika kule wakapata mtihani, wajasiriamali wale Mhe. Mwenyekiti, waliuza kuku wao, aliyekuwa na ng'ombe wake akauza ng'ombe wake, aliyekuwa na vitu vyake vyengine kwenye akiba yake akaitoa.

Mhe. Mwenyekiti, akenda kule Uganda kufika Uganda narudi ya kurudia huku pia ikashinda, ule mtaji wake ushapotea. Kwa hivyo Mhe. Waziri nakuomba sana kwenye suala hili la kuwaondosha wajasiriamali kuwapeleka kutafuta masoko, watafutie kwamba ukenda Uganda na biashara hii inakubalika, sio kama umuachie mjasiriamali atoke kule kachukua makombo alawi Mhe. Ali Karume alijiuliza makombo alawi ni nini? Mhe. Mwenyekiti,

alifikiria ni jina na mtu kwamwe, kumbe ni maandazi Mhe. Ali Karume alikuwa hajui. Mhe. Ali Karume ni maandazi yale yanayoitwa masikio wengine wanaita hivyo. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo namuomba sana Mhe. Waziri muhakikishe kwamba kule Uganda au popote wanapokwenda wajasiriamali wetu, kwenda kutangaza zile biashara zao ni biashara gani ambao ile nchi wanakwendea kuuza, ina soko na watapata tija na faida ndani yake. Sio kama wafike kule, watoke hapa wafike kule halafu nauli ya kurudia washinde ni kuwadhalilisha kusema la ukweli.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nende kwenye suala la ukurasa wa 35 "Programu ya Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali". Mhe. Mwenyekiti, ujasiriamali nishaizungumza niende kwenye uendelezaji wa biashara. Kule Pemba kuna bandari ya Mkoani, Wesha na Wete. Mhe. Mwenyekiti, cha kushangaza wafanyabiashara wa Pemba wananyanyasika. Pemba kuna wafanyabiashara tena ambao kwamba wengine wakubwa kwa kuipatia Serikali yetu mapato, wa kulipa *ZRB* mpaka milioni 30 kwa mwezi. Lakini wanalipa pesa hizo, sasa leo mfanyabiashara yule anachukua biashara yake, inatoka inakuja hapa Unguja inashuka pale Malindi anapakia tena kwenye meli anakwenda nayo Mkoani Pemba, gharama mara mbili akauzaje, ni mtihani. Kwa hivyo naomba sana Mhe. Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri hili kuwafikiria wafanyabiashara wa Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, zile bandari zilizoko kule Pemba nazo zitumke, kama itakuwa kuna meli kwamba haihitaji meli ile kuja huku Unguja, basi ibakie kule kule Pemba kwa sababu gani kwamba wale wafanyabiashara itakuwa wakati mwengine wanatoa nguvu kubwa, na pesa zile zinakwenda nyingi sana ya kupakia mizigo

mara mbili. Maana itabidi sasa yeye atowe mzigo kwenye meli ile apagie meli hii ni gharama na wakati wa kushusha vile vile ni gharama. Kwa vile kusema la ukweli ni mtihani. Namuomba sana Mhe. Waziri pamoja na Waziri wa Mawasiliano mukae muliangalie hili, ili muafikirie wafanya biashara wa Pemba kwa sababu wanapata mtihani mkubwa. Mhe. Mwenyekiti, leo saruji mpaka siku nyengine itoke hapa iende Pemba, maskini bandari zipo pale, kuna bandari ya Wesha imekaa tu inafunga majahazi na mashua za madagaa, ile bandari ya Wesha inafaa kwa kushusha meli za mizigo ya kawaida ndogo ndogo.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, leo kuna meli nyengine, juzi mfanyabiashara mmoja alinilalamikia akaniambia Mheshimiwa kusema la ukweli tunaumia na ukitizama ni kweli, mfuko mmoja wa saruji Pemba ni shilingi elfu 15,000 au 16,000. Hapa Unguja ni elfu 14,000 au 13,000 ni mtihani. Lakini sasa mtihani huu unakuja wapi, unakuja huku katika masuala ya usafirishaji kwamba wafanyabiashara yule atowe saruji hapa aipeleke Pemba mtihani. Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo namuomba sana Mhe. Waziri wa Mawasiliano na Waziri wa Biashara ili kuwafikiria sana wafanya biashara hawa wapo wanaofanya biashara yao Pemba ili waweze kuzitumia zile bandari zao.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende kwenye suala la biashara za baharini. Mhe. Mwenyekiti, baharini nako biashara ambazo kwamba zina tija na faida kubwa. Mhe. Mwenyekiti, nadhani kuna wengi hawajui jongoo pau ni nini humu. Jongoo pau hufika mpaka shilingi 100,000, jongoo mweupe hufika mpaka 100,000, kuna vibazi vya kome ni shilingi 100,000, 70,000, 80,000 havishuki hashuki mpaka shilingi 20,000. Ni biashara kubwa lakini biashara hii ya bahari inadharaulika wala haithaminiwi,

wala sipati kuisikia kabisa kwamba biashara ile nayo kidogo inawafanya wale wavuvi nao wapate kunufaika. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, naiomba sana Serikali iweze kuliangalia hili suala la biashara zile za baharini, ikikushana matani ya majongoo hapa, ikenda ikiuza kwa sababu kilo moja ya jongoo ni shilingi 100,000 wakati karafuu ni shilingi 14,000, itakuwa tumeshakuwa na uchumi zaidi. Kwa hivyo naomba sana kuangalia na suala hili la biashara zile za baharini.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende kwenye suala la *Chamber of Commerce.* Mhe. Mwenyekiti, Jumuia ya Wafanyabiashara wenye Viwanda na Wakulima nayo ni mtetezi mmoja wapo ambayo kwamba ya kuhamasisha wafanyabiashara kulipa kodi zao, inajitahidi sana ile Jumuiya, inaweka vikao mara kwa mara kuwaita wafanyabiashara walipe kodi ili Serikali ipate mapato. Lakini sijui niseme nini kwenye Jumuiya ile kama Serikali wanaitambua kwamba ile Jumuiya inafanya kazi nzuri au vipi. Hivyo Mhe. Waziri ninakuomba utakapokuja hapa kutoa majumuisho uniambie kwamba mnashirikiana naje na Jumuiya ya Wafanyabiashara wenye Viwanda na Wakulima ili kuhakikisha kwamba wafanyabiashara wetu wananufaika, lakini pia vile vile na kuwasaidia wale wajasiriamali.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sina mengi ya kusema lakini isipokuwa nataka Mhe. Waziri akija anipe majibu ya shilingi bilioni 31.7 za karafuu bei moja iliyonunuliwa, alipe majibu ili niweze kufahamu vizuri kwamba bei ile ilikuwaje hata karafuu zile zikanunuliwa kwa shilingi bilioni zile pale, zikaonesha *grade* moja na wakati *grade* nyengine zipo.

Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono kwa asilimia 80, asilimia 20 namsubiri mama yaangu Bi. Amina aweze kunipa majibu ya suala langu nililomuuliza.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Suleiman Makame Ali kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Rashid Makame Shamsi akifuatiwa na Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi na Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame ajitayarishe.

Mhe. Rashid Makame Shamis: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipa fursa hii kwa kuchangia angalau machache yahusiana nayo na hotuba hii ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko.

Mhe. Mwenyekiti, awali nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa hotuba yake na uwasilishaji wake fasaha, lakini vile vile niwapongeze watendaji wake wa wizara kwa kuweza kuandaa bajeti hii ambayo kwa kweli imepangika vizuri sana. Niwapongeze vile vile kamati ambayo inahusika na Wizara hii na husuan Mhe. Hamad Abdalla Rashid kwa uwasilishaji wake, niwapongeze vile vile wafanyabiashara, wakulima wa mazao ya biashara na wajasiriamali lakini niwapongeze Wajumbe wenzangu waliotangulia katika kuichangia hotuba hii.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko ni moja kati ya Wizara muhimu sana katika kukuza uchumi na pato la nchi hii. Kwa sababu nchi nyingi ziliozoendelea basi uchumi wake umekua kutokana na sekta ya viwanda. Kwa hivyo ni Wizara muhimu lakini tukubali vile vile kwamba ni wizara tegemezi inahitaji kuwa na mashirikiano sana ya karibu, kwa sababu nchi yetu, raslimali zake nyingi ambazo zingeweza kutumika katika viwanda vyetu vinatokana na mazao ya kilimo.

Kwa hivyo haina budi Wizara yetu hii iweze kuwa karibu sana na Wizara ya Kilimo katika kuona kwamba viwanda vyetu ambavyo vipo viweze kufanya kazi. Lakini vile vile Wizara hii ina wajasiriamali ambao miongoni mwao ndio hawa hawa ambao wanaanzisha viwanda, lakini vile vile tuna Wizara ambayo inashughulika na Kazi na Uwezeshaji ambayo vile vile nayo kwa upande mwengine inashughulikia wajasiriamali.

Mhe. Mwenyekiti, ningependa sana Wizara hizi mbili lazima ziwe karibu sana na ile Wizara ya Biashara kwa sababu inawezekana kukawa na majukumu mengine yanayotekelezwa yakawa yanaingiliana. Ningependa sana wawe pamoja ili kuweza kuona kwamba wajasiriamali wanaoshughulikiwa na Wizara ya Kazi na wajasiriamali wanaoshughulikiwa na Wizara ya Biashara, basi tusije tukaona kwamba tunafanya kazi mbili ambazo zinaingiliana. Nipende sana Wizara hii ya Biashara iwe na mashirikiano na sekta mbali mbali ili kuona kwamba tunapiga hatua.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze mchango wangu baada ya dibaji hiyo katika ukurasa wa 20 kifungu 47 ambapo Wizara ilieleza matumizi yake. Nasikitishwa sana Mhe. Mwenyekiti, na takwimu ambazo zinazoonesha matumizi. Wenzetu hawa walipata fedha asilimia 52 ya bajeti iliyopita na ukitazama majukumu yao bajeti hii kwa kweli mimi naona kwamba au fedha walizoingiziwa, mimi naona kwamba hatukuwatendea haki kwa sababu hotuba ambazo zimepita za Wizara mbali mbali, hakuna wizara yoyote mpaka sasa asilimia yake ya bajeti ilikuwa 50 kwenda chini, nyingi zilikuwa kwenye asilimia 70 na 60. Sasa wenzetu hawa kuwapa asilima 52 sijui pengine makisio yalikuwa makubwa lakini walichoingiziwa kimewatosha, lakini kutokana na ukubwa wa majukumu yao, na sisi tunaelekea katika 2020 ambayo

tunatarajia uchumi wetu uwe uchumi wa kati, uchumi wa viwanda kwa asilimia hii 52, kwa kweli naona kama hatutofika mbali.

Mhe. Mwenyekiti, ukizitazama hata programu zake ndogo ndogo. Kuna programu ndogo ya ushindani halali wa biashara na kumlinda mtumiaji ni programu muhimu sana, lakini ilipata asilimia 2. Ni jambo la kusikitisha kweli kweli kwa sababu hii ni programu ambayo inamgusa kila mwananchi, kama haikutekeleza vizuri kutokana na fedha kidogo walizoingiziwa, maana yake hiyo ni hatari na kuna hatari kwamba watendaji wetu wasifike chini kuweza kukagua bidhaa ambazo tunauziwa sisi walaji.

Matokeo yake tunaweza tukala bidhaa mbovu. Lakini hata ukija huku kwenye ukuzaji wa masoko kuna asilimia 17 ambayo wameingiziwa fedha na ambayo ni asilimia ndogo. Ukija maendeleo ya ujasiriamali wameingiziwa asilimia 14. Sasa hii ni hatari. Mimi nafikiri Serikali niombe hususan Wizara ya Fedha kuweza kuwatizama wenzetu hawa kwamba wana kazi ngumu na hivo Wizara ya Fedha ili waweze kupata fedha basi mara nyingi wanategemea Wizara hii ya Biashara, Viwanda na Masoko. Kwa hivyo tuitazame vile vile katika kuingizia fedha ili yale waliyoyapanga yaweze kutekelezeka vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nije katika ukurasa wa 30 fungu la 71. Kwanza niipongeze Wizara kwa kuendelea na Sera ya Maendelo ya Viwanda. Wenzetu wameeleza kwamba hivi sasa wako katika hatua ya ukusanyaji wa maoni kwa wadau. Ni hatua ambayo ni muhimu sana kwa sababu katika kuandaa sera lazima uwapate wadau muhimu sana. Lakini ukweli Mhe. Mwenyekiti, mimi najiuliza najua sera ndio dira, sera ndio mipango, sera ndio mikakati ya kutekeleza jambo lolote lile. Nashangaa sana mpaka hii leo kwamba Serikali yetu hii haijawa na sera madhubuti ya

viwanda. Wakati tunazungumzia 2020 kuwa sisi tunataka tuingie katika uchumi wa kati, na uchumi wa kati huu lazima tuwe na viwanda. Lakini bado hatuna sera madhubuti ya viwanda. Hii ni hatari. Sasa haya yote tunayoyazungumzia juu ya maendeleo ya viwanda, kama huna sera sijui utakuwa unayatekeleza vipi. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, ningependa sana nimuombe sana Mhe. Waziri aharakishe hatua hizi ya kuweza kuiandaa Sera ya Viwanda, ili haya yote tunayoyazungumza hapa kwa sababu haya yote lazima yawemo katika sera. Kama unatekeleza vitu havimo kwenye sera bila shaka inakuwa ngumu, kwa sababu unapoandaa sera baadae inabidi uwe na Sheria na Kanuni. Mhe. Mwenyekiti, tunataka tuingie katika uchumi wa viwanda lazima tuwe na sera madhubuti ya viwanda. Hiyo ndio ambayo itatupeleka sisi uchumi wetu kuweza kunyanyuka kwa haraka sana. Kwa hivyo nimuombe sana Mhe. Waziri hatua hizi ziweze kuendelea ili tuweze kupata sera nzuri ambayo itasimamia masuala ya viwanda.

Lakini vile vile sera hii sijui kwa taratibu za hivi sasa za Baraza kwa sababu Baraza linakuwa sisi tunatunga sheria lakini mimi ni mpya. Tunatungaje sheria iwapo hatuzielewi sera zinazohusiana na sheria ile. Ningependa sana kama utaratibu huu haupo wa Baraza kuweza kupata sera, basi ni bora uwanzishwe ili tuzione sera halafu tutunge sheria kutokana na sera ile. Mimi nafikiri hapo tunaweza tukazitendea haki sera zetu. Mhe. Mwenyekiti, Wajumbe wa Baraza hili wanahitaji kujua sera za mambo mbali mbali ya nchi hii, ukiacha ile ya kutunga sheria.

Mhe. Mwenyekiti nikitoka hapo nielekee sasa katika ukurasa 30 ule ule lakini kifungu cha 72 juu ya ukusanyaji wa takwimu za viwanda. Niwapongeze wenzetu kwamba wanaendelea na

kukusanya takwimu za viwanda lakini vile vile takwimu za uzalishaji. Mhe. Mwenyekiti, wamesema kwamba takwimu za uzalishaji kwa mwaka 2016 inaendelea. Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, mimi nilitarajia kwamba takwimu hizi za uzalishaji, katika bajeti hii iwe zinasomeka katika hotuba hii. Inashangaza kuona kwamba takwimu hizi ndio inaendelea kukusanya. Kwa sababu bajeti hii tunapima uzalishaji katika viwanda upo vipi ili na wenzetu tuweze kuwapitishia bajeti, kuona kwamba wamefanya kazi nzuri lakini hatuoni vile vile ndani ya bajeti hii takwimu ya viwanda. Mhe. Mwenyekiti, tuna viwanda vingapi vya mambo gani, amejitahidi mama yangu kuweza kutoa takwimu, lakini takwimu hii haipo. Kwa Wajumbe tunashindwa kujua kwamba nchi yetu hii ina viwanda vingapi na viwanda vinavyoshughulikia na mambo gani. *(Makofi)*

Ningependa sana ni suala gumu lakini kama ataliweza atakapofanya majumuisho basi ni muhimu kuweza kujua takwimu. Lakini niwapongeze sana wenzetu kwa kuweza kufuatilia changamoto zinazokabili miradi hii ya viwanda. Niwapongeze sana kwa sababu viwanda vyetu vina changamoto nyingi. Ningependa wazidishe juhudi katika kuweza kuona wanafuatilia viwanda mbali mbali, kwa sababu hapa nimeona kiwanda kimoja tu cha Mahonda ndicho ambacho wamefanya ufuatiliaji wa kuweza kutazama changamoto.

Mhe. Mwenyekiti, Kiwanda cha Mahonda ni kiwanda cha wawekezaji kutoka nje, lakini tuna viwanda vya wawekezaji wa ndani wazalendo. Wenzetu nchi zinazoendelea wanaanza kuangalia changamoto za wazalendo kwa sababu wazalendo fedha yao inazunguka hapa hapa, lakini wageni pesa yao inakwenda nje. Mhe. Mwenyekiti, nimuombe sana Mhe. Waziri kuweza kufuatilia vile viwanda vya wazalendo na kuweza kuona changamoto mbali

mbali zinazowakabili, ili kuweza kuona kwamba tunapiga hatua za maendeleo katika viwanda. Lakini tukija hapo hapo kwenye Kiwanda cha Mahonda tunaambiwa kwamba hivi sasa tunatarajia pengine kutokana na changamoto zao tuwaongeze eneo la kulima, lakini vile vile tuwakabidhi nyumba. Naomba sana Serikali tuwe makini. Hawa watu tuwaongeze eneo lakini uzalishaji wao uko vipi.

Mhe. Mwenyekiti, lazima tuweze kupata takwimu, wanazalisha tani ngapi, tani ngani zinabaki ndani, tani ngapi zinauzwa nje. Lakini lengo la viwanda katika nchi yetu ni kuweza kuona kwamba sasa tunapunguza ule utegemezi wa kuagiza bidhaa kutoka nje. Wenzetu hii sukari ambayo inauzwa hapa bei yake ni kweli iko chini kuliko sukari ya nje kwa sababu ndio lengo tunaelekea huko, tunataka tuone kwamba tunazuia bidhaa kutoka nje na tunakuwa na bidhaa zetu za ndani. Sasa kama bei ya sukari ya Kiwanda cha Mahonda iko sawa na bei ya sukari kutoka nje, maana yake mimi sifikiri huo utakuwa wa kuwa na viwanda vya ndani. Kwa hivyo tutazame hiyo na kama haipo, lazima kuwe na tofauti kati ya sukari inayozalishwa hapa na sukari inayozalishwa nje ili kuona kwamba wananchi wetu wananufaika na bei nafuu ya zile bidhaa ambazo zinazalishwa ndani ya nchi.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, vile vile mimi nafikiri imefika wakati kuweza kum-*convince* huyu mwekezaji. Kama kweli tunataka kuzalisha sukari kwa wingi, mimi nafikiri kilimo hichi cha kutegemea mvua hakitotufikisha pahala. Kama wenzetu wametoka nje tuwashawishi basi watumie umwagiliaji ili kiwanda kiweze kuzalisha mwaka mzima. Hivi sasa kiwanda kinazalisha nafikiri awamu moja tu kwa mwaka kwa kutegemea kilimo cha mvua. Ninafikiri hiyo hatuwezi kupiga hatua. Mhe. Mwenyekiti, tuwashajihishe wenzetu kwamba watumie umwagiliaji ili tuweze

kuona uzalishaji wa miwa basi unakuwa wa mwaka mzima na kwa kiwango kikubwa. Lakini na hivi nyumba ambazo tunatarajia tuwape kutakuwa na mikataba gani. Ningependa sana Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri atakapokuja aweze kutwambia tunawapa kwa misingi gani na kwa mikataba gani.

Mhe. Mwenyekiti, niondoke sasa nielekee kifungu cha 74 kwenye ukurasa wa 31. Kwanza niipongeze Serikali na hususan Mhe. Waziri kwa kuweza kufikiria kufanya mapitio ya viwanda ambavyo vilikuwepo hapa nchini, ili kuona jinsi gani vitaweza kuendelezwa. Nikupongeze sana Mhe. Waziri kwa kuweza kufikiria hilo. Kwa sababu miaka ya sabini na thamanini nchi yetu ilikuwa na viwanda mbali mbali vidogo vidogo na kwa kweli vijana wetu wengi walipata ajira. Lakini la kusikitisha viwanda vile hivi sasa vingi kwa asilimia kubwa vimekufa. Sasa kufanya juhudi hiyo ya kuvipitia, nafikiri ni mwazo mzuri na nakuomba sana uendelee.

Mhe. Mwenyekiti, katika hotuba yake Mhe. Waziri alivitaja viwanda vya *COTEX* na Kiwanda cha Soda kufikiria pengine kuviimarisha au kuvianzisha upya kuweza kutoa motisha. Mimi ningependa kujua tu kwamba motisha huu tunaotarajia tuwape ni motisha wa aina gani. Tunawapa pesa za ruzuku au tunawapa motisha wa aina gani. Kabla hatujenda mbali huko Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri ningekuomba wewe mwenyewe ni mzoefu, mtu wa siku nyingi ni lazima tufanye utafiti wa kina. Kwanza tujiulize viwanda hivi vilikufa kwa sababu gani, tusije tukaendelea kuwapa motisha lakini kumbe hatukuweza kujua sababu hasa ya kufa kwa viwanda vyetu.

Mhe. Mwenyekiti, viwanda vyetu inawezekana vilikufa kwa mambo matatu. Kwanza ubadhirifu unawezekana uliuwa viwanda

vyetu. Sasa kama tunataka kufufua viwanda vyetu au kuanzisha vyengine, hili suala ni lazima tulijue. Watendaji wengi walikuwa siyo waadilifu, walikuwa ni wabadhirifu na hilo liliuwa viwanda. Wizi ulichangia kuuwa viwanda vyetu. Kwa mfano Kiwanda hichi cha *COTEX* Mhe. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri hichi kilikuwa kinatengeneza vitambaa kwa kumbukumbu yangu kwenye miaka ya thamanini, lakini amini Mungu ile siku ya Ijumaa wafanyakazi wa kiwanda kile basi hata kama asiyesali huwa anavaa kanzu. Kwa hivyo huwa anazongwa jora za vitambaa kwenye tumbo lake halafu anapiga kanzu yake anatoka nje, akifika nje huko anakwenda kukunjuliwa jora. Sasa katika mazingira haya ninafikiri hatuwezi kuendesha viwanda.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, ukienda Kiwanda cha Maziwa kila mfanyakazi alikuwa ana bili ya maziwa nje. Ukienda kiwanda cha Sigireti vile vile wafanyakazi huwa wanavaa madira, mapakti ya sigireti yanafichwa mpaka kwenye sehemu ambazo sizo. Mhe. Mwenyekiti, hatuwezi kuendeleza viwanda katika hali kama hiyo. Lakini sidhani kama tulikuwa na Sera ya Viwanda kwa wakati ule ambalo hili nalo ni tatizo. Sera ni kitu kimoja muhimu sana. Lakini kwa vile viwanda ambavyo vilikuwa vinaagiza malighafi kutoka nje, nalo ni tatizo. Kwa sababu kiwanda kama huna malighafi usitarajie kama kinaweza kupiga hatua. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri juhudi zako tunazipongeza lakini kuweza kufanya utafiti zaidi ili tukianza kuvifufua baadhi ya viwanda basi tuone kasoro ambazo zilijitokeza basi zimeondoka.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye maendeleo ya wajasiriamali. Niipongeze sana serikali kwa kuweza kuona umuhimu wa kuwaendeleza wajasiriamali. Uchimi wa nchi nyingi duniani ulitokana na wajasiriamali, kwa kuendelezwa kidogo kidogo na

hatimaye ndio ambao wamezaa kuwa na viwanda vidogo, viwanda vya kati na hatimaye wengine kuwa na viwanda vikubwa. Lakini kama nilivyotangulia kusema mwanzo katika progaramu hii asilimia iliyoingiziwa ya fedha ilikuwa asilimia 14. Sasa sidhani kama tuko *alert* katika kuona kwamba tunawasaidia wajasiriamali wetu kwa kuweza kuwaingizia programu hii asilimia 14 ya fedha.

Mhe. Mwenyekiti, ningemuomba sana Mhe. Waziri na Wizara ya Fedha kuweza kuona kwamba kama tunataka kuwandeleza wajisiriamali hawa, basi tukuze bajet ili wenzetu waweze kutekeleza programu hizi kama vile walivyotarajia, ili wajasiriamali wetu waweze kukua na na hatimaye kuwa na viwanda vidogo vidogo vya kati na hatimaye viwanda vikubwa.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie katika suala zima la mazao ya biashara. Nchi yetu hii ilikuwa ina mazao mengi ya biashara, lakini hivi sasa tumebaki na machache mno. Tuna haja ya kuweza kufufua na katika bajeti nimeona kwamba wenzetu wana mipango hiyo ya kuweza kufufua yale mazao ambayo pengine yalikuwa yamepungua kwa kipindi. Mhe. Mwenyekiti, tuna mazao ya biashara ambayo wenzetu ni lazima wakae na Wizara ya Kilimo, kuna mazao ya vanila, hiliki, pilipili manga, pilipili hoho ambazo zina soko sana duniani.

Mhe. Mwenyekiti, lakini leo ukiambiwa Zanzibar tuleteeni tani mbili za hiliki, tani mbili za pilipili manga kwa kweli hatuna. Lakini mahodari sana wa kutembeza wazungu kwamba sisi ndio walimaji wa viungo, lakini hatuna ukulima wa viungo wa kiasi kikubwa. Kwa hivyo hata kama tukiwa na viwanda, kama uzalishaji wetu ni mdogo tunajidanganya. Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa ni wakati wa kukaa Wizara ya Biashara ikae na Wizara ya

Kilimo tuweze kuona kwamba tunafufua mashamba ambayo yanalimwa kitaalamu. Wenzetu Bara hivi sasa wameshatushinda. Hivi sasa Mhe. Mwenyekiti, Morogoro kunazalishwa karafuu, Tanga hivi sasa wanajaribu kupanda karafuu, itafika wakati Zanzibar basi tutakuwa chini kuliko wenzetu wa mikoa mengine.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, nikwambie kwamba nilimuuliza swali moja Mhe. Waziri juu ya jinsi gani tunafanya ufuatiliaji wa miche tunayowapa wakulima kama miche ya mikarafuu, tunawapa wakulima bure. Nashukuru kwamba Mhe. Waziri aliweza kujibu kwamba bado hamjafanya *follow up* ya kuweza kuona miche hiyo inaendelea vipi. Ningependa hilo suala ulichukue, ushirikiane na wenzetu wa Kilimo msaidiane juu ya kufanya *follow up*.

Kuna fununu Mhe. Mwenyekiti, kwamba hata hii miche tunayoitoa bure hivi sasa nayo inasafirishwa kwenda Bara, inapelekwa Tanga na mengine inafika mpaka Morogoro, sisi tunaitoa bure huku wenzetu wapande, kumbe sasa inavuja inakwenda kwa wenzetu. Sasa sisi lengo letu ni kukuzisha zao la karafuu katika visiwa vyetu. Ndio pale tukaona kwamba kuna umuhimu wa kuweza kufanya *follow up* kwa miche ambayo tunaitoa kwa wakulima wetu, kwa sababu wengine sasa wao wanaifanya biashara na kuanza kuisafirisha kwenda Tanga mpaka mengine inafika Morogoro.

Mhe. Mwenyekiti, lakini vile vile kuna fununu kwamba karafuu ya Morogoro hivi sasa inaingia katika visiwa na inachanganywa na karafuu yetu. Hii ni hatari, tunaweza tukaharibu nembo yetu ya karafuu. Nikuombe sana suala hili ulifanyie utafiti kama lipo basi tuweze kujua jinsi gani ya kulikinga.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa nafasi uliyonipa na mimi nichukue fursa hii ya kusema kwamba hotuba hii nzuri ya Wizara hii ya Biashara, wizara ya msingi kabisa na naiunga mkono asilimia mia kwa mia.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Rashid Makame Shamsi kwa mchango wako. Sasa nimwite Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi akifuatiwa na Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini na Mhe. Abdalla Maulid Diwani ajitayarishe. Lakini kabla ya kumpa nafasi Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi wachangiaji hawa wanaofuata nitawapa dakika kumi kumi ili Waziri apate nafasi ya kuja kutoa majumuisho.

Kwa hivyo naanza na Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi dakika kumi atafuatiwa na Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini na Mhe. Abdalla Maulid Diwani ajitayarishe.

Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii na mimi niwe mmoja kati wa wachangiaji wa Wizara hii ya Biashara, Viwanda na Masoko.

Kwanza nampongeza sana Mhe. Waziri pamoja na watendaji wote kwa kazi kubwa wanayoifanya. Zanzibar hakuna njaa bidhaa zote zinapatikana, ukitaka mchele wa aina zote utaupata madukani, pongezi kubwa sana.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, pili nawaombea sana wananchi Ramashani Kareem wananchi wa Tanzania wote na dunia kwa jumla. Mwenyezi Mungu atujaalie kwenye Ramadhani hii mema tuyafuate na mabaya tuyawache. Tuendelee kudumisha

ushirikiano, mshikamano, umoja, undugu, urafiki, upendo na kutekeleza majukumu yetu ya kazi zetu kwa ujumla kwa salama na amani ili tupate maendeleo.

Kwanza kabisa naingia katika kitabu hichi ni kitabu kizuri sana, *data* zimeaoneshwa. Maana kuwasilisha *data*, kuna kuwasilisha kwa mdomo (*verbal*) unaeleza tu, unataja kitu fulani fulani kiasi fulani na kuna kuainisha kwa maandishi kwenye sentensi na kuna kuainisha kwa *tabulation* na hapa wamefanya *tabulation*.

Sasa mimi napendekeza tu mara nyengine ni vizuri wakaweka na ma-*graphs*, kwa sababu ma- *graphs* yanaweza ku-*cover* na kutoa maelezo ya kina kwa jambo fulani, haiwezekani kwamba kila kitu kiainishwe hapa lakini *graph* linaweza likatueleza mambo mengi kwa kipindi kirefu pengine cha miaka kumi au hata miaka mitano au sita. Napendekeza sana kuwe na ma-*graphs*, ma-*program*, *paychart* na mengine mengine.

Mhe. Mwenyekiti, nikiingia kwenye *table* ukurasa wa 8 kuna urari, kwa biashara za jumla urari uko *negative* lakini kwa biashara za hapa kwetu Tanzania kupeleka Bara kuna *minus* na nyengine tuna *plus*. Kidogo kinachonipa mashaka na wala si mashaka ninasema tu vile ninavyoona, hizi *datas* ni za Wizara ya Biashara ndio *source*. Sasa hapa naona wame-*quote source* takwimu, wakati takwimu wanapata kutoka Wizara ya Biashara kwa sababu hayo ni mambo ya biashara. Sina pingamizi kwamba wamepata kwenye takwimu pengine zinalingana ndio maana akaiweka lakini wangeainisha pia *source* kuwa ni Wizara ya Biashara wamekubaliana nayo.

Halafu ukitizama hizi takwimu kwenye urari kuna *different* ya *point one* imeachwa. Sasa sijui imeachwa wame-*correct the*

nearest au vipi, kwa sababu ukitizama juu ya *table* kumeandikwa *in millions.* Kwa hivyo ikiwa *point one over a millions* inakuwa ni *one hundred thousands* ambayo siyo idadi ndogo. Nashauri wasitizame *data* wakati mwengine pengine zinaweza kuwa zinataka *correction* au kama hazitaki *correction* basi lakini kama zinataka *correction,* basi ni bora zije kwa usahihi wa aina yake.

Mhe. Mwenyekiti, nazidi kukipongeza kitabu, kipo kizuri. Kwa hivyo sina wasi wasi na kabla sijamaliza dakika zangu naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja huku ninakokwenda nakwenda tu.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, naingia kwenye jumla ya Wizara ya Biashara kwa juu juu ukitizama ina jukumu la kusimamia mwenendo wa biashara, kudhibiti biashara, kuendeleza biashara hiyo na kuhakikisha uwepo wa bidhaa wakati wowote. Aidha inaelimisha, inatanabahisha na kutanabahisha hapa inawezekana imegundua kuna bidhaa fulani mbaya huko nje. Kwa hivyo inawatanabahisha wananchi kwamba bidhaa fulani isiletwe nchini au mkiiona msiinunue pia inakuwa ni kazi ya Wizara ya Biashara.

Mhe. Mwenyekiti, wimbi lilojitokeza kwenye biashara. Bidhaa zilizopo ama zipo zilizopitwa na wakati. Wakati mwengine wajanja wanazibadilisha pale kinabandikwa kikaratasi kwamba bado ipo *valued* wakati ambapo imesha *expire,* ni mbaya sana. Kuna maradhi mabaya sana kwenye *botulism,* maradhi wataalamu wa afya wanajua. Kuna maradhi yanayotokana na chakula cha makopo. Chakula cha makopo kilichokaa siku nyingi kina maradhi mabaya sana ambayo yanaweza kumuathiri mwanaadamu. Kwa hivyo liangaliwe sana suala la kuleta mabidhaa ambayo yamesha *expire.*

Mhe. Mwenyekiti, halafu kuna bidhaa hafifu, kuna mwenzangu mmoja hapa alichangia bidhaa ambayo unanunua kwenye chombo cha umeme sasa hivi ukitia pale kimewaka na kuungua na hizi pia ziangaliwe. Kwa sababu mwananchi maskini anayenunua ile sio kwa pesa kidogo anakwenda kuiunga hapo hapo inaungua, kidogo inamtia hasara sana inabidi akatafute nyengine na nyengine tena inakuwa ni matatizo.

Halafu tatizo jengine ni kupandisha bei holela. Bei hapa zimeainishwa mchele Shs.1200, lakini huko nje kuna mchele wa Shs.2200, Shs.3000 na kadhalika. Bei hatuwezi ku-*control* kwa sababu wenyewe wanaoleta ndiyo wanaojua gharama zao lakini pia zisimamiwe ili zisiwaumize sana wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine kuhusiana na bidhaa za madukani. Kuna maduka mengine kuna panya ukiingia ndani dukani mule panya wanakimbia na nini hii. Sasa panya kwa kawaida anatoboa anakula na anajisaidia pale pale juu ya lile gunia. Sasa kile alichojisaidia kinaingia kwenye chakula, panya wana maradhi mabaya sana ugonjwa wa tauni ambapo ukikupata huo mwili unakakamaa. Nashauri kwamba maduka yapitiwe na wapatiwe taaluma kwamba nini wafanye ili waepukane na mapanya, kwa sababu ndio duka lake hana pa kwenda pengine ndiyo hapo hapo, apewe msaada pale.

Mhe. Mwenyekiti, niingie kwenye viwanda. Uwepo wa viwanda utachangia sana mageuzi ya kiuchumi na hii imeanishwa hata kwenye kitabu. Aidha itasaidia sana kurasimisha sekta isiyo rasmi, kupunguza uagizaji bidhaa kutoka nje, kuongeza usafirishaji bidhaa kwenda nje, kuongeza thamani ya malighafi *(value exchange)* kuongeza ajira na kuongeza wigo wa malipo

kwa serikali, (kodi inakuwa inapatikana) na mapato huwa yanaongezeka.

Mhe. Mwenyekiti, kuna wawekezaji ambao watajitokeza kufanya hivi viwanda. Nashauri sana wawekezaji hawa wawe na hamasa, wawe hamasika (*right temperament)* ya kufanya biashara siyo wanakuja wangine na malengo mengine hapa, waje wawe na *right temperament* wafanye biashara na iendelee biashara. Na wazo lao la kufanya biashara pia litathminiwe linafaa. Halafu ufanyike utafiti wa kutosha juu ya hilo analotaka kulifanya mfanyabiashara yule. Mpango kazi wake siyo vibaya ukawepo na uwezo wao wa kifedha. Maana mwengine anaweza akaja kuwekeza akifika kati kati akisha, hana la kufanya kiwanda kipo lakini haendelei. Sasa hivi viwanda vilivyokuwepo hapa navyo pia viangaliwe kwa mfumo huo.

Mhe. Mwenyekiti, tuna ziara Pemba pale kuna Kiwanda cha Makonyo Chake Chake, nafikiri sijui Mhe. Suleiman Sarahani Said alizungumzia. Kiwanda kile kinatoa moshi mwingi sana, ukipita maeneo yale kiza cha moshi. Moshi una *carbon monoxide*, ile ukiivuta ndani huku kuna matatizo unaweza ukapata maradhi ya mapafu, umri unapungua ukipata maradhi haya ya mapafu. Naomba sana Kiwanda kile kiangaliwe wananchi pale wanapata matatizo hayo ya moshi, kuna moshi mbaya sana. Mimi nimeona mwenyewe sijahadithiwa, tumepita nikaona nikauliza huu moshi unatoka wapi, wakasema hii ndiyo kawaida kila siku moshi huu upo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Naomba umalizie.

Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi: Ahsante nitamaliza. La mwisho ninalotaka kulizungumzia mambo ya *SME*. Hapa najua kuna

mtaalamu mzuri sana kutoka Rwanda. Huyu aliendeleza Rwanda na kwa bahati nzuri aliwekwa Ofis ya Rais wa Rwanda na kule ukifanya mchezo Kagame anakutimua. Sasa huyu alikaa sijui miaka kumi au ngapi alikiendeleza na kule Rwanda ukienda kumeendelea kwa shughuli za *SME*.

Mhe Mwenyekiti, sasa nashauri Wizara yangu adhimu hii ya Biashara wajaribu kuziendeleza hizi *SME,* tuwapatiwe wale wenye biashara ndogo ndogo tuwakuweze ili wanaweza wakatokezea wengine ambao watakuwa na kuwa wafanya biashara wakubwa na maendeleo yatapatikana ndiyo maana mfanya biashara akiwa mkubwa atajiri mwenzake akimuajiri mwenzake ajira hiyo inaongezeka.

Kwa hivyo mimi muda wangu umekwisha Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa muda na narudia kumpongeza sana Mhe. Waziri na narudia kusema kwamba naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja sina tatizo nayo.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini na mchangiaji wetu wa mwisho kabla ya kumpisha Mhe. Waziri atakuwa Mhe. Abdalla Maulid Diwani na Mhe. Ahmada Abdulwakil Yahya ameomba dakika tatu tutampatia.

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, kupata wasaa wa kuchangia hotuba hii muhimu sana kwenye uchumi na maisha yetu. Hotuba ambayo imejaa falsafa ya Balozi Amina Salum Ali, mwenyewe ni mwana biashara,

kalelewa kwenye biashara na uchumi na hata akapata nafasi ya kutuwakilisha kama Balozi wa Afrika kule Marekani kwa vipindi viwili mfululizo. Kwa kweli nafasi ile hakupatiwa tu lakini aliitetea na akashindana na watu kuipata. Kwa hivyo kwa kweli tunampongeza sana kwa kazi yake nzuri, kitabu kidogo lakini kimejaa falsafa kubwa sana.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, naomba niende moja kwa moja kwenye kitabu cha bajeti. Mwaka uliopita wa fedha na hata mwaka huu Mhe. Waziri anaonesha ataendelea na programu zake nne:-

1. Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara
2. Programu ya Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali
3. Programu ya Ukuzaji na Uendelezaji Biashara
4. Programu ya Viwango na Tathmini ya Ubora

Lakini Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia kwa muono wangu zile programu ambazo hasa ile Programu ya Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali kwenye *sub programme* SR0202 "Maendeleo ya Ujasiriamali" imepata asilimia 14 tu ya pesa walizotiliwa mwaka jana. Haya njoo kwenye *sub programme* nyengine ya "Ukuzaji na Uendeshaji Biashara kwenye *sub programme* ya "Ushindani Halali wa Biashara na Kumlinda Mtumiaji", katika pesa walizokuwa *located* wamepata asilimia mbili tu. Njoo tena kwenye programu ya "Viwango na Udhibiti Bora", hapa ndio penye *ZBS* na mambo yote ya ukaguzi, kila kitu ndio *core* ya wizara hii. Mhe. Mwenyekiti, wamepata asilimia ishirini na tano tu. Sasa sijui mimi ningeiomba sana Serikali hasa haya mambo ya Udhibiti, Ujasiriamali, *Promotion* ya Masoko asilimia kumi na saba, ningeomba sana Mhe. Waziri akaongezwa pesa lakini na wao Wizara wenyewe wafanye *good reallocation* kwa sababu inaelekea kwenye Programu ya Utawala na Uendeshaji

imechukua asilimia sabini na nane ni *co-ordination* tu. Sasa zile kazi za *field* ambazo ndio zenye maisha zenye ndio *core* ya Wizara imepata asilimia ndogo sana. Hili namuomba sana Mhe. Waziri alizingatie pamoja na wizara kwa jumla.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sasa niende kwa suala la *ZBS* au ndio lile suala nililosema suala la viwango. Kwa kweli nimeona wengi wamelichangia lakini mimi hasa nakwenda moja moja nimekuja na chupa za maji mbili hapa makusudi. Mhe. Mwenyekiti, nataka nisome pale kwenye *composition* ya haya maji. Nimekuja na *Drop of Zanzibar*, nimekuja na *Zan Aqua,* lakini sitayasoma moja kwa moja, nishayasoma nataka kuonesha mfano tu. Humu kwa ujumla kuna *component* kama kumi na nne, wametoa *table* ndogo kwenye kila chupa mna *component* kumi na nne (14) naomba nizisome:-

1. *TDS*
2. *Sodium*
3. *Magnesium*
4. *Chlorite*
5. *Surphate*
6. *Chloride*
7. *Potassium*
8. *pH*
9. *Nitrite*
10. *Nitrate*
11. *Bicarbonate*
12. *Iron*
13. *Calcium*
14. *Haidinates*

Sasa ukizoma hizi na *brand* zetu za maji ambazo zinatumika sana, nimekwenda haraka haraka tu nimepata kama saba.

1. Super Pure
2. Kilimanjaro kutoka Tanzania Bara
3. Zan Aqua
4. Zanzibar Cool
5. Uhai kutoka Tanzania Bara
6. Drop of Zanzibar
7. Blue kutoka Tanzania Bara

Sasa hizi *components* ukiziangalia Mhe. Mwenyekiti, zinatofautiana. Hakuna *standard* ambayo labda iliyokubalika na hii inaonesha wazi. Kuna *brand* nyengine za haya maji ukiyanywa utaona uchungu, hayako safi hasa. Sasa mimi nilikuwa namuomba Mhe. Waziri hii *ZBS* tuamini. Tuipe meno ifanye kazi na cha kusikitisha zaidi hizi kampuni ziko Zanzibar.

Zan Aqua iko Zanzibar na *Drop of Zanzibar* iko Zanzibar lakini kuna *label* ya *TBS, why not label* ya *ZBS,* eeh! ifanye kazi kama haina meno tuipe meno. Lakini sasa viwanda vipo Zanzibar, maji tunakunywa Zanzibar, lakini hamna *label.* Sasa hatuiamini *ZBS.(Makofi).*

Sasa naiomba sana Mhe. Mwenyekiti, tuipe uzito unaostahiki, kama hawana vifaa waagiziwe vifaa, lakini haipendezi kwamba maji ya Zanzibar, viwanda vyetu tunakwenda kuipa *label* ya *TBS aah!* kwa kweli si jambo la busara sana. Na linawezekana kwa sababu maziwa ya Bwana Bakhresa yeye anayatengeneza Zanzibar, ana *label* sijui ya *ZBS* au *TBS,* lakini ana soko la Tanzania Bara na *The whole of Eastern Central Africa.* Lakini maji ya *drop* sijui kama yanavuka bahari hayo. Hayo maji ya *Zan Aqua* sijui kama yanavuka bahari lakini za *reverse* maji ya

Kilimanjaro, maji ya Uhai yanauzwa Zanzibar, kwa nini maji yetu yasiruhusiwe kuuzwa kule.(*Makofi*).

Sasa hili Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri tunapozungumza matatizo na viwanda vyetu vidogo vidogo kufa Zanzibar kwa matatizo haya, kuna vita baridi kwa *products* za Zanzibar kuuzwa Tanzania Bara. Ndio maana ule urari wa biashara siku zote unakuwa mkubwa *against* Zanzibar. Namuonmba sana Mhe. Waziri hili alizingatie na tutafute *mechanism* au utaratibu kuutafutia ufumbuzi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niende haraka haraka mambo leo ni mengi lakini nitazungumza kwa uchache sana. Jengine nililolitayarisha kwenye huduma za ukaguzi katika ukurasa wa 40 jadweli namba 9 "huduma ya ukaguzi", kuna eneo la ukaguzi, mezani, *weight breeze, pumps* za kuuzia mafuta, matangi ya kuuzia mafuta na *figures* pale na kazi waliyoifanya. Lakini sasa baada ya ukaguzi ule wamegundua nini. Tungemuomba sana Mhe. Waziri atuambie baada ya ukaguzi ule *what are their fundings,* wamegundua nini na wamerekebisha nini, itasaidia sana jamii na yapo mambo matatizo yapo kabisa. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, lakini hapo hapo ukiangaalia kwenye ukurasa wa 41 jadweli namba 10 "huduma za ukaguzi", maduka elfu nne na ushee, maghala 176, *bakeries* 45. Sasa kwenye *bakeries* Mhe. Mwenyekiti, Mzanzibari baada ya wali, chakula chake chengine ni mkate na leo Alhamdulillah wamekagua mabekari 45. Mimi nataka kummuliza Mhe. Waziri *bakeries* zetu ili kuweka mizani, ile tonge ya mkate ikapimwa pale bado upo. Naamini haupo kwa sababu gani, leo mkate kila mmoja anauza na *size* yake.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, lakini nakumbuka zamani ukienda *bakery* pale unakuta mizani pale tonge inapimwa na kuna mkate mdogo, wakati wetu tulikuwa tunanua pesa nne, halafu ukaja mkate mkubwa pesa nane. Sasa hivi tusiweke bei lakini ile *standard, ZBS* watuwekee *standard* mkate uwe na *standard* hii. Lakini leo naona kidogo halipo. Sasa ningemuomba sana Mhe. Waziri ndiyo pale niliposema hii *section* hii ya Ukaguzi na Uandiko wa Vifaa mizani au programu ndogo ile ya Ushindani wa Biashara ni muhimu sana na ingeongezewa pesa.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, naona unaniangalia nimalizie kwa suala la *ZSTC.* Kwa kweli tunashukuru sana *ZTSC* ni Shirika letu, wazungu wanasema lime-*live to our expectation* au limefanya kwa kweli kama kazi tuliyowapa na kwa nini basi, wenzangu wengi wamezunguza kwenda leo kumlipa mkulima asilimia 80 ya gharama za karafuu ni jambo la mfano sana.

Namalizia Mhe. Mwenyekiti, sasa kwenye ukurasa wa 58 wamesema watapanda miche mipya ya mimea ya milangilangi eka 5, mchaichai eka 10 na mrehani eka 5. Nauliza watapanda wapi. Lakini la pili ningeomba sana mbali ya kupanda wao lakini wawashirikishe wakulima wadogo wadogo, haya mashamba ya *spices* yalikuwepo, milangilangi mfano huko Kitogani, kwetu Bweleo, kule Fumba yanaota. Mhe. Mwenyekiti, wao wa-*concentrate* kufanya *co-ordination,* wa-*supervise* washirikiane na Wizara ya Kilimo kuwapa pesa wale waka-*produce* wao *rather than* wao kuzalisha.

Mhe. Mwenyekiti, ningeshauri sana *pilot project* zimefanywa sana kwa mambo haya, waende kwenye *literature* yapo na kwa kweli yapo *straight forward* si kufanya utafiti ni *production*.

Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja na kwa kweli Mhe. Waziri naomba sote tumpeni mapesa anayotaka.

Mhe. Mwenyekiti, ahsante *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Abdalla Maulid Diwani na Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil kwa dakika tatu na nitampa Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango dakika tano ili na yeye aweze kujibu hoja zile zilotolewa na Wajumbe.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante Mwenyekiti kwa kunipa fursa na mimi kuwa mchangiaji katika Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko.

Awali ya yote naungana na wale wote waliopongeza, waliotoa shukrani na mimi nikiwa miongoni mwao, lakini bila ya kupoteza muda niende moja kwa moja katika mchangio wangu.

Kwanza niipongeze Wizara ya Biashara kwa walivyotuandikia kitabu chao hiki kutuambia kwamba imeonesha biashara namna gani ya uingizaji wa bidhaa kwa Zanzibar imezidi, kwa kweli mahitaji yameonekana yapo ya kutosha, isipokuwa nguvu tuu za kuongeza biashara pengine kutokana na mitaji midogo ya wafanya biashara wetu lakini imekua kidogo, kutoka bilioni 19,000,000,000 mpaka bilioni 263,000,000,0000 hongera sana katika hilo.(*Makofi*).

Lakini nikienda mbele katika ukurasa wangu wa 8 ibara ya 18 napata wasi wasi na namna ya biashara jinsi gani inavyoifanya na naomba kunukuu.

"Mhe. Spika, kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2016 Zanzibar imepeleka

Tanzania Bara bidhaa yenye thamani ya TZ.Shs. 84,760,000.9

ukilinganisha na bidhaa zenye thamani ya TZ.Shs. 401,219,000.4".

Mhe. Mwenyekiti, napata wasi wasi kwamba tunahimizana tufanye biashara lakini sasa hivi hizo biashara ambazo zinatoka Zanzibar kwenda Bara zimepungua sijui mara ngapi, kwa hivyo watu wa hesabu wanajua. Kutoka milioni 401 mpaka milioni 84 zimezungumzwa changamoto hapa lakini hadi changamoto moja ilikuwa ni suala la *VAT*. *VAT independence*, sisi tuna *VAT* yetu Zanzibar na Bara wana *VAT* yao, kulikoni kwamba ipelekee kushuka kiasi hiki ya mapato kwa kweli yanatisha yameshuka sana na katika maelezo yako umekiri kusema tu kwamba upungufu huo umepelekea bidhaa za magari, vifaa vyenginevyo eletroniki kutokana na mabadiliko ya usimamizi wa bidhaa za kodi zikiwemo *VAT*.

Mhe. Mwenyekiti, kodi *import duty* tunajua ni ya muungano lakini *VAT* Zanzibar tuna sheria yetu ya *VAT* na Bara wana sheria ya kwao ya *VAT*. Sasa sioni kama sababu kubwa sana hii *VAT* kwenda kupelekea ushukaji wa namna hii. Kwa kweli ushukaji unatisha, hatujui 2017/2018 itakuwaje. Ninafikiri inawezekana tukaja tukakuta kuna milioni 10,000,000 au 20,000,000 kwa mwenendo huu tuliokuwa nao. Naikubali sana Mhe. Waziri ni mtaalamu, unajua lakini kwa hapa kuna sababu ya kukaa chini ukajiuliza kulikoni wapi tulipochelea au matatizo ya mabadiliko haya ya *policy* ya biashara, tumekosea wapi kuona kwamba Zanzibar hatufaidiki sana.

Mhe. Mwenyekiti, kiufupi kwamba Zanzibar ni *transit trading* kwa sababu ni kisiwa, hapa bidhaa zipite zifungue mlango kwa upande wa pili kupeleka ili watu wetu waweze kuwa na mzunguko wa pesa uwepo sana. Lakini kutokana na mwenendo huu tayari ile biashara Zanzibar inakufa hata maisha magumu kwa watu wetu yanahitajika hapa kwa sababu biashara haziingia Zanzibar na kutoka kupelekwa upande wa pili wa nchi hii.

Kutokana na soko letu sisi asilimia kubwa ya soko la wafanya biashara ya Zanzibar liko upande wa pili wa Muungano na ndiko Tanzania Bara, ni kweli kuna changamoto lakini bahati nzuri kila siku mnatwambia mnakaa kwenye vikao vya watendaji wa shughuli za kero ya Muungano, lakini kwa hili la biashara bado nitaomba sana Mhe. Waziri lazima tupate mustakabali unaostahiki kwa hili tuweze kujua wapi tunakoendelea, *unless otherwise* keshokutwa bajeti ya 2018/2019 itakujakuwa na milioni 10,000,000 hapa kwa mwenendo huu.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea mbele katika kitabu chako hiki hiki ulisema kwamba ukurasa wa 30, "Mhe. Spika, Rasimu ya awali Sera ya Maendeleo ya Viwanda imeandaliwa ambapo Wizara inaendelea kwa hatua za ukusanyaji wa maoni...". Hivi niulize zamani kulikuwa hakuna sera ya viwanda ndio maana vikapelekea kufa, kwa sababu sasa hivi unasema ndio kwanza kuna rasimu unasikiliza wadau namna gani viwanda vyetu tufanye lakini sasa sio suala kubwa sana mpaka utafute wadau ambao muda wote bado wadau hawajakamilisha hili zoezi tukajua linakuja na sheria gani ya viwanda kuangalia Zanzibar na sisi katika uchumi wa viwanda. Wenzetu sasa hivi wanapiga zogo kila kukicha wanakwenda katika uchumi wa viwanda.

Lakini Zanzibar ndio kwanza tunatoa Sera ya Maendeleo ya Viwanda iandaliwe, wakati hapo mwanzo tulikuwa na viwanda sasa hhivi vimekufa na hata juzi tu miaka mitatu au minne nyuma Kiwanda cha soda *total* kimekufa. Tujiulize kwa nini kimekufa. Kimekutwa na matatizo yale yale yanayozunguzwa hapa ya '*non terrify barriers'* ambapo kwenye kodi hamna lakini kuna watu pengine *TBS* tu, huku kuna *ZBS* huku kuna *TBS* inawekwa mikwala kwamba chombo hiki kisiingie, lakini mzigo huu umetoka Zanzibar sijui una kitu gani. Sasa iweje wenzetu wa upande wa pili wanafaidika zaidi na soko la Zanzibar kuliko sisi kwa upande huu kufaidika kule Bara.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri hapo kidogo nataka uje unifahamishe vizuri kwa sababu mimi ni shuhuda kwenye upande wa biashara, nipo katika sekta nzima ya viwanda vya maji, hakuna hata kampuni moja ya Zanzibar yenye ubavu kuhamisha maji kutoa Zanzibar kupeleka Tanzania Bara. Kwa nini iweje wenzetu kule Bara ukiangalia maji ya Kilimanjaro hapa yapo, ukiangalia Uhai hapa ipo, hii Blue, maji *varieties* yapo Zanzibar na maji yale yale sisi tunao uwezo kule Wazanzibari haridhiki kama hajapata *Drop of Zanzibar* akanywa Tanzania Bara au haridhiki kama hajapata *Zanzibar Cool,* vyereje tunashindwa kuna tatizo gani.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri nitakuomba sana katika hicho utuambie nini tatizo kwamba Zanzibar tushindwe kutoa maji yetu, tuna viwanda visivyopungua sita sisi hapa au saba na viwanda baada muda si mkubwa vitakufa, kwa sababu soko dogo, uzalishaji mkubwa. Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia gharama za umeme watu watashindwa kuwalipa wafanyakazi. Nitakuomba sana Mhe. Waziri katika hicho uje utusaidie ili liwe wazi Wazanzibari walioweka viwanda vyao na wao wapate nguvu ya

kufanya biashara kwa upande wa pili wa Zanzibar haiwezekani upande mmoja ufaidike zaidi sisi hatuwezi kufaidika.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Abdalla Maulid Diwani ahsante kwa mchango wako.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Hee**!** Mhe. Mwenyekiti, nina moja samahani kidogo moja kwa haraka haraka mambo hayajamaliza kuhusu suala zima la *ZBC* sio *Zanzibar Broadcasting*, *Zanzibar Business Society* ni Baraza la Biashara.

Mhe. Mwenyekiti, hili nakumbuka Baraza la mwisho limefanyika Baraza la nane mwaka 2014. Sasa hivi karibuni miaka mitatu halifanyika tatizo nini na kila mwaka kutokana na Sheria zao Baraza la Biashara linatakiwa lifanyike. Kile ni chombo cha wafanya biashara wetu hapa kwenda kutoa changamoto zao, kero zao na kutafutiwa ufumbuzi kuona namna gani biashara Zanzibar inaendelea. Mhe. Waziri nitakuomba sana suala hili kuja kunielezea.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, ijapokuwa kuwa jambo mambo mengi yapo nashukuru vile vile naunga mkono hoja.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Abdalla Maulid Diwani kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil na mwisho nimpishe Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango.

Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hiyo ya upendeleo ya dakika tatu.

Mimi Mhe. Mwenyekiti, kwanza nampongeza sana Mhe. Waziri kwa jinsi alivyoiandaa bajeti hii ambayo ina utaalamu mkubwa. Bajeti hii si kushangaa kwa sababu mama ninamfahamu ni mchumi na ni mwanadiplomasia na aliyeishi nchi mbali mbali ikiwemo Marekani.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, katika mchango wangu kwanza napongeza juhudi zilizofanyika hadi kupatikana *branding* karafuu yetu. Katika mchango wangu ambao umebidi uniguse kwamba Zanzibar ni sehemu ya Afrika na kuna soko huria linaitwa *AGOA*, soko ambalo dunia nzima nchi ya Afrika imeipa upendeleo maalum wa kuuza bidhaa zinafika 6000 aina mbali mbali. Soko hili liko huria halina ushuru na mpaka dakika ya leo Marekani imeruhusu bidhaa za aina mbali mbali zipelekwe bila ya ushuru wa aina yoyote.

Mhe. Mwenyekiti, sijui Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa upande wetu kama ni Afrika, Zanzibar tumefanya juhudi gani ya kusafirisha bidhaa zile ambazo hazina ushuru ilimradi tu ziwe na nembo ya Zanzibar. Kama hatujalitumia soko hilo, hilo liko wazi na Mhe. Waziri atusaidie kidogo tu kahamasisha vipi wafanyabiashara ili kutumia soko hilo la *AGOA*.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, mimi kwa jumla naunga mkono bajeti hii asilimia mia moja. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango na baadae nitamwita Mhe. Waziri kwa ajili ya majumuisho ya hoja zilizotolewa.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kukushukuru wewe kwa kunipa fursa hii na mimi kupata nafasi ya kuchangia ijapokuwa kwa dakika chache hotuba ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko. (*Makofi*).

Baada ya kukushukuru Mheshimiwa nimshukuru sana Mhe. Rais Dkt. Ali Mohamed Shein kwa miongozo yake na hasa kwa msukumo wake katika suala zima la kuendeleza viwanda katika nchi hii. Nimshukuru sana Mhe. Waziri wa wizara hii, Katibu Mkuu na watendaji wote kwa kazi nzuri walioifanya katika mwaka huu tunaomalizia 2017. Lakini vile vile kuandaa hotuba nzuri sana yenye mwelekeo mzuri wa kuimarisha viwanda na biashara katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, nchi yetu inafanya mengi sana kwa ajili ya kuweka mazingira bora yatakayoweza kukuza fursa za uwekezaji, fursa za biashara lakini vile vile kukuza uchumi katika nchi hii. Suala zima kama tunavyoliona la miundombinu ni eneo moja kubwa sana Mhe. Mwenyekiti, ambalo serikali yetu inaliweka kwa dhamira ya makusudi kabisa ya kukuza biashara lakini vile vile kuchangia katika ukuaji wa uchumi. Jitihada kubwa tunaziona katika ujenzi wa viwanja vyetu vya ndege kama *gateway,* lakini vile vile mipango ya ujenzi wa bandari za kisasa zitakazosaidia kukuza fursa za biashara, vile vile uwekezaji mkubwa unaofanywa na serikali yetu katika miundombinu mengine ikiwemo umeme, maji na pia katika uwekaji wa sera sahihi zitakazosaidia kukuza uwekezaji biashara katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na hayo serikali kupitia wizara hii inafanya juhudi kubwa sana ya kuwaandaa vijana wetu kuwa wajasiriamali makini na kubadilisha *culture* yao kwenda kwenye *culture* ya ujasiriamali ambayo ni chachu ya ukuaji wa viwanda

katika nchi hii. Juhudi kubwa zinafanywa na nimpongeze sana Mhe. Waziri amekuwa mstari wa mbele sana katika kufuatilia suala la upatikanaji wa masoko kwa bidhaa zinazozalishwa katika nchi yetu. Yeye amekuwa mfuatiliaji mkubwa sana wa kuhakikisha pia bidhaa hasa zinazozalishwa na wajasiriamali wadogo wadogo zinapata soko ndani na nje ya nchi. Taaluma mbali mbali kwa kushirikiana na wizara inayohusika na masuala ya kazi zimekuwa zikitolewa na kwa maana ya mafunzo kwa wajasiriamali wetu kuweza kuzalisha bidhaa zenye viwango, lakini vile vile kuwa na vifungashio bora vitakavyovutia bidhaa hizo.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na hayo yote lakini serikali yetu imeweka mashirikiano makubwa sana na sekta binafsi, na katika kukuza mashirikiano hayo kuna Baraza la Biashara ambalo limeundwa na linaendeshwa chini ya Mwenyekiti wa Mhe. Rais Dkt. Ali Mohamed Shein. Lakini Sera ya *PPP* imeandaliwa, vile vile kunakuwepo na mashirikiano na kusaidia kukua kwa *Chamber of Commerce*. Haya yote ni jitihada za kukuza biashara katika nchi yetu, vile vile kukuza uwekezaji katika nchi yetu. Yapo mambo katika mjadala yalizungumzwa na moja lilihusiana sana na masuala ya uwekezaji.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niseme kidogo tu kwenye eneo hili kwamba Zanzibar tuna utaratibu mzuri sana wa kukuza uwekezaji katika nchi yetu. Na wawekezaji kwa kweli wanatakiwa kwanza mwekezaji yeyote yule aoneshe nia ya kutaka kuwekeza katika nchi yetu, ajaze fomu ya *intention* ya kutaka kuwekeza katika nchi yetu na fomu hiyo inapatikana kwenye mtandao au kwenye *website* ya *ZIPA*. Mara baada ya kujaza ndani ya wiki moja anapata majibu yake. (*Makofi*).

Lakini baada ya kupata majibu anatakiwa sasa apate fomu ajaze fomu, ambapo fomu hiyo ndio inayolipiwa ile fomu ya *intention* hatakiwi kulipa kitu chochote, lakini hii anatakiwa kulipa dola za Kimarekani mia mbili…

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri samahani kidogo naomba nimpishe Naibu Spika aendelee.

(Hapa Mhe. Naibu Spika alikalia kiti)

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa tuendelee.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema mwekezaji mwanzo kabisa anahitajika kujaza fomu ya *intention* ya kutaka kuwekeza na ndani ya wiki moja anapata majibu yake na baadae anajaza fomu ya *application* ambayo anailipia kwa dola za Kimarekani 200, na anatakiwa baada ya kujaza fomu hiyo awasilishe pamoja na nyaraka nyengine zikiwemo na *business plan copy* 10, ambazo *copy* 10 hizi zinawasilishwa katika taasisi mbali mbali zinazohusika, na taasisi hizo zinakutana ndani ya wiki mbili kujadili kuhusiana na ombi lile la uwekezaji.

Ndani ya wiki tatu baada ya kikao kile kukaa mwekezaji huyu anatakiwa apewe *certificate* ya uwekezaji, kwa maana ya *Entering Investment Certificate*. Hapo hutakiwa lakini kwa msaada wa *ZIPA* kuweza kukamilisha taratibu nyengine ikiwemo ya kupatikana kwa ardhi, vibali vyengine kama mazingira na masuala mengine yanayohitajika.

Kwa hivyo utaratibu uko wazi, utaratibu rahisi sana kwa mwekezaji yeyote anayetaka kuwekeza katika nchi yetu kuufuata

utaratibu huu na muda uliopo ni muda mfupi. Lakini pamoja na hayo hivi sasa serikali imo katika mazingatio maalum ya kuhakikisha kwamba tunakuwa na *One Stop Centre* na hilo limo katika mjadala na hivi karibuni litapatiwa ufumbuzi wake, ili taasisi zote zinazohusika katika kukuza fursa ya uwekezaji ziwe mahala pamoja, ziwe kwenye *umbrella* moja ili kurahisisha wawekezaji wetu na kutopata usumbufu kama unavyozungumzwa na Waheshimiwa Wajumbe.

Mhe. Naibu Spika, lakini pamoja na hayo yote serikali kupitia Sheria ya *ZIPA*, Sheria Nam.11 ya 2004 imeweka utaratibu mzuri sana wa vivutio kwa wawekezaji hao na umeelezwa vizuri, vivutio vya kodi na visivyo vya kodi. Utaratibu upo wazi na hivi sasa serikali iko katika dhamira ya kuweka vivutio zaidi kwa miradi ambayo itaitwa miradi ya kimkakati (*Strategic Investment).* Kwa hivyo hayo yote yamewekwa na yanaandaliwa kwa ajili ya kuvutia uwekezaji katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, katika uchangiaji lipo moja lilizungumzwa suala la kodi la kwamba tumekuwa mara zote tunapandisha kodi na hakuna mwaka hata mmoja ambao tumeshusha kodi. Niseme kwa dhamira ile ile ya kukuza uwekezaji, kukuza biashara katika nchi yetu lakini pia kuwapa unafuu wananchi wetu wanaotumia huduma na bidhaa zinazoagizwa katika nchi yetu, serikali kwa miaka miwili hivi sasa haijaongeza kodi ya aina yoyote ile. (*Makofi*).

Katika bajeti ya mwaka 2016/2017 hatukuongeza kodi, bajeti ya mwaka huu pia tumeshatoa tamko kwamba hakutaongezwa kodi na kinachofanyika sasa hivi Mhe. Naibu Spika, ni kwamba kutokana na vyanzo tulivyonavyo kuongeza udhibiti wa ukusanyaji wa mapato hayo lakini vile vile matumizi yake yaende

katika yale maeneo ambayo yana ulazima wa matumizi. Kwa hivyo si suala la kuongeza kodi na yote yanafanywa kutoa unafuu kwa wawekezaji lakini vile vile kutoa fursa ya kuwavutia zaidi wawekezaji kutoka nje na wa ndani lakini pia kuwasaidia wananchi wetu wasipate ugumu na makali ya maisha.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, suala la *TRA* nalo lilizungumzwa na niseme Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko ni wizara muhimu sana, kwa sababu zaidi ya asilimia 60 ya mapato yanayokusanywa na *TRA* yanatokana na biashara za kimataifa. Kwa hivyo mahusiano ya mapato na mahusiano ya Wizara hii ya Biashara ni makubwa sana, kupitia *TRA* pekee zaidi ya asilimia 60 ya mapato yake basi yanatokana na biashara za kimataifa.

Lakini kitu gani kinachotokea kuwepo na utofauti kwa bidhaa zinazotoka hapa Zanzibar, zinazosafirishwa kupelekwa upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hii tumewahi kuieleza mara nyingi lakini naomba niirudie inatokana na kuwa na mifumo miwili tofauti, chombo kimoja, chombo cha Muungano lakini tuna mifumo miwili tofauti. Hapa Zanzibar mpaka sasa tunatumia mfumo ule ule wa *scudder plus plus***,** wakati wenzetu wa Tanzania Bara wanatumia sasa mfumo wa *Tanzania Custom Information System (TACIS*). Sasa suala ni ku-*harmonize* na sisi kwa upande wa Zanzibar kuna mambo ambayo tulisema ni lazima kwanza tukutane na tukubaliane. Kwa sababu huu mfumo wa *TACIS* unataka kuwepo na *centralization* ya *system*, tuwe na *centralize system* katika kituo kimoja kule Dar es Salaam na kwa upande wa Tanzania Bara hicho ndivyo kilivyo kwa vituo vyote isipokuwa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, sisi tunasema kwamba pamoja na hayo yote ni lazima tuwe na mazingatio maalum kwa upande wetu. Kwa hivyo

yako mambo Mhe. Naibu Spika ambayo hivi sasa tunaendelea kuyazungumza kupitia vikao vya Mawaziri wa SMT na SMZ vinavyoongozwa na Mhe. Makamu wa Rais na kuhudhuriwa na Mhe. Waziri Mkuu kwa upande wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa upande wa Zanzibar. Suala hili bado tunaendelea na majadiliano nalo na ningewaomba sana Waheshimiwa Wajumbe wakasubiri hadi pale tutakapokamilisha masuala haya.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba nitamke kwamba naiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika: Nakushukuru sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango. Waheshimiwa Wajumbe sasa hivi tunampisha Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko kwa ajili ya kuja kujibu hoja za Waheshimiwa Wajumbe. Mhe. Waziri karibu sana.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Naibu Spika, mimi naomba nichukue nafasi hii kukushukuru wewe mwenyewe kwa kunipa nafasi ya kuja kufanya majumuisho kwa kujibu hoja za Waheshimiwa Wajumbe.

Mhe. Naibu Spika, bajeti yangu imechangiwa na Wajumbe waliochangia moja kwa moja wanaofika 14 na kuna Wajumbe wengine wamechangia kwa maandishi. Kwa hivyo naomba niwataje. Kwanza kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Fedha, Biashara na Kilimo.

1. Mhe. Suleiman Sarahan Said
2. Ali Suleiman Ali

3. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy
4. Mhe. Omar Seif Abeid
5. Mhe. Hidaya Ali Makame
6. Mhe. Panya Ali Abdalla
7. Mhe. Suleiman Makame Ali
8. Mhe. Rashid Makame Shamsi
9. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi
10. Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini
11. Mhe. Abdalla Maulid Diwani
12. Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil
13. Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango.

Waliochangia kwa maandishi ni.

1. Mhe. Naibu Waziri wa Afya
2. Mhe. Khadija Omar Kibano
3. Mhe. Juma Ali Khatib (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum)
4. Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto
5. Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira
6. Mhe. Waziri wa Habari, Utalii na Michezo
7. Mhe. Naibu Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto
8. Mhe. Miraji Khamis Mussa

Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba…

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri kwanza mimi mwenyewe nimechangia kwa maandishi Mheshimiwa. Halafu kuna wachangiaji wengine ambao wamechangia hujawataja, ninafikiria ni Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf sijamsikia, Mhe. Omar Seif

Abeid, Mhe. Suleiman Sarahan Said, Mhe. Suleiman Makame Ali na Mhe. Ali Suleiman Ali nafikiri hawa walichangia. Mheshimiwa naomba waingie kwenye *hansard*, endelea.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Sawa Mhe. Naibu Spika, nimewataja waliochangia kwa mdomo halafu wamechangia kwa maandishi, mimi wengine michango yao sijaipata mpaka sasa hivi, lakini kama imekuja kwa maandishi basi nawataja wamechangia ya ziada kwa maandishi, lakini bahati mbaya sijapata…

Mhe. Naibu Spika: Hawa wamechangia kwa maneno, hao niliowataja.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Sawa nashukuru Mhe. Naibu Spika, wataingia kwenye *hansard*, ingawa mimi mbele yangu hapa michango yao sina, lakini kwa sababu ndio wakati wenyewe papo kwa papo lakini michango haijafika.

Mhe. Naibu Spika, naomba niseme tu kwamba nawashukuru wote walioleta kwa maandishi, waliochangia kwa kusema nawashukuru sana, wote katika michango yenu mumeonesha imani mliyokuwa nayo na wizara yetu na watendaji wetu na mimi mwenyewe binafsi na nyote mumeyakubali maudhui ambayo tumeyazungumza katika bajeti hii.

Nawashukuru sana mmenipa moyo mkubwa sana, kwa heshima na taadhima nawashukuru na nakuahidini tutajitahidi kufanya kazi kama nilivyoahidi kipindi cha mwaka jana mimi na Katibu wangu Mkuu ni wapya, lakini tutajitahidi kufanya kazi kwa mujibu wa maslahi ya nchi yetu.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, michango yote niseme kwamba imejenga hakuna mchango hata mmoja uliokuwa umekuja haukujenga zaidi, dhana nzima ya kuendesha biashara, kuendesha viwanda kusimamia masuala mazima ya mwenendo wa biashara, kusimamia masuala mazima ya viwanda, vile vile kushauri jinsi ya kulinda maslahi ya wananchi, kulinda afya za wananchi wa Zanzibar, yote haya kwa kweli michango yote mimi nashukuru ilikuwa mizuri na imetupa maelekezo na muelekeo mzuri.

Mhe. Naibu Spika, vile vile naomba niwashukuru wale Mawaziri waliochangia michango yao pia imejibu hoja za msingi ambazo zimeelezwa na baadhi ya Wajumbe kwa sababu baadhi ya maelezo yaliyoulizwa hapa yameingiliana na Wizara ambayo wanazisimamia. Kwa hivyo mimi sitojibu tena masuala haya kwa sababu wamekwishajibiwa kwa ufasaha zaidi na kwa umakini zaidi, kwa hivyo watasaidia katika kuleta taswira nzuri ya bajeti inayokuja ya mwaka 2017/2018.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nitajibu hoja kwa jumla halafu nitajazia zile ambazo zilizokuwa zinahitaji kupata maelekezo. Naomba nichukue nafasi hii kujibu kwanza hoja ya taarifa iliyosomwa ya Kamati yetu ya Fedha, Biashara na Kilimo.

Mhe. Naibu Spika, niwashukuru sana Wajumbe wa Kamati hii ni wenzangu, tunafanya kazi vizuri, wananishauri vizuri na mimi tunaelekezana vizuri. Kubwa ambalo walikuwa wanataka kujua ni kuhusu tatizo la kutopatiwa *certificate* ya ubora wajasiriamali hawa wa Kiwanda hiki cha Mkipimiliki. Mkipimiliki mimi mwenyewe nimeshatembelea kiwanda hiki, nimetembelea Ofisi zao zilioko karibu na Micheweni, nimetembelea na Ofisi zao vile vile zilizoko mjini pale Pemba, nafikiri Wete pale.

Mhe. Naibu Spika, tatizo liliopo kwamba hiki kiwanda au wajasiriamali hawa hawakuweza kufikia kiwango cha ubora. Hapa kuna vitu viwili tofauti Mhe. Naibu Spika, unaweza wewe kuzalisha bidhaa lakini zile bidhaa zikawa hazijafikia kiwango cha ubora, lakini bado zikawa zinatumika mjini. Kwa mfano kama hizi sabuni, sabuni nyingi mnazoziona sasa hivi hazijaweza kupewa kiwango cha ubora kwa sababu bado mazingira ya kutengeneza sabuni hizi nyingi zao hazijafikia kile kiwango ambacho kinachotakiwa kwa mfano cha madawa yanayotiwa au manukato na kadhalika, ni vingi ambavyo ni vya wajasiriamali.

Mhe. Naibu Spika, lakini tunajitahidi kuwaambia *ZBS* na vile vile *TBS* wanasaidia kuhakikisha kwamba na wao kidogo kidogo wanafuata maelekezo wanayopewa ili waweze kufikia kiwango kinachotakiwa. Kiwanda hiki kuanzia mwaka 2015 tarehe 17 mwezi wa Septemba kilifanyiwa ukaguzi wa kwanza, *sample* 30 zilichukuliwa na *ZBS* za aina mbali mbali, maana kuna sabuni za mwani, sabuni za mchaichai, sabuni za *caliptors*, sabuni za karafuu na kadhalika. Aina tano zimechukuliwa lakini vile vile kwa kawaida *ZBS* huwa wanakwenda wakaangalia maeneo yale yanayofanyiwa ile kazi wakaona maeneo yenyewe. Mimi mwenyewe pia nimekwenda kuangalia bado kuna mambo ambayo yanatakiwa yakamilike ndio kiwanda hiki kiweze kupewa huo ubora.

Mhe. Naibu Spika, walielekezwa kwamba jamani tengenezeni kituo cha kupimia kama *laboratory* ya kupimia na *ZBS* waliwafanyia michoro na wakawasaidia kazi nyengine, lakini mpaka sasa hivi jambo hilo halijafanywa.

Mhe. Naibu Spika, mimi mwenyewe binafsi nilikuwa na kikao nao walikuja Ofisini kwetu na tukawaambia, kwa ajili ya hizi

sabuni kutumika hapa hapa Tanzania sisi hatuoni tatizo kubwa lakini hatuwezi kukupeni *certificate* ya ubora kwa sababu hao ambao watakuja ku-*certify* ni Wamarekani na Wamarekani watataka kitu ambacho kina uhakika watakwenda mpaka katika kiwanda kuangalia na kiwanda kile vile kilivyo wanavyotengeneza sabuni zao, walivyoweka *raw material* zao na kadhalika bado hakijaweza kufikia kupewa ubora huo.

Mhe. Naibu Spika, mimi nakubali kwamba ni muhimu hiki kiwanda kipewe ubora lakini kwa hali ilivyo, niliwaomba mimi basi waje tutafute wataalamu watakaowezesha sasa kutengeneza sabuni zao kwa mujibu wa viwango. Kwa mfano niliambiwa kama kuna dawa fulani wanayotumia katika sabuni ni nyingi sana na tuliwaambia basi kapunguzeni hiyo dawa ili sabuni hizi ziweze kupitia na hasa *TBS* wakufanyieni na mpaka sasa hivi nafikiri jambo hili hawajalifanya.

Kwa hivyo si kama kampuni hii wajasiriamali hawa wanaonewa ama nini, najua milioni thalathini dola ni kitu pesa nyingi sana lakini nawaomba bado warudi tuwatafutie wataalamu wa kutengeneza sabuni ili ile sabuni yao iweze kufikia ubora ambao unatakiwa katika upande wa kwamba wanatakiwa Wamarekani wapate *certificate* ile. Sio kwamba kwa matumizi ya Zanzibar peke yake lakini isahihishwe na ikabidhiwe kwa hii kampuni ambayo inawasaidia wao, wabia wao Wamarekani. Kwa hivyo nawaomba tu warudi tena Ofisini tuweze kutafuta watu ambao ni wataalamu waweze kuwasaidia wafikie katika kiwango hicho ambacho kitakubaliwa na *ZBS* na pia *TBS.* Kwa sababu mpaka *TBS* nimewapelekea dakika za mwisho mwaka 2017 mwezi wa Febuari tumewapelekea pia bidhaa zao hizi, lakini mpaka *TBS* hawakuweza vile vile kuwapa *certificate* hiyo ya ubora.

Mhe. Naibu Spika, jengine ambalo lilizungumzwa na Kamati yetu katika ripoti yao ni kuhusu suala la maghala. Mwaka jana niliulizwa suala la maghala nikalitolea ufafanuzi, nikasema maghala mengi yaliyokuwepo hapa kwetu Zanzibar yalitokana na BIZANJE, yalitokana na Shirika la Viwanda, yalitokana na Shirika la Songambele. Maghala haya mengi yao yameuzwa mengine, mengine yamekodishwa na mengine sasa hivi yamebadilishwa matumizi. Kwa hivyo tulitakiwa tutoe taarifa tumepeleka taarifa sisi maghala yalivyo yote, tumegundua kwamba baadhi ya maghala tuliambiwa tarehe ya kumalizika mkataba ule umekwisha lakini bahati mbaya maghala mengine yakawa yameongezewa mkataba.

Sasa mimi nakubali kwamba wanataka tutoe taarifa nyengine za ziada. Mimi nitaomba tutashirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango kwa sababu hawa wana uhakikimali na hii mali haiko kwenye Wizara ya Biashara tena kwa sababu sehemu kubwa ya mali hii zilikuwa za zamani na zimekabidhiwa kwa Mhakikimali; tutashirikiana na Mhakikimali atayarishe taarifa inayotakiwa ili Kamati nayo wapelekewe tufikie hatma ya hili suala. Lakini kweli maghala ya serikali yalikwepo lakini mengine yameuzwa, mengine yamekuwa mahoteli, mengine yamefanyiwa mambo mengine. Kwa hivyo serikali ilitoa uamuzi wa halali kwa wale wengine ambao waliouziwa na wale ambao wameongezewa muda pia ni utaratibu wa halali. Kwa hivyo tutashirikiana na Wizara ya Fedha, Uhakikimali kuleta taarifa hiyo ambayo inayotakiwa.

Mhe. Naibu Spika, jengine ambalo lilizungumzwa na Kamati ni kuhusu *ZBS* na utaratibu wa kununua vifaa kwa ajili ya maabara. Naomba nitoe taarifa tu kwamba taratibu zao zimekamilika na vifaa vyote vilivyokuwa vifike vimeshafika, tunategemea sasa hivi kujiandaa kwa vifaa kwa maabara ya mwaka 2018, utaratibu

wa mwaka huu kwenye bajeti umepewa pesa vile vile kununua baadhi ya vifaa kwa ajili ya maabara ambayo itakayofuata mwaka unaokuja wa 2018. Mhe. Naibu Spika, hiyo kazi nimeshaifanya na tuko pazuri na *ZBS* sasa hivi itaendelea kutoa huduma kama inavyotakiwa.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, sasa naomba nije nijibu hoja za Mhe. Suleiman Sarahan Said. Mhe. Suleiman Sarahan alizungumza mambo mengi lakini kubwa ambalo nataka nilizungumze mengine nitayazungumza huko kwa sababu yameunganika na wengine, ni kuhusu suala la Kiwanda cha Makonyo. Hili limezungumzwa na yeye na Mwakilishi mwengine nafikiri Mhe. Abdalla Maulid Diwani. Kiwanda cha Makonyo kipo Pemba Chake Chake. Wizara ilifanya utafiti kwa kushirikiana na *TILDO* kampuni hii ya *TILDO* ya utafiti kutoka Tanzania Bara, wakawaangalia kile kiwanda vizuri sana na wakatoa mapendekezo kwamba tatizo la moshi litatuliwe kwa kuwa na vifaa ambavyo vitapelekea ule moshi uende juu zaidi, kusudi usishukie chini ardhini na kuwaumiza wananchi. Kwa maana hiyo kwamba sisi Wizara hatufikirii kama kiwanda tutakihamisha, kwa sababu ni gharama sana kukihamisha kile kiwanda. Lakini pia tuliwaita Kampuni ya India ikafanya *adjustment,* kile kiwanda sasa lile bomba limeongezwa kutoka mita 15 mpaka mita 24 ili ule moshi usiwaathiri zaidi na sasa hivi ukiangalia kuna tofauti kubwa kati ya kabla hapo na sasa hivi.

Lakini pia hivi karibuni tumeita wataalamu na tumeona kwamba kile kiwanda kinatumia mashine za zamani sana na zimeshapitwa na wakati, kuna uwezekano kama tutaweza kupata wawekezaji kuweza kukiangalia kile kiwanda na kukibadilisha mashine tukitia mashine za kisasa zitakazoweza kutoa mafuta mengi na vile vile kutoa mafuta yaliyokuwa safi.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa samahani kidogo, Waheshimiwa Wajumbe mnaotoka murudi haraka kwa sababu kutakuwa na kupitisha vifungu na *quorum* yetu ni ndogo. Kwa hivyo naomba mkimaliza tu najua mnakwenda kusali lakini mkimaliza mrudi. Endelea Mheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Naibu Spika, Mhe. Suleiman Sarahan pia alizungumzia kuhusu mazao mengine kwa mfano alizungumzia mazao ya maembe na vile vile suala zima la vipodozi na manukato. Na mimi nilieleza katika hotuba yangu kama sasa hivi tuna mikakati mengine mipya na hii nataka nizungumze kwa ujumla, kwa sababu Wajumbe wengi walizungumzia suala hili.

Mhe. Naibu Spika, sisi pale Wizarani tuliangalia, kwanza niseme tu kwamba Sheria ya Viwanda ipo, Sera ya Viwanda ipo, Sera ya Ujasiriamali ipo na Sheria ya Ujasiriamali ipo. Sheria ya Viwanda ni ya mwaka 1998 wakati huo kulikuwa kuna sera yake na sheria yake. Kati kati hapo Mhe. Naibu Spika, kulikuwa na mapendekezo, Wizara haijakaa tu kuangalia sheria toka mwaka 1998 wakati maamuzi mengi yamepita ya Serikali lakini pia hali halisi ya uchumi inabadilika na hali halisi ya mazingira ya dunia inabadilika, huwezi tu kuwa na sheria ya 1998 bila ya kuitizama. Lakini kubwa kwamba Sheria hii ya 1998 haikufanya kazi vizuri, mule kwenye Sheria kuna mambo mengi yamezungumzwa mpaka masuala ya *cash economic zone*, masuala ya kuwa na vituo kama mfano hiyo *SMIDO* yamezungumzwa kwenye Sheria ile lakini hayakutekelezwa.

Kwa hivyo Sheria hii ikabidi tuifanyie mapitio. Sasa ninachozungumzia hapa kwenye hotuba yangu kwamba tuliwaomba *UNIDO* kupitia Sera yetu ya Viwanda ili Sera hii

iendane na wakati, na hapa tukasema kwamba Sera hii kwa sababu tunaweza kufanya jambo ambalo linawagusa watu wengine, Sera ya Viwanda sio Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko peke yake, Sera ya Viwanda inawahusu wafanyabiashara, inawahusu sekta nyengine kama Kilimo, Mawasiliano, Wizara ya Fedha, *Chamber of Commerce* na kadhalika. Kwa hivyo wote hawa wanatakiwa watoe maoni katika hizi Sera tunazozipitisha ikiwa ya biashara, ikiwa ya viwanda na sheria zake lazima hawa tunasema walengwa watoe maoni, kwa sababu tunataka hizi sheria ziweze kufanya kazi ikiwa sheria kama zinafanywa zikawa kama za 1998 mambo mengi hayakutekelezwa.

Kwa hivo katika suala zima hili la kutizama Sheria na hizi Sera za Viwanda tukasema tuweke mkakati katika kuangalia na ku-*prioritize* viwanda vya aina gani. Kwa hivyo tuka-*prioritize* vianda katika sekta vifuatazo:

Kwanza tumesema viwanda vinavyotokana na kilimo (*agro-industry*) na ndio hivyo ambavyo Mhe. Suleiman na wengine wamezungumzia, vikiwemo Viwanda vya Makonyo, masuala ya karafuu, matunda, mbogamboga na vitu vyengine ambavyo vinavyotokana na upande wa kilimo.

Sekta ya pili tukasema tuangalie viwanda vinavyotokana na mambo bahari, ndio maana tukasema kwamba sasa hivi tunakwenda katika suala zima la *blue economic*, sio tu kuangalia uvuvi tu lakini *blue economic* tutaangalia sekta nzima ya bahari, uchumi wa bahari. Kwa hivyo kuna uvuvi, kuna ufugaji wa maji baridi, kuna ufugaji wa samaki na vitu vyengine, kuna ufugaji wa pweza, majongoo na kadhalika na mambo mengine. Kuna chumvi, kuna mwani na kadhalika hii yote inaitwa *blue economic*,

ukienda *deep* zaidi unakuta mpaka masuala ya mafuta yaliopo baharini na kadhalika.

Sekta ya tatu tukasema ni *manufacture,* yaani uzalishaji katika viwanda. Humu ndimo ambamo tunashirikiana na Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo kuwa na viwanda ambavyo vitaweza kuchangia katika sekta ya utalii ili watalii wakija waweze kununua bidhaa zao na waweze kuondoka nazo.(*Makofi*).

Sekta nyengine tuliyosema muhimu ni ya suala la upande wa madawa. Upande wa madawa kwa mfano chumvi sasa hivi kuna watu wanafanya chumvi lakini pia wanafanya madawa yanatokana na chumvi. Kuna *caustic powder,* kuna *baking powder* na kila kitu wanafanya baadhi ya watu. Kwa hivyo hii nayo ni sekta ingawa ni ndogo sasa hivi, lakini tunataka tuipandishe na vile vile kuangalia *EPZ* ambazo zitakazokuja kutengeneza madawa ya binadamu. Kwa hivyo nayo sekta hii tumeipa kipaumbele.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, sekta nyengine ambayo tumeipa kipaumbele ni katika kuangalia teknolojia. Teknolojia itaajiri vijana wetu wengi sana. Kuna nchi sasa hivi wako nchi moja lakini wanafanya vifaa kwa ajili ya nchi nyengine na wanauza, wanafanya ramani, wanafanya taarifa mbali mbali. kwa hivyo teknolojia tumesema nayo ni sekta ambayo tunataka kuifanyia kazi huko mbele.

Mhe. Naibu Spika, nije katika sekta hii ya viwanda vya kilimo. Kwa hivyo masuala ya embe, shokishoki na vyengine vyote hivyo vimo katika hii sekta ya kilimo. Mhe. Naibu Spika, tatizo liliopo sisi Zanzibar kilimo chetu uzalishaji umepungua, tukitaka viwanda viende lazima uzalishaji uwe mkubwa. Tumemsikia Waziri wa Kilimo akizungumzia mikakati yake lakini bado sisi

tunasisitiza kilimo cha matunda, mbogamboga, *spice* na kadhalika uzalishaji wake lazima uongezeke. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nimetembelea nchi nyingi kwa nia ya kutafuta soko lakini kila unakokwenda unaambiwa soko lipo mnaweza kuzalisha kiasi gani? Unasema mimi naweza kuzalisha 60, anakwambia mimi nipe kontena mia moja kwa mwaka mnaweza kutoa? Hatuwezi Mhe. Naibu Spika. Natoa mfano pilipili manga tumetakiwa kontena 10 imetuchukua mpaka leo tumeshindwa kupeleka kontena 10. Kwa hivyo tunapenda maendeleo na tunataka maendeleo yapatikane lakini sisi Wawakilishi tuna wajibu na tushirikiane na Wizara ya Kilimo, tuna wajibu kuhimiza kilimo. Kwa sababu viwanda vya Zanzibar kwa kuanzia lazima vitokane na raslimali ambazo tunazalisha sisi wenyewe na raslimali ya Zanzibar ni *spices*, mbogamboga na matunda. Mhe. Naibu Spika, zamani tukiuza embe sisi za Muyuni tukiuza Muscat, nani sasa hivi anauza embe za Muyuni hakuna. Lakini tulikuwa tuko juu tumekwenda chini kabisa. Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, kutoka chini kwenda juu lazima tutafute mkakati wa kuweza kuongeza mazao haya tuweze kuyasindika. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, la pili tunapozungumzia usindikaji si lazima uwe na viwanda vikubwa, hawa wajasiriamali sasa hivi wapo na wanafanya kazi hii vizuri sana, utakuta bidhaa zote mimi kwangu Mheshimiwa anayekuja aje atizame, kuna bidhaa za kila aina, kuna ma-*salad masala*, kuna kila kitu. Lakini sasa ukiwaambia, sasa tupeni *quantity* kubwa, hawana uwezo. Kuna kampuni zimekwenda Dubai kwenye maonesho wakaambiwa tunataka bidhaa za *spices* hawakuweza kupeleka kontena nyengine. Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, tutilie mkazo kilimo hiki kiendelee ili tuweze kuuza biashara zetu.

Huko huko tukizungumza masuala ya nazi yanakuja humo humo, nazi minazi haipo tuwe na ratiba ya kuongeza minazi, minazi yote imekatwa. Hivi leo pale viwanda vidogo vidogo kuna Kiwanda cha Mafuta kutoka China hawawezi kununua nazi hapa hakuna, nazi itoke Tanga. Sasa hivi mfano mafuta sasa hivi imekuwa *deal* maneno ya mjini, *deal* ya mafuta ya nazi lakini Unguja hakuna mafuta ya nazi zamani tukiuza, wala mbata hatuna zamani tukiuza, wala mashudu yale ya mbata tukifanya kutoka nazi sijui mashudu yanaitwaje hakuna. Vitu vyote havipo Mheshimiwa. Kwa hivyo hii *speech* yetu imekaa kama ni *wake-up call* kwa Wawakilishi na wananchi wa Zanzibar sasa hivi tujibadilishe tujipange vyengine. Shokishoki hazitoshi haziko, tunataka shokishoki zetu ziko wapi za kuuza kiasi hicho? Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, hii ni *challenge* ya Wizara ya Kilimo na serikali kwa pamoja, tuongeze uzalishaji tuweze kutengeneza na kusarifu vifaa vyetu, mazao yetu ili tuweze kwenda mbele. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Suleiman Sarahan Said alizungumzia masuala ya kutoa mashine ndogo ndogo na nitamuunga mkono Mhe. Ali Suleiman Ali na wote waliozungumza masuala ya kuwapa nguvu wajasiriamali. Mhe. Naibu Spika, wajasiriamali sisi Wizara ya Biashara tunawapenda sana na ni wadau wetu wakubwa sana, kwa nini nasema hivyo. Kwa sababu katika hesabu niliyopewa ya haraka haraka viwanda vilioko Zanzibar ni kama 2,015; asilimia 95 ya viwanda hivyo ni wajasiriamali.

Tafsiri ya wajasiriamali nini? Ni wale ambao wanaoajiri watu chini ya tano mpaka watu zaidi labda ya kumi, lakini kila ukienda juu unaanza kuingia katika viwanda vidogo vidogo. Kwa hivyo ukichukua hiyo sehemu asilimia 95 ya Zanzibar ni wajasiriamali wengi na viwanda vidogo vidogo. Viwanda vilivyokuwa vikubwa hapa Zanzibar nitavihesabu ni cha Kiwanda cha Sukari-

Mahonda; Kiwanda cha Said Salum Bakhresa cha Azam; cha unga wa ngano. Viwanda vitatu hivi ndio vikubwa na Kiwanda cha Makonyo cha Pemba. Viwanda vinne ndio vikubwa ndio viwanda hasa ukisema habari ya viwanda hivi ndio viwanda, lakini vilivyobakia viko vya kati kati, kuna cha CHATEPA cha Chai na vyengine vidogo vidogo vya chai na vya *spices*.

Kwa hivyo mimi nilipozungumza na wajasiriamali hawa ndio watu ambao tunawalenga kwa sababu ndio ambao wanatakiwa wakuzwe, wanaita kuwa-*graduate* kutoka wadogo, kuwa wa kati na kuwa wakubwa. Kwa hivyo sehemu kubwa ya sera ya wajasiriamali sisi tunasimamia sera ya wajasiriamali, wenzetu wawekezaji wanasimamia wajasiriamali wao wenyewe ndio wana-*deal* nao, wanakaa nao, wanazungumza nao na sisi tunasimamia sera, sisi tunawasaidia pale ambapo tunahisi tuwasaidie. Lakini baada ya hivyo tumepitia hii Sera ya Wajasiriamali ya mwaka 2006 na tukasema kwamba lazima twende mbele zaidi, kwa vipi? Twende mbele zaidi kwa kuwajengea chombo cha kuwasimamia kuwapa teknolojia, kuwapa mikopo, kuwatafutia masoko, kuwaunganisha na mambo ya mashine mbali mbali. Mhe. Suleiman Sarahan alizungumza mashine ndogo ndogo na Mhe. Ali Suleiman alizungumza mambo hayo hayo.

Mashine ndogo ndogo lazima kuwe na chombo kinachowapatia mashine na utaalamu huo. *SIDO* wanafanya hivyo. Zanzibar hakuna chombo kama hicho. *Mbweni Technology Collage* sasa hivi kuna *incubation* wanawasomesha, wakitoka pale hawana tena kwenda kununua mashine wala hawapewi nini. Kwa hivyo *SMIDO* ndio watakaokuwa kazi yao hiyo kuwasomesha, kuwapata mkopo, kuwapatia mashine ndogo ndogo na kuwasaidia soko, vile vile ku-*identify* bidhaa, maana wakati mwengine

unaweza kufanya bidhaa ukafikiria wewe mwenyewe, lakini bidhaa ile haina soko. Kwa hivyo tutawasaidia kuwaambia mwaka huu tunataka mtayarishe bidhaa za aina fulani ili muweze kuingia katika soko la ndani na soko la nje ya nchi.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, nitakupa mfano wa suala moja. Kwa mfano unga wa muhogo Unguja sasa hivi umekuwa *deal* haupo kabisa. Lakini unga wa muhogo una soko Muscat na Dubai. Kwa hivyo unapokuwa unafanya biashara kama hii lazima tuwaambie wajasiriamali, jamani ingieni katika utaratibu wa kutoa *product* ambayo ina soko, ziko nyingi ambazo zina masoko lakini bado utaratibu hatujaweza kuuweka vizuri.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli kwa upande wa wajasiriamali tumejiandaa vizuri sana na ningewaomba Waheshimiwa Wawakilishi wawe na subra tuone mwaka huu tunajitahidi kuendelea kuwapangia utaratibu mzuri na kuuweka kabisa katika wizarani kwetu na Wizara ya Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi na vile vile tumeshakaa Wizara zote tatu hizi tumeshakaa tunafanyakazi kwa pamoja tumekubaliana, tushafanya vikao zaidi ya vinne tumewashirikisha wafanyabiashara, tumewashirikisha mabenki, benki nne zimekuja na wako tayari kutoa mikopo na vile vile tumesema tuwapatie utalaamu *SIDO* wamekuja na wako tayari kuwafundisha, tumezungumza vile vile na chombo kama hichi cha India cha kuwafundisha. Kwa hivyo tuko vizuri sana Mhe. Naibu Spika. Ningeomba tu yale masuala yaliyozungumzwa yote hapa pili pili hoho na kadhalika yote haya tunayatizama vizuri zaidi.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, vile vile nizungumzie suala la viwanda, kwa mfumo Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) alizungumza habari ya

viwanda vya ujenzi vilioko Bara vya *tiles.* Ni kweli viwanda ya ujenzi viko Bara na saruji ya Dangote imeshawahi kuingia huku, kwa hivyo sisi hatuzuii bidhaa za Bara zinakuja na wananchi wanafaidika na sisi tunatizama utaratibu gani tunaweza na sisi kuwa na viwanda vikubwa kama hivi ili nayo vile vile biashara hii iweze kwenda Bara.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf alizungumzia kwa urefu kuhusu takwimu nilizotoa. Mhe. Naibu Spika, tukubalia wala tusiwe na ubishi kwamba biashara Zanzibar na Bara imepungua. Lakini pia biashara na nje katika kuuza sisi nje mwaka jana ilipungua, kwa sababu mwaka jana karafuu imepungua hatukuuza nyingi, lakini vile vile mwani umepungua hatujauza mwingi. Hayo yote ni ukweli wala haupingiki.(*Makofi*).

Vile vile uagiziaji anataka kujua uagiziaji mkubwa ni bidhaa zipi. Ni bidhaa zote ambazo tunazoagiza Zanzibar sehemu kubwa ni bidhaa zinazotoka nje ya nchi na nyengine zinazotoka Bara, mbali ukiacha mchele, ukiacha vyakula. Lakini bidhaa nyingi madawa na kadhalika kama hayakutoka India na Pakistani na kwengine basi yatakuwa yanatoka Bara. Kwa hivyo *list* ya bidhaa tunazotumia sisi kutoka Bara, maji, vibiriti na kadhalika.

Hili ni suala jengine la matatizo ya biashara kati yetu sisi na Bara. Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango amelizungumza vizuri. Niseme tu kweli hii hali ipo na tuna wajibu wa kuzungumza na Serikali ya Muungano, tumejitahidi kukutana na wenzetu wa Serikali ya Muungano mpaka juzi wametuletea jawabu wakasema wao wako tayari tulizungumze wakati wakimaliza bajeti yao na sisi.

Sisi Mhe. Naibu Spika, tumejiandaa kwa sababu hii ni nchi moja ya Tanzania. Kwa hivyo soko la Tanzania ni soko letu wote, haiwezekani ikawa soko likawa la Bara lakini Zanzibar hawali-*access* soko la Tanzania Bara. Hiyo inakwenda bila ya mazungumzo. Sasa kuna vikwazo vikwazo vidogo vidogo ukiuliza unaambiwa Afisa mmoja kafanya hivi na mwengine kafanya hivi. Ndio maana tukasema tukae na Serikali ya Muungano sekta inayohusika ili kujadili mambo haya na kuweza kuyamaliza.

Kwa hivyo ninachokuombeni n ndugu zangu Waheshimiwa Wawakilishi msubiri tuzungumze na Serikali ya Muungano, kwa sababu hii *list* ya bidhaa zinazokwama kwenda Bara ni nyingi, sio maji peke yake, maziwa yalikwama, maji, madawa na kadhalika, mpaka chai ya *spice* ilishakwama akaambiwa wewe huwezi kuuza hapa mpaka ufungue *agent.* Haya ni mambo ambayo tunayasema yanazungumzika wala yasitufanye kufikiria vibaya, ni maofisa wadogo wadogo pengine huko au nini ,lakini sisi tunangojea Waziri wa Biashara Serikali ya Muungano na watendaji wake na sisi tutakaa kulizungumza hili na halafu kulipeleka katika vikao vya Muungano. Naweza kusema kwamba hili jambo limebakia halijazungumzwa bado. Kwa hivyo muwe na stahamala msuburi tulizungumze. (*Makofi*).

Jengine Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango ameshajibu masuala yanayohusiana na sisi ya *Chamber of Commerce* na *private sectors* na kadhalika ameshajibu, namshukuru sana mchango wake Mhe. Waziri wa Fedha umesaidia. (*Makofi*)

Jengine Mhe. Naibu Spika, ni mchango wa Mhe. Omar Seif Abeid. Mhe. Omar Seif Abeid alizungumzia kuhusu hizi *figures.*

Nadhani niseme tu tumeshazowea kuzungumza bilioni lakini mwaka huu tunakwenda kunako trilioni, na ndio manaa tukawa hatukuisema mambo ya bilioni hapa. Lakini hizi takwimu zote mnanzoziona ni za bilioni. Kwa hivyo hapa hakuna ubabaifu wala hakuna upotofu wa takwimu, takwimu zinajieleza na takwimu hizi ni zetu tumezipeleka Kwa sababu takwimu ndio kituo cha takwimu zote za nchi. Kwa hivyo ingawa sisi tunazizalisha takwimu hizi lakini tunazipeleka kule.

Jengine Mhe. naibu Spika, nisema sasa hivi sisi tumeona udhaifu tuliokuwa nao hata kama najua mnakumbuka Mhe. Rais alituitisha Mawaziri wote na wizara zote kwenda kupewa somo kuhusu takwimu, na tumelikubali somo lile na sasa hivi tunarekebisha. Ndio maana nikasema humu watendaji wangu wamebadilisha wameshasomeshwa utaratibu wa kuweka takwimu vizuri. Kwa hivyo takwimu mtakazoziona mwakani zitakuwa tofauti. Na vile vile nimuunge mkono Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi alizungumzia kuhusu ma-*paychart* na kadhalika katika bajeti yetu. Mheshimiwa watalaamu tunao mwakani tutafanya hivyo, tutakuleteeni hizi *chart* na nini na nategemea mtaweza kuzifahamu tutakufahamisheni. Lakini tunataka tuanze mwakani katika utaalamu ambao tumepewa nitakuleteeni na mtaziangalia hizi takwimu moja baada ya moja.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, ninakubali labda kwamba humu kuna mambo mengine hatuyaeleza kwa urefu kwamba sababu nilidhani kwamba hichi kitabu kitakuwa kikubwa sana na maeneno yatakuwa marefu zaidi. Lakini tutafanya hivyo mwakani mtayaona mambo mengine tofauti, tutakwenda kwa mujibu wengine humu watalaamu mnavyotaka au mlivyozowea tutakwenda hivyo. Mara nyingi mimi huwa nasema Wizara ya

Biashara ni wizara ya viwango, basi mwakani tutaongeza viwango vyetu muone hivyo mnavyotaka iwe. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, kuhusu Kiwanda cha Mahonda. kiwanda cha Mahonda labda niunganishe na viwanda vile ambavyo zamani vilivyokuwa vikifanya kazi halafu vikawa vimekufa. Katika jambo la mwanzo tulipokuwa tunataka kupitia hii sera, kui-*review* hii sera tukasema tuangalie tumekosea wapi, tusiangalie tulivyoanguka tuangalie tulivyojikwaa. Tumeangalia tukakuta mambo mengi kama walivyosema wenyewe Waheshimiwa hapa vilikuwa vyengine *input substitution* yaani vinanunuliwa vitu kutoka nje, vyengine vinategemea *raw materials* kutoka nje, vyengine vilikuwa ghali uendeshaji wake, vyengine ubadhirifu alizungumza Mhe. Mwakilishi hapa, wizi ulikuwa mwingi na nadhalika.

Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, viwanda hivi vimekufa na vilikuwa vingi, vyengine vilikufa na vyengine vikawa-*privatize*, maana sio vyote vilikufa. Lakini tukasema tuangalie hivi ambavyo vina muelekeo wa kufufuka ndio tukatembelea Kiwanda cha Soda, tutakuta Kiwanda cha Soda kimekufa kwa sababu ya *competition*, cha soda hakijafa kwa sababu ya wizi au nini, kimekufa kwa sababu ya *competition.* Na hii ni kwa sababu wafanya biashara wengine si wa kweli, wanaagizia bidhaa ambazo zina *compete* na bidhaa zetu. Kwa hivyo ninachoomba Waheshimiwa mwakani na nyinyi mlisisitize hilo kwamba bajeti yetu tulinde viwanda vyetu kwa kuwekea kodi halisi na vile vile uchunguzi kule bandarini uwe wa hakika. Kwa sababu kama vikopo vya soda vinavyokuja vinafichwa kunako magari, wanauza kirahisi wakati Kiwanda cha Soda wanakuwa hawawezi kuuza inakuwa ghali. Sisi wenyewe tunakwenda kununua soda, tunanunua soda ya aina ya Shani. Shani shilingi efu moja iweje kutoka Dubai wakati huyu wa

Kiwanda cha Soda hawezi kuuza Shani kwa shilingi kwa shilingi elfu moja, kama vile hawalipi kodi au nini. Kwa hivyo hilo ni moja sababu yenyewe.

Lakini kwa upande wa Kiwanda cha Mahonda kile baada ya kufufuliwa kikaja hichi cha sasa hivi kinazalisha kwa mwaka, kwa sababu tatizo walilokuwa nao Kiwanda cha Mahonda hawana ardhi ya kutosha kuzalisha miwa. Kama unavyojua kiwanda unatakiwa ukilishe ndio kiweze kutoa matunda. Kiwanda cha Mahonda waliahidiwa kupewa ardhi lakini ardhi yao sehemu kubwa hawajapata, ardhi yao ndio inatumiwa na wakulima sasa hivi na nyengine ziko katika maeneo mengine ya serikali. Kwa hivyo wanazalisha wao sasa hivi mwaka huu walivyozalisha wamezalisha tani elfu nne na kidogo ya sukari.

Lakini hawa wanao uwezo wa kufikisha mpaka tani elfu saba, mpaka eflu tisa kama watapewa uwezo wa kuweza kupata ardhi ya kulima miwa. Tumewashajihisha kwamba sasa hivi wafanye utaratibu wa *contract farming* ni upi, wa kuwataka wakulima wengine walime miwa ili wao wanunue miwa na hiyo wameshaanza. Kuna wakulima wanalima miwa sasa hivi lakini tukienda mbele basi na wananchi wa Zanzibar washajihike zaidi walime miwa. Kiwanda hichi kama hakina miwa hakiwezi kuweza kuzalisha sukari, kwa sababu miwa ndio *material* yake, unakilisha miwa kile halafu ndio kizae sukari. (*Makofi*).

Lakini niseme Mhe. Naibu Spika, ni kiwanda kizuri, cha kisasa kina uwezo mkubwa sana wa kuweza kufanya kazi. Lakini pia kina uwezo wa kuendesha uchumi sehemu kubwa ya uchumi wa Kaskazini. Kwa mfano umeme wanatoa, kuna maji wanalizalisha na nakadhalika. Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, kiwanda hichi tukiendeleze na tukipe *support* ya kila aina na serikali ndio maana

ikaunda kamati tukakabidhiwa sisi Wizara yetu ya Biashara kukisimamia. Kwa upande wa *spirit* sio kama ni *product* mpya wanayotengeneza, haya ni matokeo yanayotokana na sukari. Kwa hivyo wao wanapolipa kodi, wanalipa kodi pamoja na *spirit,* mashudu na vile wanaouza kwa ajili ya vyakula vya wanyama na kadhalika, wanalipia kodi vyote hivyo. (*Makofi*).

Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, hii *spirit* hapo zamani ilikuwa ikifanyiwa mnajua nyinyi "maziko saa nane", lakini sasa hivi wameitia rangi ndani hainywiki. Sasa hivi wanawauzia *University* na maskuli kwa ajili ya *laboratories,* lakini hao wenye kiwanda walifanya utaratibu wa kutengeneza haya wanaziita *stove* ambazo zinatumia *spirit* ambazo akinamama wengi wanapenda wa vijijini, si gharama kubwa kushinda gesi. Kwa hivyo wamekuja na tunawasaidia kuanzisha mradi huu ili uwasaidie na sisi tuweze kupata mapato mengine sasa, sio tu ya *stove* lakini ya kutumia *oven* na vile vile na mapato mengine.

Mhe. Naibu Spika, katika takwimu ya *export* vile vile ni sawa sawa ni bilioni hii sio shilingi milioni, mnaposoma muangalie kule juu kumeandikwa milioni ziro, ziro, ziro. Kwa hivyo ile inaonesha kwamba sio milioni ni bilioni hizi bidhaa zote zilizokuwa zimeoneshwa.

Jengine Mhe. Naibu Spika, kuhusu hesabu za mikarafuu. Karafuu Mhe. Naibu Spika, ningependa nimfahamishe tu Mhe. Omar Seif Abeid kwamba tunapokuwa tunauza karafuu, karafuu zipo za aina nyingi kama alivyosema yeye mwenyewe. Kwa bahati nzuri mwaka huu na hii nimeambiwa na watu wetu tuliowauzia karafuu, karafuu nyingi za Zanzibar kipindi cha miaka miwili hii zote zina ubora juu, nyingi zao zina ubora wa juu na kwa *average* hesabu waliofanya wenyewe ni kwamba karafuu zilizouzwa tani elfu

mbili mia mbili na thalathini kwa shilingi elfu kumi na nne, sawa na bilioni thalathini na moja nukta mbili.(*Makofi*).

Lakini pia kuna karafuu tani ishirini na nane zilizouzwa ambazo ni karafuu hai. Karafuu hai bei yake ni tofauti, tunaelewana karafuu ni *organic* na karafuu hai zilizouzwa ziliuzwa kwa shilingi elfu kumi saba na mia tano. Lakini pia unapouza karafuu hai bei pia inakuwa ni tofauti kushinda karafuu za kawaida. Kama karafuu hizi tuliuza kwa bei ya elfu nane na mia mbili, karafuu hai tumeuza kwa dola elfu tisa. Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, hesabu hizi ni sawa sawa ukijumlisha thalathini na moja nukta mbili na ziro nukta tano, unapata jumla shilingi milioni thalathini na moja nukta saba, hesabu hapa haikuchezewa ni sawa sawa kama tulivyokuwa tumesema.

Mhe. Naibu Spika, niongeze tu katika hili suala la wajasiriamali na hili alilizungumza Mhe. Omar Seif Abeid na Mhe. Hidaya Ali Makame. Wajasiriamali walemavu nao hao nao tunawapa kipaumbele, kuna walemavu waliokuwa hawaoni, kuna walemavu waliokuwa hawana viungo wote hawa tumewatia katika mkakati huo ili watakapokuja itakuwa inawahudumia na wao kuwawezesha kuwa na soko lao na zile bidhaa zao kuweza kuuza katika soko lao. Kuna mambo mazuri wanayafanya hawa katika baadhi ya vikundi, wanatengeneza ma-*doormat* na mambo mengine. Kwa hivyo wao ni binadamu na sisi tunawapa kupaombele.(Makofi).

Kwa upande wa suala zima la vijana tulisema kwamba mwaka huu tunataka tuwatumie vijana, kwa sababu vijana kupitia Mabaraza ya Vijana wanapata bajeti yao, wanapata fedha za kujiendeleza. Lakini vile vile katika mkakati wetu mpya tumesema sasa hivi tuwe na mashamba kwa sababu tunataka

kuendeleza bidhaa za kilimo, bidhaa za *spices* na *spices* lazima uwe na mashamba ya mchai chai, mashamba ya mreheni, mashamba mengine na kadhalika na kadhika. Sasa vijana lazima wapaiwe eneo waweze kulima bidhaa hizo.

Kwa hivyo vijana tutakuwa nao na tutawapa kipaumbele na nilisema pale mwanzo mabenki wametwambia wako tayari kutoa mikopo, lakini mikopo hii iende katika vikundi. Tumeshazungumza na tutaendelea kuzungumza na kuona kwamba tunawawekaje vijana ili Halmashauri za Wilaya na vile vile Mfuko wao wa Mabaraza uwasaidie kuanzisha biashara. Bara wameanzisha kuna miradi mingi ya vijana kwenye Halmashauri, miradi ya kufuga ng'ombe, wanatengeneza maziwa, yanategeneza *yogurt* na kila kitu. Kwa nini wameweza wao na sisi tushindwe na najiuliza kila siku, haitowezekana tutaweza kuwashajihisha vijana wetu tukiwa tunakaa pamoja na kuunganisha nguvu tulizokuwa nazo. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, kuhusu wakulima wadogo wadogo. Hili nalizungumza kwa upekee. Mhe. Naibu Spika, siku moja tulifanya kikao sisi tukauliza wakulima wameshajihishwa, kwa mfano wakulima wanaolima tungule. Mwaka juzi wakulima walima tungule mpaka nikawakuta kwenye *incubation* wanafundishwa jinsi ya kulima tungule na kuweza kuzitengeneza. Baadae tungule zikawa nyingi soko likawa limekwenda. Suala ambalo nilililokuwa nawauliza kila siku nikikaa na wenzangu, kwanza mkataba uliokuwa umetiwa saini kati ya wafanyabiashara wenye mahoteli na wakulima wetu na jinsi watalavyoweza kupata bidhaa zao, hapa Zanzibar mkataba wa aina gani. Sasa sielewi kama kuna mkataba ulitiwa lakini kama mkataba haupo lazima wenye mahoteli na wao wachangie wanunue bidhaa zetu. Lakini la pili

katika kuuliza watu wa kilimo wakatwambia kwamba hakuna utaratibu huo.

Kwa hivyo mtu anapotaka kununua tungule kwa mfano hawa watu wa mahoteli anakuja hapa Soko la Mwanakwerekwe au anakwenda kwengine na huo si utaratibu mzuri. Utaratibu mzuri lazima kuwekwe eneo ambapo wakulima watakwenda kuuza vitu vyao kule kwa utaratibu uliowekwa na wenye hoteli watakwenda kuchukuwa vitu vyao kule. Haya tumezungumza pamoja na Wizara ya Kilimo na Wizara Uwezshaji ili serikali iwe na msimamo. Hatuwezi kuwaachia wenye mahoteli wakanunua vitu kutoka nje ya Zanzibar, lazima wanunue vifaa vyetu kutoka Zanzibar, bila ya hivyo bidhaa zetu zitakuwa haziuziki. Kwa sababu sisi tunajenga soko lakini soko hatulitumii. Soko maana yake ni kufuatilia hawa ambao wananunua. Hali hiyo ilikuwa kwa upande wa asali, asali ilikuwa inatengenezwa Zanzibar lakini ilikuwa wenye mahoteli hawanunui asali ya Zanzibar. Sasa hivi hali kidogo nimeambiwa imekaa vizuri. (*Makofi*).

Kwa hivyo sisi tumeshaanza kazi tutaendelea na wenzangu wizara nyengine tatu zinazohusika kuona kwamba hizi kasoro zinarekebishwa, soko lipo lakini halijapangwa vizuri. Hili suala liliulizwa bidhaa zinazokwenda Bara. Bidhaa zinazokwenda Bara ndio hizo bidhaa za magari, yaani nakusudia zile bidhaa kubwa ambazo zinatoa tofauti katika takwimu zetu, ni bidhaa za magari. Magari yalikuwa yanakwenda sana Bara lakini sasa hivi biashara hii imepungua kidogo yanakwenda magari, lakini sio kama kule miaka miwili nyuma ilivyokuwa imepungua. Lakini pia na bidhaa nyengine sasa hivi zinawekwa vikwazo. Kwa hivyo ndio maana takwimu hii ikapungua, kwa sababu vile vile mkumbuke kuna suala la usajili wa magari. Usajili wa magari Bara hawakubali

usajili ile *registration* ya Zanzibar. Kwa hivyo bado hapo pana hitilafu katika hilo vile vile.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, najibu hoja zile zilizokuwa peke yake peke yake pamoja ambazo wengi wamezichangia. Mhe. Naibu Spika, alitaka kujua *ZBS* na *ZFBA. ZBS* ni chombo cha viwango. Viwango vinavyotakiwa kwanza kwa ajili ya vitu vinavyoingia nchini, kuona kwamba vinakidhi haja ya viwango vile na nitatoa mifano. Lakini vile vile kwa bidhaa zinazotengenezwa ndani ya viwanda kwa sababu lazima kuwe na nembo ya viwango. Kwa sababu unapokwenda kwenye nembo ya viwango kuna maelezo pale unaeleza bidhaa hii ina kadhaa ina kadhaa. Lakini vile vile wanatakiwa waweke viwango vya Zanzibar, nadhani ndio hayo hitilafu tutazoziona kati ya viwango vya maji vya Bara (*TBS)* na viwango vya maji vya Zanzibar. Tumeshafanya mpaka sasa hivi viwango 71. Sasa viwango wanakaa wataalamu wetu, watalaamu wakikaa ndio wanapanga viwango vya maji, wataalamu wetu wamepanga maji ya Zanzibar na utaalamu wetu ni haya ambayo wameyasema, waliotia katika *list* ile.

Kwa hivyo kuna tofauti sasa hivi. Viwango vya Zanzibar halafu na viwango vya Tanzania Bara na kuna viwango vya *East Afrika*, tukeshajua hivyo itakuwa rahisi. Kwa hivyo *ZBS* inasimamia haya yote masuala ya viwango vya vyakula vinavyokuja na masuala ya vifaa vinavyotumia, masuala ya vifaa ambavyo tunasafirisha vyote hivi inabidi vinasimamiwa katika hili. *ZFBA* wao jukumu lao kuangalia yale masuala yanayohusu afya. Vyakula tunavyokula tumboni visituumize au tunavyowalisha watoto wetu visiumize au vinavyosambaa sambaa mjini visiwe vinaleta *polution*. Kwa hivyo *ZFDA* zaidi ndio maana ikaweko Wizara ya Afya, muelekeo wake zaidi ni wa mambo ya kiafya na sisi *ZBS* kuna mambo ya afya kidogo, lakini kama kuna jambo linalohusu

afya zaidi tunakwenda *ZFDA* kushirikiana na wao. Kwa hivyo nadhani hiyo ndio tofauti kubwa iliyopo, sio kwamba wafanyakazi wanaingiliana hapana. Kila mtu anafanyakazi kwa mujibu wa ile *mandate* aliyopewa, lakini kwa mujibu wa mambo ambayo anatakiwa wayafanye.

Mhe. Naibu Spika, nitatoa mfano mmoja *ZFDA* wameongeza chombo kule bandarini cha kuweka miozi, *ZBS* hatuweki mionzi sisi si kazi yetu. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, nafikiri Mhe. Panya Ali Abdalla atakuwa amenielewa. (*Makofi*)

Kuna masuala waliuliza Waheshimiwa Wajumbe kuhusu bidhaa mbovu zifuatiliwe na vingi tu walizungumza Waheshimiwa kuhusu bidhaa na vyakula vinavyokuja vimechelewa, inakuwa wanabadilisha ile nembo ya *safari date.* Ni kweli tumeyaona hayo Mhe. Naibu Spika, yote tumeyaona na hatua zimechukuliwa. Kuna kipindi mwaka jana tuliweza kuharibu bidhaa zaidi ya milioni kumi na saba zikachomwa moto na vyengine vikaangamizwa, tunaona na tunafuatilia. Kitengo changu cha ufuatiliaji cha Kumlinda Mtumiaji kinafuatilia, lakini pia na kuangalia suala zima la kuangalia vyakula je, vinafikia uzani unaotakiwa, vinafikia uzima unaotakiwa, tunafanya na tunatembelea maeneo yote na nimesema katika hotuba yangu tumetembelea maeneo yote na idadi ya sehemu ambazo tumetembelea.

Suala la mikate kuwa kuna mizani na kuwa kuna *standard* ya mikate, mimi nitalichukua na nitalifanyia kazi. Naona kweli tofauti zipo, kila mtu anafanya mkate wake na nini, lakini hilo nalipokea na tutalifanyia kazi. Hili amezungumza Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, jengine ambalo ni la kipekee alilozungumza Mhe. Suleiman Makame, mengine amezungumzia wajasiriamali, kwa nini tukawapa wajasiriamali hawa ambao walikwenda Uganda. Mhe. Naibu Spika, wizara yetu sisi Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko tunafanyakazi pamoja na Wizara ya Uwekezaji, lakini wajasiriamali hao wote wanaokwenda kwenye maonesho wako chini ya Wizara ya Uwezeshaji.

Mhe. Naibu Spika, sisi tulisaidia fedha na wao wenyewe walisaidia fedha. Kwa hivyo wengine walipewa nauli ya kwenda na wengine wakapewa nauli ya kwenda na kurudi, na wengine wakawa hawakupewa nauli. Wanatizamwa kwa mujibu, huwezi kujua soko gani kwa sababu ni maonesho. Tatizo kubwa liliopo hapa sisi hatuna uwezo wa kuwasafirisha wajasiriamali, bajeti yangu mumeiona nyinyi wenyewe hatuna uwezo huo, wala Wizara ya Uwezeshaji hawana uwezo huo. Kwa hivyo wajasiriamali wanaambiwa pesa tulizokuwa nazo ni ndogo na mara nyingi wenyewe wanashikilia kuwa tunataka kwenda. Kwa hivyo tunawaambia sisi pesa tutakazokutoleeni ni nauli, mkifika huko mtajitegemea wenyewe. Sio jambo zuri lakini tutafanya nini wakati sisi hatuna uwezo.

Mhe. Naibu Spika, hata nje ya nchi wanakwenda vile vile lakini wakifika kule wana bahati ama wanauza ama hawauzi inakuwa ni tatizo. Kwa hivyo nadhani tutalizungumza zaidi tena wizara zetu mbili ili kuona tutafanya nini, labda kuwa na malengo, sio kama kila mtu anataka kwenda kwenye maonesho aende, aseme nitakwenda kwa nguvu zangu. Lakini tutakuwa na malengo tutaona watakaokwenda watakuwa na tija, watarudi na wao vile vile wanufaike. Mhe. Naibu Spika, ni kweli walipata matatizo kwa sababu sisi hatukuwahudumia kikamilifu. Lakini pia nasema

tuombeeni mwakani bajeti yetu nayo iongezewe fedha ili tuweze kuwahudumia. *(Makofi)*

Suala la biashara za Pemba. Mhe. Naibu Spika, Pemba nafikiri jambo hili lilikuja hata ule wakati wa mimi nikiwa kiongozi awamu nyengine, kwamba utaratibu wa biashara Pemba. Hivi karibuni nilipata mtaalamu alikwenda Pemba, aliniambia faini alizozigundua akasema Pemba wanafanyabiashara zaidi na Tanga na Mombasa, kwa sababu wako karibu kule sana, lakini pia wanafanyabiashara na Zanzibar. Kwa hivyo suala la kutumia bandari ambayo itawarahisishia bidhaa zao ziwe karibu kupunguza gharama. Gharama huwezi kuzipunguza kwa sababu uko Pemba, gharama za usafiri zipo. Huwezi kutoa mzigo kutoka Unguja ukaupeleka Pemba bila kulipa gharama. Jambo ambalo la kuzungumza sasa hivi ni kuangalia, na vizuri Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji anakuja kesho na ameninong'oneza kwamba kuna utaratibu wanaufikiria wao wenyewe. Kwa hivyo kesho atakuwa na maelezo mengine mazuri pengine ameshafanya mambo mengine mazuri.

Mhe. Naibu Spika, lakini niseme tu Bakharesa meli hii ya *Sea Link* ilipoanza imeleta matumaini makubwa. Sasa hivi bidhaa nyingi zinakwenda Pemba kwa vizuri lakini vile vile zinatoka Pemba kwenda Tanga. Kwa hivyo hili alilosema Mhe. Mwakililishi tulifanyie kazi zaidi, lakini inawezekana mpaka hapo hii miundombinu itakapofanyika vizuri, basi kwa nini tusiwaruhusu Pemba wakapeleka bidhaa zao moja kwa moja Wete, Mkoani au Chake Chake, lakini kwa sasa hivi miundombinu hiyo haipo, tuwe na subra, serikali ikipata uwezo itajenga miundombinu hii angalau basi kama meli ifike Wete, nafikiri hilo linazungumzika Mhe. Naibu Spika.(*Makofi*).

Jengine ambalo alizungumza Mhe. Omar kuhusu biashara za bahari, sio kweli biashara za bahari zamani zilikuwa zikiuzwa na *ZSTC*, sasa hivi Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi wameanzisha mpango kabambe wa kuwashajihisha wakulima kulima biashara hizi za baharini, kama majongoo ya pwani, pweza, ngisi na kadhalika. Mhe. Naibu Spika, jambo hili ni zuri sana na mimi nakubali kwamba hili tutalifanyia kazi, katika suala zima la kuangalia masoko na hizi bidhaa za baharini tutaanza kuzifanyia kazi tena vizuri, ili na wao wanaohusika na biashara hii wapate tija. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Rashid Makame Shamsi aliyoyazungumza namuunga mkono kwa asilimia mia juu ya mia, kama mnavyoona sasa hivi bajeti yetu ni miaka miwili huu utakuwa ni mwaka wa pili, bajeti yetu iko sehemu kubwa ni *OC* na sehemu kubwa mishahara, na sehemu kubwa tunanunua vifaa kwa ajili ya *ZBS*. Lakini matarajio yangu mwakani bajeti ya maendeleo tuombe basi tutashirikiana pamoja bajeti ya maendeleo iongezeke. Lakini huwezi kuongeza bajeti ya maendeleo bila ya kuwa na mpango. Ndio maana tukafanya mapitio ya sera ya viwanda na kuna mkakati mengine. Kwa hivyo kwa mfano kwa *SMIDO* peke yake tumeomba kujenga vituo viwili vya kuweza kuanzisha na kuwasaidia wawekezaji wajasiriamali. Kwa hivyo peke yake hapo tutahitaji pesa nyingi kwa ajili ya utekelezaji sasa wa viwanda vyenyewe na usimamiaji wa viwanda. Kwa hivyo katika kipindi cha mwaka huu na mwaka jana tumeanza kidogo kidogo, lakini katika upande wa maendeleo pesa yetu ya kufanya shughuli nyengine ilikuwa ni kidogo, lakini natarajia mwakani serikali yetu itatuwezesha baada ya kuwa na miradi na mipango ambayo itahitaji tupatiwe fedha hizo.(*Makofi*).

Jengine Mhe. Naibu Spika, karafuu za Morogoro zipo zilikuja lakini Sheria ya Karafuu hairuhusu kununua nje ya Zanzibar. Kwa hivyo hizi karafuu zilikuwa magunia sijui mane yale, karafuu hizi hazikununuliwa ikabidi ziharibiwe. Lakini utaratibu tulioweka hatukubali kununua karafuu kutoka nje. Kwa hivyo yeyote atakayeleta karafuu kutoka Morogoro hiyo ni magendo ambayo tutayashughulikia kisheria. *(Makofi)*

Jengine Mhe. Naibu Spika, ni kwamba miche ilikuwa inapelekwa Tanga ni kweli. Tumepata kesi ile ya miche kupelekwa Tanga lakini pia suala la miche ya mikarafuu nayo inahitaji kazi maalum. Kwa hivyo napokea ushauri wa Mhe. Mwakilishi tutaufanyia kazi na Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, kwa sababu sasa hivi tatizo sio hilo, liliopo sasa hivi hata miche yenyewe ya mikarafuu sio mingi, tumetembelea sisi maeneo yote ya vitalu. Kwa hivyo kuna haja kwanza tuongeze miche ya mikarafuu, lakini tuisimamie vizuri zaidi. Jambo hilo tutalisimamia mwakani tutakuja kuona utaratibu mzuri zaidi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kuhusu takwimu za viwanda kama nilivyosema tumebadilisha utaratibu wa kukusanya takwimu. Lakini tatizo kubwa la viwanda, viwanda vingi hivi nilivyosema ni *informal* havijarasimiwa rasmi, wengine hatuvijui viko majumbani mwa watu, wanafanya fanya vitu vya ujasiriamali. Kwa hivyo kuna zoezi la kurasimisha hivi viwanda vidogo vidogo, tunataka kuvirasimisha ili vionekane katika utaratibu mzima wa kuweka hesabu na takwimu za viwanda. Kwa hivyo uko mradi ule wa MKURABITA tunahangaika nao, lakini nafikiri baadae mwakani tukija kwenye jitihada zetu tutazidi kuwa zaidi.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu kama nilivyosema takwimu nimeshazijibu, labda suala jengine ni kupandisha mambo ya bei, hili la bei sijalizungumza. Mhe. Naibu Spika, kama ninavyosema siku zote bei tunazisimamia, tunatoa bei elekezi na bei elekezi inatoka kutokana na kuangalia vigezo vitatu. Bei ya kutoka nje *A4B*, bei za *Insurance*, bei ya wachukuzi na mpaka viwango vyengine. Tunaangalia bei na tunasema hii ndio bei elekezi, atakayeuza chakula au chochote, vitu vitatu au vinne ambavyo muhimu, juu ya bei hii basi atakuwa anakwenda kinyume na utaratibu ambao tumejiwekea. Mpaka sasa hivi bado hii hali ni nzuri, tumeona mpaka sasa hivi bei zimekwenda vizuri kwa kweli hazikuharibika sana hazikupanda sana. Mkiangalia bei mwaka huu na wenzetu Tanzania Bara kulikuwa na utofauti mkubwa sana wa bei.

Jengine Mhe. Naibu Spika, ni lazima tumshukuru Mhe. Rais wetu Dkt. Ali Mohamed Shein na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa kuendelea maisha kipindi kirefu sana kutoa nafuu ya kodi kwa ajili ya kuweka bei zisiwe zimepanda sana. Mimi nasema kwamba tusiwe na wasi wasi bei tunaziendeleza hivyo hivyo tunazifuatilia. Kwa hivyo twende kwa mujibu ambao tuko, hatuwezi kurudi nyuma utaratibu wa zamani wa kuwa na Tume ya Bei. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, hoja zilizozungumzwa na Mhe. Dkt. Khalid nimeziunga mkono na amenisaidia sana kufafanua. Kuna hoja zilizozungumzwa na Mhe. Abdalla Maulid Diwani, zimezungumzwa pia na Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango. Lakini niseme jambo la Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakili kwamba suala la *AGOA*, sisi Zanzibar hatujaingia kwenye *AGOA* kwa sababu viwanda vyetu bado ni vichanga na inabidi tujipanga vizuri. Hata kule Bara hawajaingia *AGOA*, ingawa kuna Sera ya

AGOA tunashiriki kwenye vikao vya *AGOA* pamoja na Serikali ya Muungano, lakini bado kuna haja kubwa sana kukaza buti ili kuweza kuingia katika soko hili mahususi kwa ajili ya biashara zetu.

Mhe. Naibu Spika, michango yote iliyoulizwa kwa maandishi kama nilivyosema ni mizuri, wameniunga mkono na mengine ya ziada nimeshayajibu kwa pamoja. Labda niseme tu Mhe. Naibu Spika, nashukuru sana kwa michango ya Waheshimiwa Wajumbe, waliokuwa wametuuliza na nimejaribu kutoa ufafanuzi ili waweze kuelewa tunatoka wapi na tunakwenda wapi. *(Makofi)*

Sasa Mhe. Naibu Spika, nimalizie kwa kusema kwamba Wizara yangu na watendaji wangu kwa kweli wamejitahidi. Tulivyofika mwaka huu ukitupima, sio sawa na mwaka jana. Hata ukiangalia vile vile tulisema hapa kwamba uzalishaji katika viwanda umeongezeka kwa asilimia nzuri sana na tunatumaini kwamba mwaka huu, kwa sababu utaratibu wetu sera, sheria na kanuni mwaka huu tutaweza kuzimaliza zote na tutaanza vile vile kuangalia sasa sera nyengine za ziada.

Kwa mfano sera ya *Special Economic Zone* ama tunasema kwa Kiswahili labda tuseme kama *freeport,* tumeona huko nyuma ambapo aliuliza mmoja katika Wawakilishi, huko nyuma bidhaa zilikuwa rahisi hapa wakija watu kutoka nchi zote kununua, lakini kati kati baada ya kubadilisha utaratibu ikawa sasa hivi bidhaa kutoka Zanzibar zikifika Bara wanakuwa wanapata msukosuko. Lakini tunasema *Free Economic Zone* na hii *SEZ,* yote hii ni kusababisha kila mtu aje Zanzibar kununua bidhaa. Yeyote atakayeleta bidhaa kutoka nje atapewa ghala hapa, atapewa *facility* hapa na bei itakuwa nafuu, kutoka hapa yeye mwenyewe ajitegemee kwenda kuuza anakokwenda kuuza. Hiyo ndio sera

ambayo imo katika ile ripoti ya *SEZ* ambayo tunataka tuifanyie kazi na tutaileta sheria yake ikipitishwa, itakuja kwenye Baraza na kujadiliwa.

La mwisho kabisa alizungumzia kwamba sera zije hapa. Hilo mimi siwezi kulitolea maamuzi na serikali imesikia, kwa sababu huko nyuma zilikuwa zikija hapa lakini sasa ikiwa maombi turudishe tena sera hapa, basi serikali imelisikia na litafanyiwa kazi.

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko kwa majumuisho yako mazuri sana.

Waheshimiwa Wajumbe Mhe. Waziri ametoa hoja. Sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja hii wanyooshe mikono, wanaokataa. Wanaokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Baraza limejadili na kuikubali hotuba ya bajeti ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko. Sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili kuvipitisha vifungu vya matumizi vya wizara yangu. *(Makofi)*

KAMATI YA MATUMIZI

FUNGU R01 -WIZARA YA BIASHARA, VIWANDA NA MASOKO

Jumla Kuu **455,224,000**

FUNGU R01 -WIZARA YA BIASHARA, VIWANDA NA MASOKO

Kifungu PR0101

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana mama yangu Mhe. Waziri wa wizara hii kwa majumuisho mazuri sana, lakini kuna eneo katika mchango wangu nilisoma vizuri katika kitabu hiki wakati ule alipokuwa anaeleza nyenzo ambazo amezitumia katika kusukuma bajeti ya wizara yake. Lakini katika nyenzo moja muhimu ambayo mara nyingi tunaipata kwa kupitia mikutano ya *EAC* sikuiona na mchango ule nilipeleka mwisho kwa sababu nilikosa fursa ya kuchangia. Kwa hivyo sitomlaumu kwenye eneo hilo kwa sababu hakunijibu.

Mhe. Mwenyekiti, lakini katika kitabu kikubwa pia programu hii ya kuratibu mikutano ya majadiliano ya kibiashara kikanda na kimataifa haikuwekewa fedha. Sasa sijui nimuulize tu Mhe. Waziri katika eneo hili, kwa sababu mara nyingi kwenye *EAC* kuna masuala ya biashara, viwanda, fedha na uwekezaji na kuna sera yake maalum, naona haikutajwa ku-*support* bajeti yetu hii. Je, ni vipi tutaweza kushirikiana na wenzetu hawa katika maeneo haya.

Mhe. Mwenyekiti, naomba Mhe. Waziri anijibu katika eneo hili.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, kweli tukiangalia bajeti yetu ya nyuma tulikuwa tuna vipindi maalum kwa ajili ya shughuli za kuratibu mikutano na majadiliano ya kikanda na kimataifa. Lakini safari hii kwenye hii bajeti imebadilishwa kwa hivyo vyote hivi vimetiwa katika upande wa Idara ya Mipango na Sera. Kwa hivyo hizi fedha zitashughulikiwa katika Idara hii ya Mipango na Sera, ahsante.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, kwanza niendelee kumpongeze Mhe. Waziri. Katika nyenzo hizi ambazo amezionesha katika kitabu chake nyenzo nane. Kuna nyenzo hii ambayo niliishauri katika mchango wangu ule wa maandishi dakika za mwisho wa kuingiza yale makubaliano na majadiliano muhimu ya kibiashara kutoka *EAC*, baada ya nane ziwe tisa. Sijui hili Mhe. Waziri analionaje.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, suala zima la uratibu kuhusu majadiliano ya kibiashara ya kitaifa na ya kikanda yanasimamiwa na Ofisi ya Rais. Sisi tunaalikwa na kushiriki katika ile *component* yetu sisi. Kwa hivyo haya tuliyoyasema ni kwa upande wa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko, sio ya jumla wote kwa sababu ni kubwa, wanakuwemo na Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji na wengineo. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, mimi nimpongeze sana Mhe. Waziri, hili suala katika Jimbo lake la Jang'ombe lilivyokuwa Kwahani, sasa hivi nimekuwa mimi. Kwa hivyo sina mashaka naye.

Lakini katika mchango wangu nilimuuliza tu vipi kuhusu suala zima la Baraza la Biashara (*ZNBC*), na kiutaratibu kila mwaka linakuwa lifanyike mara moja na Baraza la mwisho la Biashara limefanyika mwaka 2004 ambalo ni Baraza la Biashara la nane, kuna la tisa lilitakiwa lije. Je, anieleze tu inakuwa vipi halafu tuendelee.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli suala lake nimeliona, lakini niliona Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango aliyazungumza kwa jumla mashirikiano yetu na sekta binafsi. Lakini ni kweli ilibidi Baraza la Zanzibar hili linasimamiwa na Ikulu Afisi ya Rais, lakini sisi ndio tuna *secretariat* na kilikuwa kikutane, kikao cha mwisho ilikuwa mwaka 2014, nafikiri mwaka 2015 kulikuwa na uchaguzi, kwa zile harakati za uchaguzi hatukuweza kukutana.

Lakini yakatoka maamuzi ya Serikali kwamba hili Baraza litizamwe tena. Je, linafanya kazi inayotakiwa kwa ufanisi, kwa sababu inaonekana kwamba hili Baraza limekuwa kama ni kituo cha wafanyabiashara kunung'unika mambo yao. Lakini Serikali haioni tabu lakini tuliona hata kama itakuwa wafayabiashara watakuwa wanazungumza mambo yanayohusu biasahra zao, lakini tuwe na ufanisi wa matokeo ambayo yatakuwa mazuri.

Kwa hivyo kwa uamuzi huo ikabidi tufanye utafiti na mapendekezo. La kwanza ilikuwa ni kufanya sheria na sheria hiyo imeshapitishwa Baraza la Mapinduzi na iko njiani kuja katika Baraza la Wawakilishi. Ndani ya sheria hiyo kuna mambo mengi ambayo katika kutizama yamependekezwa katika kikao cha mwisho ambacho ndio kikuwa cha Baraza ikiwemo pia Mabaraza ya Wilaya na Mabaraza ya Mikoa na kadhalika.

Kwa hivyo hivi sasa ilikuwa tufanye kikao cha Baraza lakini agizo tulilokuwa nalo tufanye kiao cha Baraza hili mwezi wa Juni/Julai. Lakini kwa sababu maandalizi yasingekuwa si ya ufanisi na wafanyabiashara wenyewe wameanza uchaguzi juzi, walikuwa na uchaguzi wana uongozi mpya. Kwa hivyo imebidi sasa hivi mkutano huo ufanyike pengine baada pengine ya mwezi wa Agosti au Septemba, baada ya wenyewe wafanyabiashara kusema kwamba wao watakuwa tayari, wametupa mapendekezo tunasubiri kukaa nao kuona tupange tarehe ngapi.

Lakini sisi kwa Serikali tumeshajitayarisha, tayari sheria ipo na kikao cha utekelezaji *secretariat* wameshakaa vile vile kuandaa jambo hili. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Tunaendelea.

Kifungu PR0101 Program Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Biashara	2,344,358,000
Kifungu PR0102 Program Kuu ya Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali	912,581,000
Kifungu PR0103 Program Kuu ya Ukuzaji na Uendelezaji wa Biashara	

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, bado naendelea kumwambia mama yangu pale Mhe. Amina wakati mchango wangu ulikwenda mwisho nilitegemea kuchangia moja kwa moja. Kwa hivyo hapa silaumu isipokuwa kuna suala la ile *Non Tarrif Barrier* (*NTB),* katika eneo moja muhimu la kuwasaidia wafanya biashara ni kuepukana na vikwazo visivyokuwa vya kiushuru ambavyo wanavipata. Nilitaka kujua ni jitihada gani za Serikali

katika kutatua changamoto hizi kupitia miongozo ile hasa ile ya *EAC* au Jumuiya ya Afrika ya Mashariki.

Mhe. Mwenyekiti, naomba ufafanuzi majibu.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Mhe. Miraji aliuliza suala hili lakini masuala yalikuwa mengi. Sasa ni kwamba suala zima la *Non Tarrif Barrier*, sisi kwa hapa Zanzibar kinachotusumbua zaidi ni kati ya sisi na Bara.

Kwa hivyo hiyo ndio ambayo imekuwa kikwazo kwetu, lakini sasa katika kuhangaika na tuna mradi huu wa pamoja wa mambo ya *Export* na Serikali ya Muungano, basi tumepata mfadhili wa kuweza kutushirikisha katika *process* nzima. Kwa sababu kule Bara kuna Kamati ya kurahisisha biashara kwa kuondosha hivi vikwazo ambavyo sio vya kodi. *Non Tarrif Barrier* ni kama vile vikwazo ambavyo si vya kodi. Kwa mfano mizigo inakwenda kama ya Zanzibar ikifika Bara inaambiwa viwango havijafika inaambiwa ufungue *agent*, unaambiwa ufanye nini, unazungurushwa zungushwa, hivyo ndio vikwazo anavyozungumza Mhe. Miraji.

Lakini pamoja na hayo kwamba hii Kamati ipo na Wajumbe wake ilikuwa hatukuwa tunashirikishwa kikamilifu. Sasa hivi tumepata kupitia *Chamber of Commerce*, kuna mtu wetu kutoka Zanzibar ambaye anasimamia kwenye Kamati hii kwa upande wa Zanzibar, yeye ndio kiongozi, kusimamia masuala yote ya *NTBS* na anashiriki vikao vyote vya *East Africa* na vikao vile vinavyofanyika kwa upande wa Serikali ya Muungano.

Kwa hivyo matarajio yetu sisi kwamba haya ambayo mapendekezo yatafanyiwa kazi kwa sababu tuna watu wetu ambao wanafuatilia. Vile vile juzi tu palikuwa na semina kuwafahamisha wafanyabiashara, zilikuwa semina mbili ili kuwafahamisha hiyo *NTBS* ndio nini na muelekeo wetu ni nini.

Kwa hivyo namuomba Mhe. Miraji Khamis Mussa afahamu kwamba sisi tumeligundua na tunalifanyia kazi na tunatarajia mwaka huu tunaweza kufika pahali pazuri ahsante.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa majibu lakini nipongeze pia ile azma ya serikali katika kutatua changamoto hizi, naomba tuendelee.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Mwenyekiti, niendelee kumsifu Waziri kutokana na maelezo yake mazuri lakini kidogo nataka ufafanuzi katika kifungu cha SR 010302, "Ushindani Halali wa Kibiashara na Kumlinda Mtumiaji". Hapa kidogo nilikuwa namuomba Mhe. Waziri atufafanulie kidogo kuhusu habari ya mtumiaji kama ikiwa ni sehemu moja ya afya ya binadamu kuhusu habari ya fidia kama Shirika au Kampuni italeta bidhaa au kiwanda kitatoa bidhaa ambayo itaweza kumuathiri au kuathiri mlaji. Sijui Waziri anatueleza nini kuhusu suala hili.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, kuhusu "Ushindani Halali wa Kibiashara na Kumlinda Mtumiaji", ni kweli kwa kawaida kampuni zile ambazo zinazotengeneza bidhaa wanatakiwa walipe fidia wale ambao waliumizwa kwa ajili ya kutumia vyakula hiyo, ni sheria ya kimataifa. Na sisi kwa upande wetu sasa hivi tunapitia utaratibu huu na Sheria tunaupitia kuona kwa kiasi gani tutaweza kumlinda mtumiaji wetu zaidi, kwa sababu sisi tusiangalie bidhaa

zinakotoka lakini tuangalie na bidhaa hapa hapa nchini zilizotengenezwa nchini, lakini pia na kule zinakotengenezwa nako vile vile wanatakiwa wawalipe wale ambao watumiaji. Hayo aliyoyasema ni kweli sheria za kimataifa inatakiwa wawalipe *compensation* kama mtumia bidhaa ambayo imewapa madhara.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nilikuwa maana yake ninamtahadharisha au natoa maoni yangu kwamba katika jumla ya sheria ambazo tutatunga basi tuweze kuweka za kimataifa ili kumlinda mlaji.Tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Tunaendelea.

Kifungu PR0103 Program Kuu ya Ukuzaji na Uendelezaji wa Biashara	1,469,461,000
Kfungu PR0104 Program Kuu ya Viwango na Tathmini ya Ubora	2,483,800,000
JUMLA KUU	**7,210,200,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Naibu Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha Makadirio ya Fedha ya Wizara yangu bila ya mabadiliko, sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza yako liyakubali makadirio hayo.

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe hoja imetolewa sasa niwahoji wanaokubaliana na hoja hiyo wanyooshe mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda.(*Makofi*)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Waheshimiwa Wajumbe na mimi nichukue fursa hii kumpongeza sana Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko kwa kupitisha bajeti yake vizuri sana, lakini pia nimtakie kila la kheri yeye na timu yake kwa utekelezaji wa bajeti ambayo tumeipitisha hapa leo.

Waheshimiwa Wajumbe baada ya kusema hayo naahirisha kikao hadi kesho saa 3.00 asubuhi.

(Saa 7.44 mchana Baraza liliahirishwa hadi tarehe 31/5/2017 saa 3.00 asubuhi)